

**Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)**

**BUNGE LA TANZANIA**

**MAJADILIANO YA BUNGE**

**MKUTANO WA KUMI NA MBILI**

**Kikao cha Arobaini na Sita – Tarehe 15 Agosti, 2008**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Anne S. Makinda) Alisoma Dua*

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:-**

Hotuba ya Bajeti ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

**MHE. ANNE K. MALECELÀ K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU:-**

Taarifa ya Kamati ya Miundombinu kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa Mwaka wa Fedha uliopita pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

**MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI KWA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:-**

Taarifa ya Msemaji wa Kambi ya Upinzani kuhusu utekelezaji wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kwa Mwaka wa Fedha uliopita, pamoja na maoni ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

**MASWALI NA MAJIBU**

### **Barabara ya Mpakani**

**MHE. HERBET J. MTANGI K.n.y. MBARUK K. MWANDORO** aliuliza:-

Kwa kuwa, barabara ya mpakani itokayo Jasini Kupitia Totohovu hadi Horohoro Mwakijembe na Hifadhi ya Taifa ya Mkomazi/Umba kupitia vijiji vya Kimuni na Ngomeni hadi Mnazi ni muhimu sana kwa ulinzi na usalama wa Taifa letu na kwa kukuza utalii, biashara na shughuli nyingine; na kwa kuwa ni kama barabara hiyo imetelekezwa:-

(a)Je, Serikali haioni umuhimu wa kuendeleza barabara hiyo ili kukidhi malengo hayo?

(b)Je, isingekuwa bora zaidi kwa barabara hiyo kuanzia Jasini ika-ambaa hadi Horohoro badala ya kuelekea Totohovu na baadaye kupitia Duga hadi Horohoro?

(c)Je, Serikali haioni kwamba sasa ni wakati muafaka wa kujenga barabara kutoka Daluni hadi Mwakijembe kuungana na barabara hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mkuu, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbaruk Kassim Mwandoro, Mbunge wa Mkinga, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa barabara ya mpakani ya Jasini kupitia Totonovu hadi Horohoro ni muhimu katika shughuli za ulinzi wa taifa letu pamoja na kukuza shughuli za utalii, biashara na shughuli nyingine kama vile usafirishaji wa mazao ya wananchi hadi kwenye masoko. Aidha, ufinyu wa Bajeti ya Serikali, ndio kikwazo cha baadhi ya barabara za mipakani kutofanyiwa matengenezo ikiwamo barabara ya Yasini – Totonovu hadi Horohoro.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya kutoka Yasini kupitia Mahandakini na Totonovu hutumika zaidi na wakazi wa vitongoji vya Jasini, Totonovu na Mahandakini kwa ajili ya biashara na kusafirisha mazao mbalimbali wakiwemo samaki ambao husafirishwa hadi Jijini Tanga. Barabara ya kuanzia Jasini hadi Horohoro kwa sasa haipo na inahitaji matengenezo makubwa na kujengwa upya.

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara hii ni ya kijiji inaviunganisha vitongoji vya Jasini, Mahandakini na totonovu. Barabara hii inafanyiwa matengenezo madogo madogo na wakazi wa vijiji hivyo. Barabara hii inapitika kwa shida majira ya mvua kutokana na kupita kandokando ya ufukwe wa bahari. Barabara hiyo huunganishwa na barabara

itokayo Zingibari kupitia Moa – Mayomboni – Totonovu hadi Mbuluni, yenyе umbali wa kilometra 12. (*Makofī*)

Kwa ujumla barabara hii inafanyiwa matengenezo ya mara kwa mara na Halmashauri ya wilaya ya Mkinga kwa kutumia fedha za mfuko wa barabara.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge, kuwa huu ni wakati muafaka wa kutengeneza barabara ya Daluni – Mwakijembe, yenyе urefu wa kilometra 27. Barabara hii inaweza kurahisisha mawasiliano kutoka tarafa ya Maramba hadi tarafa ya Mkinga na kuunganishwa na barabara ya Mwakijembe hadi kitongoji cha Mwakiburi ambacho kiko katika barabara kuu itokayo Tanga hadi Horohoro. Sehemu hii ya barabara huwa inafanyiwa matengenezo na Halmashauri ya wilaya ya Mkinga kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2008/2009 Halmashauri ya wilaya ya Mkinga, imetenga fedha kiasi cha 13,000,000/= kwa matengenezo ya mara kwa mara kilometra 20 na shilingi milioni 8.4 kwa ajili ya matengenezo ya sehemu korofí kilomita saba, kwa barabara ya Mwakijemba – Mwakiburu (Duga).

Sehemu ya barabara ya Daluni – Mwakijembe iko katika hali ya kutotengenezeka, *non maintainable condition*, hivyo kuhitaji matengenezo makubwa, *rehabilitation*. Tatizo lililopo ni upatikanaji wa fedha za kutosha kutengeneza barabara hiyo. Naishauri Halmashauri ya Mkinga kuweka kwenye Bajeti barabara hiyo ili kuondoa kero kwa wananchi.

**MHE. MOHAMED R. ABDALLAH:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri na kwa kuwa wilaya ya Mkinga, sasa hivi ni mpya na Halmashauri ya Wilaya inajitahidi kuona uwezekano inawasaidia vipi wananchi wake katika suala zima la miundombini.

Je, Mheshimiwa Waziri, haoni kwamba sasa Wizara kuna haja ya makusudi kuwaongezea fedha katika barabara hizi ili waweze kukomboka kwa haraka zaidi kama ilivyokuwa zamani, lazima waende mpaka Muheza?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Rished Abdallah, kama ifuatavyo:-

Serikali inafahamu kwamba wilaya ya Mkinga ni mpya na kwa mwaka huu imetengewa 278,000,000/= kwa ajili ya kujenga barabara zake. Lakini kwa sasa tunaangalia mtandao mzima wa barabara ya Mkinga kwasababu ni wilaya mpya ili katika Bajeti ijayo tuone kwamba tutawasaidiaje katika kuunganisha barabara zao. Barabara nyingi utakuta ni zile barabara za vijiji na hazijapandishwa hadhi kuwa barabara za wilaya. Kwahiyoo, tunaiomba wilaya ya Mkinga wafanye utaratibu kuzipandisha hadhi

hizo barabara ili ziwe za wilaya ili ziingie katika mfumo wa barabara ambazo zinahudumiwa na Halmashauri ya wilaya.

Na. 398

### **Watumishi Wanaokwenda Masomoni Nje ya Nchi**

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA** aliuliza:-

Kwa kuwa, imefahamika kwamba wapo watumishi wa serikali ambao hupelekwa nchi za nje kwa masomo, *scholarship*, na baada ya kumaliza masomo yao hawarudi nchini:-

- (a) Je, Serikali inaliambia nini Bunge, kuhusiana na jambo hili la Kahawa?
- (b) Je, ni hasara kiasi gani imepatikana tangu mwaka 1998 – 2008 kutokana na watumishi kutorudi nchini baada ya masomo yao?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mossy Suleiman Mussa, Mbunge wa Mfenesini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba wako watumishi wa Serikali ambao wamepelekwa nchi za nje kimasomo kupitia Wizara na Taasisi mbalimbali za Serikali ambao hawakurudi nchini kutoa huduma inayotokana na mafunzo hayo.

Takwimu zilizopo zinaonesha kuwa kati ya mwaka 1998 – 2008, takribani watumishi 35 waliofadhiiliwa kupata mafunzo katika nchi mbalimbali kama vile Marekani, Uingereza, Uganda na Afrika Kusini, na kadhalika hawakurejea nchini kama ifuatavyo:- ·

.	Wauguzi Waandamizi .....	17
.	Wataalamu wa Maabara.....	1
.	Waalimu wa Lugha .....	2
.	Wahadhiri katika Fani ya Uhandisi ....	3
.	Wahadhiri katika Fani ya Ualimu .....	2
.	Wataalamu wa Teknolojia ya Habari ..	2
.	Mtaalamu wa Jiolojia .....	1
.	Afisa Tawala .....	2
.	Mchumi .....	1
.	Mtaalamu wa Takwimu.....	1
.	Katibu Muhtasi .....	1
.	Mtaalamu wa Mazingira.....	1

· Mpishi kaika Makazi ya Viongozi.....	1
· Jumla .....	35

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulifahamisha Bunge lako Tukufu kwamba mtumishi asiporejea kazini baada ya masomo anahesabika kwamba ameacha kazi, *absconded*. Kutokana na kutokurejea Serikali inachukua hatua za kinidhamu kwa watumishi wote 35 ambao hawakurejea kazini kuanzia 1998 – 2008 kwa kuwaachisha kazi.

Ofisi yangu inaendelea kuchukua hatua ya kufuatilia ili kutambua watumishi wengine ambao bado taarifa rasmi za kutorejea nchini hazijapatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hatua hii, napenda kutoa wito kwa waajiri wote kuhakikisha kwamba kabla ya kuwaruhusu watumishi wao kwenda masomoni nje ya nchi, wajaze fomu za mkataba wa kuhudhuria mafunzo kama inavyoelekezwa katika Kanuni za Kudumu za utumishi wa Umma, *Standing Orders*, za mwaka 1994 kifungu G (15) na (16). Mkataba huo, unasisitiza umuhimu wa watumishi kurejea nchini baada ya kumaliza mafunzo yao kuongeza tija katika utendaji wao wa kazi.

- (b) Mheshimiwa Naibu Spika, hasara zilizopatikana ni pamoja na:-
- Upungufu wa watumishi kwenye kada ya Wahadhiri na Wauguzi Waandamizi.
- Ongezeko lisilo la lazima la Makadirio ya Bajeti ya mishahara ya watumishi mwaka hadi mwaka.
- Kuzorotesha utendaji kazi kwenye maeneo yanayohitajika kwenye kada za wahandisi na wauguzi na kada nyinginezo.
- Gharama kubwa ya kuwapata watumishi wapya kwa kutangaza nafasi zilizo wazi na kuajiri upya, na kadhalika.

**MHE. MOSSY SULEIMAN MUSSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, asante kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri, naomba kuuliza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Serikali, imekuwa ikitumia fedha nyingi sana kusomesha watumishi kwa maana ya kuboresha taaluma zao na kuja kuwatumikia Watanzania; na kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa adhabu hiyo ya kuwaachisha kazi. Je, kwa kuwa serikali ina mkono mrefu, hayo ndio maamuzi ya mwisho?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukubaliana naye kwamba ni kweli Serikali inapoteza hela nyingi sana katika kuwasomesha watumishi mbalimbali nje ya nchi.

Tunachofanya kama Serikali ni kuwafuatilia kwa karibu sana ili kuhakikisha kwamba wanarudi nchini, hiyo ni hatua moja. Lakini hatua ya pili pia kuongea nao pindi viongozi mbalimbali wanapoenda nchi za nje, kama mnakumbuka Mheshimiwa Rais, akikutana nao kule nchi za nje anawaeleza kwamba warudi nchini ili waweze kulitumikia taifa. Kwa hiyo, tunaendelea kuwafuatilia kwa karibu ili tuhakikishe kwamba wanarudi na kulitumikia taifa letu. (*Makofi*).

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kupewa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa, wapo Watanzania wengi sana, sina takwimu, wanafanya kazi nje ya nchi na wana marupurupu mazuri. Je, Serikali haioni kwamba umefika wakati kukaa nao na kuwaomba wawekeze mapato yao nchini ili nchi ipate fedha za kigeni kama wanavyofanya nchi ya Rwanda, nchi ya Uganda na nchi ya Kenya? (*Makofi*).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA(K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Musalika kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nakubaliana naye kabisa kwamba ni vyema tukawashauri wale wenzetu wawekeze ndani ya nchi. Lakini kama amefuatilia kwenye vyombo vyaya habari Mheshimiwa Rais, anapokwenda nchi za nje, anakaa na hao wenzetu ambaa wanafanya kazi nchi za nje na kuwaambia kwamba wawekeze katika nchi yetu. Nafikiri taarifa hizo wote tunazo kwamba Mheshimiwa Rais, anafanya kazi kubwa sana ya kuwa-*encourage* wale wenzetu waje wawekeze katika nchi yetu.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kunipatia nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa na kama alivyokiri mwenyewe Mheshimiwa Waziri, Serikali inatumia pesa nyingi sana kuwasomesha hawa watu huko nchi za nje na wakati huo huo wengine wanashindwa kurudi nchini. Kuna sababu gani ya Serikali kuendelea sasa kuwabembeleza kwenda kuongea nao wakati wame-*default*.

Kwanini tusiandike barua kwenye nchi wanazosoma baada ya kumaliza masomo yao nchi hizo zisiwaajiri? (*Makofi*).

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (K.n.y. WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Zambi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli hao wenzetu wanaenda kufanya kazi kule katika nchi za nje kwa ajili ya kutafuta maslahi, na kwa kweli hatuwezi tukawabana sana

kwamba wasiende kutafuta maslahi. Ni kama sisi Waheshimiwa Wabunge, tuna taaluma zetu, tumeamua kutoka kwenye taaluma zetu tumekuja kugombea kwenye ubunge. Pengine ni kwa ajili ya maslahi, pengine kwa ajili ya kuwakilisha wananchi. Kwa hiyo, mimi naona kwamba si vizuri kuwabana ili wasiajiriwe bali ni kuongea nao tu kwamba ni vizuri wakashafanya kule warudi kwenye nchi yao na vilevile wakipata marupurupu mengi warudi kuwekeza katika nchi yao. (*Makofi*).

Na. 399

### **Kupanda Kwa Bei za Vyakula**

**MHE. SAID J. NKUMBA K.n.y. AZIZA S. ALLY** aliuliza:-

Kwa kuwa bei ya vyakula imepanda kwa kasi kubwa sana kwa bidhaa kama sukari, mafuta ya kula na hata saruji:-

- (a) Je, Serikali inatoa tamko gani kuhusu upandaji wa bei hizo?
- (b) Je, ni nini sababu ya kupanda kwa bei ya vyakula pamoja na vitu vingine?
- (c) Je, Serikali ina mkakati gani madhubuti wa kuhakikisha kuwa bei hizo zinadhibitiwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI ( MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aziza Sleyum Ally, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa bei za vyakula zimepanda. Kupanda kwa bei za vyakula kumetokana na upungufu wa chakula hasa mahindi na mchele ndani na nje ya nchi. Ufumbuzi wa tatizo hili ni kuhakikisha kwamba tunajitosheleza kwa bidhaa muhimu hasa mazao ya chakula. Serikali kwa upande wake itatoa kipaumbele katika sekta ya kilimo ili mapinduzi ya kijani yaweze kutekelezwa kwa vitendo. Aidha, Serikali inawaomba pia wananchi kushiriki kikamilifu katika shughuli za kilimo. Tukiimarika katika uzalishaji kwa kiwango kikubwa tutapunguza mfumuko wa bei.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zifuatazo zimeonekana kuchangia kupanda kwa bei za vyakula pamoja na vitu vingine hapa nchini:-

(i) Mazao ya chakula hasa nafaka kwa baadhi ya nchi yametumika katika uzalishaji wa mafuta, *bio fuel*, hivyo kusababisha uhaba wa chakula.

(ii)Kupanda kwa bei ya mafuta katika soko la dunia kumesababisha gharama za usafirishaji wa bidhaa mbalimbali na hasa chakula kupanda.

(iii)Kupanda kwa gharama ya umeme hapa nchini kumesababisha pia kupanda kwa bidhaa zinazozalishwa viwandani.

(iv)Kukua kwa sekta ya ujenzi hapa nchini kusikoendana na uzalishaji kumeongeza mahitaji ya vifaa mbalimbali vya ujenzi.

(c) Mikakati iliyopangwa na Serikali ambayo kwa kiwango kikubwa itasaidia kudhibiti ni kama ifuatavyo:-

(i) Kusimamisha kwa muda uuzaaji wa mazao ya nafaka nchi za nje, hususan mahindi na mchele.

(ii)Kusimamisha kwa muda uuzaaji wa saruji nchi za nje.

(iii)Kipaumbele kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo kwa kuwekeza zaidi katika sekta ya kilimo. Uwekezaji huo utakwenda sambamba na kilimo cha umwagiliaji.

(iv)Kupitishwa kwa sheria ya petroli kumetoa fursa ya kuagiza mafuta kwa jumla. Hatua hii itapunguza ongezeko la mara kwa mara la bei ya mafuta na hivyo kutoa unafuu katika usafiri na usafirishaji.

(v)Kuendeleza mazungumzo na mwekezaji juu ya kuanzisha kiwanda cha saruji pamoa na kiwanda cha mbolea katika mkoa wa Mtwara.

(vi)Kuendeleza utafiti wa kuzalisha mbegu bora ambazo zitatoa mazao bora na kwa wingi na pia zinazohimili maradhi.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa naibu Spika, nashukuru sana kupata maelezo ya majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, lakini nina swali moja dogo tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa bidhaa zinazouzwa sehemu zilizo mbali na uzalishaji, kwa mafano sukari, sementi na batii, zinaongezeka bei kutokana na umbali na wa gharama za usafirishaji na kuwafanya wananchi walio mbali na maeneo ya uzalishaji kama maeneo ya Tabora, Mwanza, Shinyanga, kununua bidhaa hizi kwa bei kubwa sana. Sasa Serikali ina mpango gani ili kuleta uwiano wa bei ya aina moja aidha kwa kuweka ruzuku au kuwasaidia kupunguza kodi ili bidhaa zinaposafirishwa mtu aliyepo Kigoma aweze kununua sawa na mtu aliyepo Dar-es-Salaam? (*Makofii*).

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nkumba, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoeleza kwamba gharama za bidhaa mbalimbali zimepanda kutokana na mapungufu aidha yaliyoko ndani ya nchi na nje ya nchi na pia kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta. Kwa vyovyote vile, hata ukisema unataka kuondosha kodi kwa bidhaa hizo, bidhaa hizo kwasababu bei ya mafuta iko juu, usafirishaji utaongezeka, vyo vyote itakavyokuwa bidhaa hizo zitakuwa zina bei za juu kutokana na gharama za usafirishaji. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge, avute subira, hivi leo nimejaribu kuangalia katika soko la dunia bei ya mafuta sasa hivi inapungua na imefikia dola 115 kwa pipa na kuna matarajio itashuka zaidi. Hapo itakaposhuka basi gharama nazo vilevile zitaweza kupungua. (*Makofi*).

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, pamoja na bei ya mafuta kupungua duniani lakini hapa Tanzania bado, hakuna hata wakati mmoja bei hizo zimepungua napo katika Tanzania tumeona mapungufu hayo yaktokea.

Je, Serikali bado haina utaratibu wa kuona bei ya dunia inapopungua kwa mfano imepungua sasa hivi kama dola 35, bado Watanzania wanapata bei kubwa zaidi na kwa muda huo itaendelea hata itakapopungua mpaka chini zaidi. Kuna utaratibu gani wa Serikali kuhakikisha bei ya dunia inapopungua na hapa ndani ya nchi bei hiyo nayo inapungua? (*Makofi*).

**WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Naomba kuongezea majibu yaliyotolewa na Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Uchumi kwa Swali la Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulihakikishia Bunge lako na wananchi kwa ujumla kwamba Serikali kuititia Wizara ya Nishati na Madini, pamoja na taasisi ambazo zinaratibu na kusimamia masuala ya mafuta kuna utaratibu wake ambao tumekuwa na vikao vya kila mwezi.

Lakini pia *EWURA* kama ambavyo tumekuwa trukifua tilia kuititia vyombo vya habari wamekuwa wakitoa taarifa kwa umma kuonyesha mwenendo wa bei za mafuta. Lakini pia mwenendo kwa hali halisi kulingana na bei yake ilivyo katika soko la dunia.

Kwa hiyo, ninachosema ni kwamba kwa vile vipindi ambavyo mafuta yanakuwa yameagizwa na makampuni yetu hapa utaratibu upo wa kuhakikisha kwamba tunafua tilia. Ile bei inapobadilika kule kwenye soko la dunia, pamoja na kuzingatia gharama zilizoko hapa sisi bei yetu inakwendaje?

Kadiri inavyoshuka sasa hivi na juzi au jana kuna vyombo vya habari vimendika vimeliona hilo kwamba sasa hivi kwa kweli bei imeshaanza kushuka katika baadhi ya vituo na tunaendelea kuratibu hilo kuhakikisha kwamba kadiri inavyoshuka na sisi

tunahakikisha kwamba kama taifa tunanufaika na mabadiliko hayo. Ahsante sana (*Makofî*).

Na. 400

### **Kupanda Kwa Gharama za Maisha Nchini**

#### **MHE. STEPHEN J. GALINOMA** aliuliza:-

Kwa kuwa gharama za maisha kwa Mtanzania zimeongezeka sana na lindi la umasikini limeongezeka mara dufu, ambapo upandaji wa bei za mafuta na vyakula hapa nchini na nje ya nchi kama vile huko Haiti, Misri, Senegal na kwingineko unaripotiwa kuzitumbukiza nchi zinazoendelea kwenye machafuko; na kwa kuwa utaratibu wa soko huria umechangia sana tatizo hilo:-

Je, Serikali inatambua hali hii? Na haioni umuhimu wa kurejesha utaratibu wa awali wa kudhibiti na kupanga bei angalau za bidhaa za msingi?

#### **NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA UCHUMI (MHE. OMAR YUSSUF MZEE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha na Uchumi, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Stephen Jones Galinoma, Mbunge wa Jimbo la Kalenga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 22/7/2008 wakati nikijibu swalii Namba 266 la Mheshimiwa Juma Abdallah Njwayo, Mbunge wa Jimbo la Tandahimba, tarehe 30/07/2008 nikijibu swalii Namba 309 la Mheshimiwa James Philip Musalika, Mbunge wa Jimbo la Nyang'wale, nilitoa maelezo ya kina juu ya mfumuko wa bei kulikosababisha kupanda kwa gharama ya maisha kwa Mtanzania.

Kutokana na wananchi wengi kuguswa na hali hii lako Tukufu kuwa Serikali inatambua kuwa gharama za maisha zimeongezeka kutokana na kupanda kwa bei ya mafuta na chakula.

Kupanda kwa gharama za maisha kunakotokana na mfumuko wa bei ni eneo moja tu katii ya mambo yanayochangia kuongezeka kwa umasikini.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo mwaka 1996 Serikali iliamua kufuata mfumo wa soko huria baada ya kupata matatizo kwenye utaratibu wa awali wa kusimamia na kudhibiti bei za bidhaa mbalimbali.

Mfumuko wa bei katika mwaka 1995 ulikuwa ni 27.4% mwaka mmoja kabla ya kuanzishwa kwa utaratibu huo. Utaratibu wa soko huria umesaidia sana kushuka kwa mfumuko wa bei hadi kuwa tarakimu moja, *single digit*.

Kwa maana hiyo ni dhahiri kwamba kupanda kwa mfumuko wa bei kwa 9.3% kulikojitokeza mwezi Juni mwaka 2008 kutoka 7% mwaka 2007 hakujachangiwa na soko huria bali kumechangiwa na upungufu wa bidhaa za vyakula katiika soko la ndani na lile la nje hasa kwa mazao ya nafaka.

Pamoja na kupanda kwa bei ya mafuta duniani kulikosababisha usafirishaji wa bidhaa nazo kupanda.

Kwa hiyo kurejesha utaratibu wa awali wa kudhibiti na kupanga bei hakutasaidia sana kutokana na kwamba kuna uwezekano mkubwa kwa ushindani katika soko kuwa mdogo na hatimaye kupungua kwa bidhaa na kupanda kwa bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, njia muafaka ya kudhibiti bei ni kuhakikisha kuwa tunazalisha na kuitosheleza kwa bidhaa muhimu hasa chakula ambacho kinachukua karibu 60% ya mfumuko wa bei.

**MHE. STEPHEN JONES GALINOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza namshukuru sana Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na ya kitaalam. Nachukulia kwamba matokeo ya uzalishaji yatachukua muda mrefu kwani kilimo kama tunavyojuu haikupewa fedha za kutosha ili kuanzisha na kutekeleza azma yake ya *green revolution*.

Je, katika muda huo wa kati yaani *interim period* wananchi waendelee kuteseka wakati tunasubiri matokeo ya uzalishaji wa *green revolution*?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Stephen J. Galinoma la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwanza, nataka nimhakikishie kwamba nia ya Serikali siyo kuona wananchi wake wanateseka. Lakini nataka nimuhakikishie kwamba kilimo siyo suala la muda mrefu. Sasa hivi kuna mbegu za mahindi katika kipindi cha miezi mitatu au minne hadi sita tayari yanaanza kuvunwa. La msingi ambalo nimelisema na Serikali inasema ni kuhakikisha kwamba tunajitosheleza kwa chakula, tukiweza kujitosheleza kwa chakula hali yetu ya mfumuko wa bei itashuka kwa sababu chakula kinachukua takribani 60% kama 60% ya mfumuko inaweza ikashuka basi *definitely* na hali ya maisha vilevile inaweza ikaboreka.

**MHE. BENITO WILLIAM MALANGALILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Katika mwaka 1990 au 1992 Wakuu wa Mikoa wa Iringa, Mbeya, Rukwa na Ruvuma walikaa kujadili namna ya kutumia Mahindi yaliyokuwa mengi sana wakati huo. Hii ni kutokana na sababu bei ya Mbolea ilikuwa ya chini na Serikali ilikuwa inatoa ruzuku kubwa.

Sasa, kwa kuwa dunia nzima inasema kuna tatizo kubwa sana la chakula. Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba inatoa ruzuku kubwa ya Mbolea kiasi kwamba wakulima waweeze kuzalisha mahindi ya kutosha hususani katika hiyo Mikoa minne niliyoitaja?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. OMAR YUSSUF MZEE):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana naye kwamba kuna haja ya kutoa ruzuku ya mbolea kwa wananchi lakini nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hivi sasa Serikali 60% ni ruzuku hiyo bei ya mbolea unayoiona 60% ni ruzuku. Mkulima analipa 40%. Pale ambao uwezo wa Serikali utakapokuwa mzuri basi Serikali itakuwa haina budi kuweza kuliangalia suala hili ili uzalishaji wa vyakula uweze nao kuongezeka.

Na. 401

#### **Ufunguzi wa Chuo cha Afya Mpanda**

**MHE. SAID AMOUR ARFI** aliuliza:-

Kwa kuwa, katika mpango wa Maendeleo ya Afya, chuo kilichopo Mpanda kilipangwa kufunguliwa katika mwaka wa 2007/2008.

Je, mpaka sasa kwa nini Chuo hicho hakijafunguliwa?

#### **NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Said Amour Arfi Mbunge wa Mpanda kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Serikali ilikuwa na mpango wa kukifungua Chuo cha Mpanda katika mwaka 2007/2008 ili kuongeza wanafunzi watarajali katika kada ya Tabitu. Chuo cha Mpanda ni mionganoni mwa vyuo vitano vilivyofungwa mwaka 1995 kufuatia mabadiliko katika Sekta ya Afya yaliyoanza mwanzo mwa miaka ya tisini.

Lengo lilikuwa ni kuwa na idadi ya vyuo ambavyo Serikali ingeweza kuviedesha kwa ufanisi. Kutowana na ongezeko la mahitaji ya sasa ya watumishi katika Sekta ya Afya, na kufuatia Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi unaolenga kuwa na Zahanati katika kila kijiji na Kituo cha Afya kaika kila Kata, Serikali imeamua kuvifufua vyuo vyote vilivyofungwa kikiwemo cha Mpanda ili kuongeza idadi ya udahili na hivyo kuongeza idadi ya watumishi katika soko la ajira.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyoileza Bunge lako Tukufu katika Mkutano huu tarehe 5 Agosti, 2008 wakati nikijibu swali Na. 346 la Mheshimiwa Felix Ntibenda Kijiko, Mbunge wa Muhammadi, Chuo cha Mpanda ni mionganini mwa vyuo vinavyotembelewa na kufanyiwa ukaguzi uli kutathmini uwezekano wa kuvifungua mwaka 2007/2008. Kwa bahati mbaya chuo hicho hakikuwa katika hali nzuri ya kupeleka wanafunzi kwa mwaka 2007/2008, kwani mfumo wa maji takatatu na umeme vyote vilikuwa katika hali mbaya sana.

Aidha, madarasa na mabweni nayo yamechakaa. Kutowana na mazingira ya chuo hicho, Serikali haikuweza kukifungua. Naomba kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa Serikali imetenga fedha katika bajeti yake ya mwaka 2008/2009 ili kutekeleza hatua za mwanzo za ukarabati wa vyuo vyote vilivyo kuwa vimefungwa kikiwemo cha Mpanda.

**MHE. SAID AMOUR ARFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Naibu Waziri kwa majibu yake, siwezi kusema kwamba ni mazuri sana. Naomba anieleze sasa kwamba maelezo yaliyotolewa na Waziri wakati anawasilisha Bajeti yake ya Wizara ya Afya ya kufunguliwa kwa Chuo cha Mpanda na vyuo vingine si kweli kwamba vyuo hivyo sasa vinakarabatiwa?

Swali la pili, kwa sababu vyuo hivi vilikuwa vianze katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 na havikuweza kufunguliwa, fedha iliyokuwa imetengwa kwa ajili ya shughuli hiyo na fedha iliyotengwa mwaka huu. Je, atatuhakikishia kwamba Chuo hicho kitapokea wanafunzi mwaka huu?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Said Amour Arfi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, maelezo aliyokuwa ametoa Mheshimiwa Waziri wa Afya alipokuwa anawasilisha hotuba yake ni ya ukweli. Kama nilivyoileza katika jibu langu la msingi na kama Mheshimiwa Waziri aliyokuwa ameeleza alipokuwa anatoa hotuba yake ni kwamba vyuo hivi tulitarajia kwamba tungeweza kuvimalizia ili tuweze kuweka wanafunzi, kuvifungua na kufundisha wanafunzi.

Lakini kutowana na hali mbaya na kwa sababu vyuo hivi vinataka wanafunzi waende pale waweze kuwa katika mazingira mazuri na waweze kusoma vizuri hatuwezi kuwapeleka kama havijawa tayari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nataka niseme tu kwamba Serikali ina nia thabiti ya kuvitengeneza vyuo hivi na Chuo cha Mpanda kwa sababu sasa hivi ukarabati utakuwa unaendelea na ni wazi kwamba haiwezekani tukaanza leo na tukamaliza kesho, nataka tu Mheshimiwa Mbunge aaminii na tukubaliane kwamba kweli kabisa tutavitengeneza katika hali nzuri ili wanafunzi tutakaowapeleka pale watakuwa wanaishi katika mazingira mazuri na wasoma ili wapate kuwa Madaktari na Wauguzi wazuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. (*Makofii*)

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya na Ustawi wa jamii nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa hivi sasa kuna upungufu mkubwa sana wa wataalamu wa afya na wa kada mbalimbali, kwa mfano Wilaya ya Mpwapwa tu peke yake kuna upungufu wa watumishi 117 na kwa kuwa kwa maelezo ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuna vyuo vitano yaani Mpanda, Ngufu, Nachingwea, Kagemu Bukoba na Iringa;?

Na kwa kuwa, suala hili ni la muda mrefu tumeomba vyuo hivi vyote vifunguliwe ili tufundishe Waganga wa kutosha na kuwapeleka kwenye Zahanati zetu.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri pamoja na majibu yake atahakikisha kwamba vyuo hivi vinakarabatiwa haraka ili tupeleke wanafunzi wa kutosha kwa sababu utaratibu wa kujenga Zahanati unaanza katika Bajeti hii katika vijiji vyote?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa George Malima Lubeleje, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokuwa najibu maswali yote yaliyoulizwa hapa Bungeni, tunakubali kabisa kwamba upungufu ni mkubwa si kwa Mpwapwa tu lakini ni kwa nchi nzima lakini vilevile tumeshasema kwamba tumeshatenga fedha na kukaratabi kwa kweli kama nilivyo sema tena hatuwezi tukaufanya tena katika kipindi cha mwezi mmoja tukaona kwamba imemalizika na kuona kwamba tunaweza tukapeleka wanafunzi.

Lakini tunachoahidi kama Serikali ni kwamba tutafanya ukarabati vyuo hivi kwa sababu nia yetu kweli ni kuhakikisha kweli huu mpango wa MMAM unaboreka. Kwa hiyo, bila kuwa na watumishi na wafanyakazi na watumishi kupatikana hatutaweza kuukamilisha mpango huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Waheshimiwa Wabunge mtuamini kwamba Serikali imedhamiria na sisi tutafanya kadri ya uwezo wetu ili kuhakikisha kwamba vyuo hivi vyote vinafunguliwa ili kukidhi mahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nakuamini Mheshimiwa! Sasa tunaendeleo na Wizara ya Miundombinu Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi atauliza.

Na. 402

### **Hipic Fund kwa Ajili ya Kutengeneza Barabara**

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania ilibahatika kupata fedha kutoka *HIPIC FUND* kwa ajili ya kutengeneza Barabara za vijiji kwenye Mkoa wa Lindi na kwa kuwa, Barabara zilizoahidiwa kutengenezwa kwa fedha hizo ni Tingi – Kipatimu (km 50); Nachingwea – Kilimarondo (km60) Nachingwea – Liwale (km30) na Nanganga – Ruangwa (km60) zenye jumla ya kilometra 200 na kwamba zingetengenezwa kwa muda wa miezi 16 kuanzia mwaka 2006 hadi 2008.

Lakini hadi sasa Barabara hizo hazijakamilishwa na kila mwaka hupunguzwa kilometra za kujengwa kutokana na kupanda kwa vifaa vya ujenzi tangu pale mradi ulipoanza 2005-2008, badala ya kilometra 50 kwa Barabara ya Tingi, sasa ni kilometra 21, na ile ya Nachingwea sasa ni kilometra 35m Nanganga kilometra 45 na kufanya jumla ya yote kuwa kilomita 114 badala ya 200 iliyokusudiwa hapo mwanzo.

Kwa kuwa, upungufu huo wa urefu wa Barabara hizo unatokanana ucheleweshaji wa ufungaji wa tenda na kuchelewa kuanza kwa ujenzi hivyo kusababisha vifaa vya ujenzi kupanda bei. Je, hizi kilomita 86 zilizopungua kutokana na athari hizo Serikali itakuwa tayari kufidia kwa kuzijenga ili kutimiza azma ya wananchi ya kuwa na Barabara nzuri?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Serikali ilikusudia kuzifanya matengenezo Barabara za Mkoa zenyе jumla ya urefu wa kilometa 200 Mkoani Lindi kutokana na fedha za *HIPIC* katika mwaka wa fedha 2003/2004. Lakini kutokana na kupanda kwa gharama za Vifaa vya Ujenzi, ililazimu Serikali kufanya mabadiliko ya matengenezo ya Barabara kutoka km 200 na kuwa km 110 kwa kutumia gharama ya shilingi bilioni 5.161. Mabadiliko haya yaliathiri umblai uliokusudiwa katika kila Barabara na kufanya upungue kwa jumla ya kilometa 90.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya juhudhi mbalimbali za kutafuta fedha ili kuweza kufidia km. 90 zilizopungua katika mradi wa awali. Juhudi hizo ni pamoja na Serikali kutenga fedha kila mwaka ili kuzihudumia Barabara hizo. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Serikali ilitenga jumla ya shilingi milioni 207 ili kufanya matengenezo maalum ya km.4 katika Barabara ya Nachingwe – Liwale na mwaka huu wa fedha wa 2008/2009, jumla ya Shilingi milioni 616 zimetengwa ili kufanya matengenezo maalum ya km. 13 katika Barabara ya Nachingwe – Liwale. Vilevile, shilingi milioni 300 zimetengwa kwa ajili ya matengenezo maalum ya km. 10 kwenye Barabara ya Nachingwe – Kilimarondo.

Aidha, zabuni kwa ajili ya matengenezo ya Barabara ya Tingi – Kipatimu zilitangazwa na kufunguliwa tarehe 23 Mei, 2008. Baada ya uchambuzi wa zabuni hizi, hakukupatikana Mkandarasi aliyekidhi matakwa ya mkataba wa ujenzi wa Barabara hiyo. Hivyo Zabuni kwa ajili ya matengenezo ya Barabara ya Tingi – Kipatimu zitarudiwa kutangazwa mwezi huu wa Agosti, 2008.

**MHE. FATMA ABDALLAH MIKIDADI:** Mheshimiwa Naibu Spika, hapo mwanzo Barabara zote zilikuwa na Wakandarasi ninataka kupata maelekezo, Mkandarasi wa mwanzo wa Tingi – Kipatimu amechukuliwa hatua gani?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kifupi ningependa kujibu swali la Mheshimiwa Fatma Abdallah Mikidadi, kama ifuatavyo:-

Kwa Barabara hii ya Tingi – Kipatimu Mkandarasi wa awali alikuwa ni *D.B. Shapriya* ambaye kwa bahati mbaya sana bila taarifa aliacha kazi na akahamisha vifaa pamoja na wafanyakazi mwezi Desemba, 2007 bila ya kukamilisha Barabara hiyo ya Tingi-Kipatimu. Serikali kuitia *TANROADS* imechukua hatua chache kama ifuatavyo:-

Moja, imesitisha mkataba huo na *D.B. Shapriya* lakini namba mbili yake pia imeiomba Benki yake yaani Benki ya Mkandarasi huyu yaani *Exim Bank* imkate shilingi milioni 169 ambazo alikuwa amelipwa kama malipo ya awali.

Lakini pia *TANROADS* imeitaka benki kumkata jumla ya shilingi milioni 200 ambayo ni 20% ya gharama ya mradi huu.

*TANROADS* pia imeiandikia *CRB* yaani Mamlaka ya Usajili wa Wakandarasi kuwajulisha kuhusu tabia hii mbaya ambayo Mkandarasi huyu ameifanya ili Mamlaka ichukue hatua zake za kisheria.

Lakini kwa sababu ya tatizo hilo lililotokea Serikali sasa hivi inafikiria kum-*black list* Mkandarasi huyu ili asipewe tena kazi ya kujenga miundombinu ya Barabara.

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa, Barabara hiyo hiyo ya kutoka Nanganga kwenda Ruangwa kuna njia ya mkato ya kwenda Ndanda hadi Masasi. Barabara hii ni muhimu kwa sababu wagonjwa wengi wanatumia kwenda Ndanda Hospitali.

Je, Waziri na Wizara yake wana mpango gani wakuiboresha Barabara hii na hasa katika ujenzi wa daraja dogo pale Lukuledi pale katika maeneo ya Chinongo.

**NAIBU SPIKA:** Lakini Mheshimiwa Raynald A. Mrope ujue hili swali ni lingine kabisa.

Naibu Waziri naomba ujibu kwa kifupi sana kwa sababu likiwa *original* linapata majibu vizuri.

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ridhaa yako naomba kujibu swali la Mheshimiwa Raynald A. Mrope kwa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli hili swali ni jipya kabisa kwa kweli sikuweza kulitafakari na kuangalia mipango ambayo Serikali ilikuwa nayo wakati nakuja Bungeni. Kwa hiyo, nitampatia majibu Mheshimiwa Mbunge kwa maandishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Na. 403

### **Reli ya Kaskazini**

**MHE. OMAR SHABANI KWAANGW' K.n.y. MHE. MICHAEL LEKULE LAIZER** aliuliza:-

Kwa kuwa, Tanzania ni mionganini mwa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki na ina ushirikiano wa kibiashara na nchi nyingine; na kwa kuwa, tunayo Reli ya Kaskazini inayotoka Dar es Salaam – Tanga – Arusha lakini kwa sasa haitumiki:-

- (a) Je, ni sababu zipi zilizosababisha reli hiyo isitumike?
- (b) Kama bado kuna umuhimu wa kutumia reli hiyo, kwa ajili ya kusafirisha mizigo na abiria. Je, ni lini reli hiyo itafanyiwa ukarabati ili iweze kutumika?

**NAUBU WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, Mbunge wa Longido, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Reli ya Kaskazini inayoanza Dar es Salaam – Tanga - Arusha bado inatumika kwa kusafirisha mizigo. Usafirishaji wa abiria ulisitishwa kutokana na upungufu wa injini na mabehewa uliosababishwa na uchakavu na Shirika kushindwa kununua injini na mabehewa ya kutosha.

Aidha, pamoja na upungufu wa injini na mabehewa, sehemu hii ina ushindani mkubwa kwa njia ya ya mabasi hasa baada ya kuboresha kwa barabara na hivyo kufanya idadi ya abiria waliohitaji huduma ya reli kupungua sana.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia umuhimu wa wa kutumia reli hasa kati ya Dar es Salaam – Tanga na Arusha, Mkodishaji *TRL* alianzisha tena safari za treni kubeba saruji kutoka Kiwanda cha Tanga kwenda Mwanza na Kigoma tarehe 5 Juni, 2008. Aidha, *TRL* inatarajia pia kuanzisha ubebaji wa Saruji kutoka Tanga kwenda Moshi na Arusha kuanzia leo (15/8/2008).

Kutokana na umuhimu wa reli hiyo, Mkodishaji alifanya kikao na wateja wakubwa pamoja na wazalishaji mjini Arusha mwishoni mwa mwezi Julai, 2008 ili kuwashakikishia wateja hao urejeshwaji wa huduma hiyo ya usafiri wa reli na hivyo kuwashimiza waanze kusafirisha mizigo yao kwa njia ya reli.

**MHE. OMAR SHABANI KWAANGW’:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili ya nyongeza.

La kwanza, sababu ambazo amezitaja Mheshimiwa Waziri za kusitisha usafirishaji wa abiria kwa reli hii ni uchakavu wa mabehewa ya injini lakini vilevile ushindaji wa njia ya barabara.

Je, Mheshimiwa Waziri anataka kutuambia kwamba sasa usafiri wa abiria kwa reli hii hautafufuliwa tena?

La pili, kama sababu za ushindani zinaweza kusitisha usafirishaji wa abiria, Mheshimiwa Waziri anataka kutuambia kwamba ipo siku itatokea kwamba njia ya barabara itakapokuwa imeboreshwa kati ya Dodoma na Mwanza kwamba usafirishaji wa abiria nao utasitishwa kama ulivyofanywa kwa njia? (*Makofi*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Omar Shabani Kwaang' kwa kifupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nilivyojibu katika swal la msingi kwamba Serikali kupitia shirika la *TRL* inafanya juhudu kuimarisha na kuboreshanjia za usafiri wa Reli maana ni usafiri muhimu na njia kuu pamoja na njia zote za matawi zimeanza kufanyiwa kazi na karibu njia zote za matawi zimefunguliwa na Serikali itaendelea kuhudumia usafiri huu ili kuuboresha na kuhakikisha kwamba unakidhi mahitaji ya usafiri ya usafiri wa mizigo mikubwa na usafiri wa masafa marefu nchini Tanzania kwa sababu ndiyo usafiri pekee ambao ni rahisi kushinda usafiri wa aina nyingine nchini.

**MHE. KAIKA SANING'O TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kumipa nafasi niulize swal dogo moja la nyongeza.

Kwa kuwa, kiwanda cha Minjingu kimeanza uzalishaji wa mbolea aina ya *Ammonium Sulphate*. Je, katika siku zijazo Serikali haina mpango wa kufanya *extension* ya reli hii ya Kati kutoka Arusha kuja Minjingu kwa ajili ya kubeba mizigo hiyo na kuuza nchi za jirani ambazo tuna Ushirikiano nazo kibashara?

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swal la nyongeza la Mheshimiwa Kaika Saningo Telele, kama ifuatavyo:-

Serikali ina mpango wa kujenga miundombinu kwa ajili ya kusafirisha mbolea ile ya Minjingu na pia kujenga *extension* ya Reli kwenda *Lake Natron* kwa ajili ya mradi wa magadi katika eneo hilo. Kwa hiyo, Serikali sasa hivi inafanya majadiliano na nchi mbalimbali ilikukweza kupata ufadhili kwa ajili ujenzi huo.

Swali Na. 404 Liliondolewa na Muuliza Swal Mheshimiwa Kidawa Hamid Salehe.

## **Kujenga Nyumba kwa Ajili ya Askari Polisi**

**MHE. RIZIKI OMARI JUMA** aliuliza:-

Kwa kuwa mwaka 2007/2008 Serikali iliahidi Bungeni kuwa, itajenga ghorofa za kuishi Askari Polisi Dar es Salaam na Zanzibar (Unguja na Pemba):-

(a)Je, Serikali itawafikiria lini Askari wanaofanya kazi huko vijijini ambako hata nyumba za kupanga ni za shida?

(b)Kwa kuwa, nyumba ya kuishi Askari wa Kituo cha Pongwe Mkoani Tanga iko katika hali mbaya sana. Je, Serikali ina mpango gani wa kuwajengea nyumba nyingine ili waondokane na adha hiyo?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI – (K.n.y.  
WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Riziki Omar Juma, Mbunge Viti Maalum, lenye sehemu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba mwaka 2007/2008 Serikali iliahidi Bungeni kuwa itajenga nyumba za ghorofa za kuishi Askari Polisi Dar es Salaam na Zanzibar. Ujenzi wa maghorofa hayo umeanza katika Kambi ya Barabara ya Kilwa Jijini Dar es Salaam, Unguja na Pemba. Lengo la Serikali ni kujenga nyumba za kutosha kuwawezesha Askari Polisi wote nchini wanaofanya kazi katika vituo vya Mijini na vijijini wakae katika Kambi. Lakini nia hiyo ya Serikali inakwamishwa na ifinyu wa Bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la ujenzi wa makazi ya Askari wetu ni jukumu ambalo Serikali inalitilia maanani sana.

Aidha, Serikali imeona umuhimu wa kushirikisha taasisi za fedha hapa nchini ili kusaidia ujenzi wa makazi ya Askari wetu. Hivi sasa Serikali imeingia mkataba na *NSSF* kujenga maghorofa 60 katika Jiji la Dar es Salaam pia Unguja na Pemba. Serikali inaendeleza majadiliano na taasisi mbalimbali za fedha ili nazo vilevile zisaidie ujenzi wa makazi ya Askari.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kwamba hatutaweza kuwajengea nyumba za kutosha Askari wote kwa mara moja lakini zoezi hili litafanyika kwa awamu kadri raslimali inavyoruhusu. Sambamba na Serikali kuendelea kutenga fedha katika Bajeti zake za maendeleo za kila mwaka kwa ajili ya ujenzi wa nyumba za Askari, lengo la Serikali ni kutatua tatizo la makazi kwa Askari wote hadi wa vijijini zikiwemo nyumba kwa ajili ya Askari wa Kituo cha Polisi cha Pongwe, Mkoani Tanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia nafasi hii kutoa wito kwa wananchi na wadau mbalimbali kushirikiana na Serikali katika ujenzi wa nyumba za Askari Polisi kama wanavyoshiriki katika kujenga nyumba za Watendaji wengine wa Serikali.

**MHE. RIZIKI OMARI JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwanza nimshukuru Mheshimiwa Waziri wa Ardhi aliyejibu kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani, jinsi alivyonijibu kwa ufasaha. Lakini naomba nimwulize swalii moja tu dogo la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kituo cha Polisi cha Pongwe Askari wake walikuwa wanaishi katika nyumba ambayo ilikuwa ni zahanati hapo awali. Lakini sasa hivi jengo hilo limekuwa bovu kiasi cha kutisha, linavunja, vigae vimevunjika mpaka zile nyaya za umeme zimeoza askari hulazimika kukaa chini ya miti muda mrefu sana.

Je, Mheshimiwa Waziri haini kwamba kuna haja ya kuliangalia kwa jicho la huruma tatizo hili na kufanya ukarabati wa nyumba hiyo angalau kufidia muda huu ambaa Askari wanaishi na huku Serikali inafanya mazungumzo na taasisi za fedha ?

Mheshimiwa Spika, nakushukuru.

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI – (K.n.y.)**  
**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya ndani ya Nchi napenda kujibu swalii la nyongeza la Mheshimiwa Riziki Omari Juma, Mbunge Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tatizo la makazi ya Askari Polisi, tatizo la uchakavu wa nyumba za Askari ni kubwa sana, hapa kila Mbunge angeweza akasimama akasema hilo hilo alilolisema Mheshimiwa Riziki Omari Juma. Ndiyo maana katika jibu langu la msingi nikasema kwamba Serikali kwa sasa hivi inafanya jitihada kubwa kabisa kujenga vilevile na kukarabati.

Mwaka huu wa fedha zimetengwa shilingi bilioni 7.8 na sehemu ya fedha hizo zinakwenda kukarabati nyumba za Askari. Lakini kwa sababu ni nyingi mno hazitafika kila mahali. Kwa hiyo, ninamwomba Mheshimiwa Mbunge avute subira na Pongwe vilevile tutafika.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuuliza swalii moja la nyongeza.

Kwa kuwa, kwa kweli Askari wetu wanafanya kazi nzuri na wananchi wanajua kabisa Askari wetu wanafanya kazi nzuri pamoja na kuishi mahali pa ajabu ajabu.

Serikali haioni kwamba ni muhimu ifanye *operation* nchi nzima kuwashirikisha wananchi wao watoe mabati na vifaa vingine ili wananchi wasaidie kufyatua matofali na kujenga?

**WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI (K.n.y.)**  
**WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa kutambua kazi nzuri inayofanywa na Jeshi letu la Polisi pamoja na kwamba katika mazingira magumu lakini wanafanya kazi nzuri. Tunashukuru kwa shukrani ambazo Mheshimiwa Mbunge amezitoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu *operation* ya kujenga nyumba za Polisi ni wazo zuri na ndiyo maana katika jibu langu la msingi nilitoa wito kwa wananchi nchi nzima kwamba jinsi ambavyo wanajitolea kujenga nyumba za Walimu, Madaktari na kadhalika tunaomba vilevile waone na hawa Polisi nao ni watendaji wa Serikali, watendaji wa umma. Kwa hiyo, washirikiane. Kuna baadhi ya maeneo wameanza na nawashukuru sana, wamefyatua matofali, wanaanza kujenga, wanaomba tu bati na mbao.

Kwa hiyo, naomba na kule Iramba waanze, wakianza kufyatua matofali na kuanza kujenga, wakaomba tu bati na mbaao nadhani Wizara itakuwa tayari kushirikiana na nao.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante ingawa muda umekwisha lakini tuna dakika zile za kulipia. Kwa hiyo, tunaendelea na swali lakina Wizara ya Nishati na Madini. Mheshimiwa Clemence Lyamba atauliza.

Na. 406

### **Ulipaji wa Ankara za Umeme – Mikumi**

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA** aliuliza:-

Kwa kuwa wateja wanaotumia umeme katika Mji Mdogo wa Mikumi wanalazimika kutumia gharama ya zaidi ya Sh. 3,500/= kusafiri umbali wa kilomita themanini kwenda Kidatu na kurudi kwa ajili ya kulipia ankara za umeme:-

Je, Serikali inasemaje kuhusu kuwaelekeza *TANESCO* kuweka *computer* moja Mjini Mikumi ili wateja wake walipe ankara zao hapo Mikumi badala ya kuwabebesha mzigo wa gharama zisizo za lazima wakati gharama ya umeme tayari imepanda?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Clemence Beatus Lyamba, Mbunge wa Mikumi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua kuwepo kwa tatizo la ulipaji wa ankara za umeme katika Mji Mdogo wa Mikumi linalosababisha wananchi wa eneo hilo kusafiri umbali mrefu kwenda Kidatu kulipia ankara za umeme.

Licha ya Mji Mdogo wa Mikumi ambaa una wateja wanaotumia huduma ya umeme wapatao 570 kuwa na ofisi za *TANESCO*, imekuwa vigumu kwa shirika kuweka miundombinu ya ofisi kama kompyuta kwa ajili ya ulipaji wa ankara za umeme katika ofisi hizo kama alivyoshauri Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu ya kutokutolewa huduma hiyo katika Mji Mdogo wa Mikumi ni kutokuwepo kwa Benki katika mji huo. Hata hivyo, ili kuwaondolea usumbufu wananchi wanaotaka kulipa ankara za umeme, kila Ijumaa ya mwisho wa mwezi wafanyakazi wa Idara ya Mapato *TANESCO* kutoka Kilombero hufika Mikumi ili kupokea malipo ya ankara kutoka kwa wateja.

Siku ya kulipa ankara hutangazwa mapema kuititia matangazo yanayobandikwa katika ofisi ndogo ya *TANESCO* Mikumi, vituo yva mabasi na kwa vipaza sauti ili wateja husika waweze kuijandaa na kuitumia siku hiyo kikamilifu kwa ajili ya kulipa ankara za umeme. Utaratibu huu umeanza miezi mitano iliyopita.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali hii kwa kiasi fulani imeondoa usumbufu kwa wateja wa umeme wa Mikumi kwenda kulipia bili zao za umeme Kidatu. Napenda kumshukuru na kumpongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia suala hili kama mojawapo ya kero zinazowakabili wananchi wa Jimbo lake la Mikumi.

**MHE. CLEMENCE B. LYAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi. Pamoja na majibu mazuri kiasi ya Mheshimiwa Naibu Waziri ambayo hayakidhi kuondoa kero niliyioieleza katika swali langu, nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri ana taarifa kwamba muda unaotolewa na Idara ya Mapato *TANESCO* Kilombero wa kulipa *bill* pale mikumi kwa wateja 570 waliotapakaa katika maeneo mbalimbali hautoshi kuweza kuwafanya wateja wale kulipa *bill* zao kwa wakati na pia idara hiyo siyo *regular* katika kuwasili kwa siku wanazotangaza?

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, swali la pili, Serikali inaonaje kama utaratibu ungeingiwa baina ya *TANESCO* na benki ya *SACCOS* ambayo inaendeshwa vizuri pale Mikumi kuweka utaratibu ambapo wateja wanaweza kulipia kwenye ile *SACCOS* au kuwawekea hata LUKU ili kuondoa na kuifuta kero hii moja kwa moja?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kuwafolenisha wateja mia tano sabini kwa siku moja ya mwezi kulipa ankara zao ni kero ya aina fulani.

Lakini labda niseme tu kwamba, katika utaratibu huu tofauti na ule wa kuwapeleka kilomita thelathini na tano mwendo mmoja na thelathini na tano kurudi kutoka Kidatu, mapato yaliyobadilika katika kukusanya pale pale Mikumi Mjini ni kwamba mwanzoni walikuwa wanakusanya kama milioni saba kwa mwezi na sasa wanakusanya kiasi cha milioni kumi na mbili.

Pamoja na hayo naomba nimkumbushe Mheshimiwa Mbunge na Waheshimiwa Wabunge kwamba, wakati tunapitisha sheria ya umeme hapa mwezi wa Nne, moja ya masharti mliyotupatia ni kwamba *TANESCO* lazima wafanye mikakati ya makusudi ya kuboresha *customer care* kwa maana ya kwamba huduma za wateja, kama wateja wanalipa basi na *TANESCO* nao lazima waboreshe huduma hiyo.

Kwa hiyo, naomba nilichukue suala hilo na niwakabidhi *TANESCO* kama moja ya changamoto ambazo wanazo katika kuwapatia huduma bora zaidi wateja, sio wa Mikumi tu isipokuwa wote wanaopata umeme na kuulipa kwa wakati unaotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, utaratibu uliokuwepo sasa hivi ni kwamba, *TANESCO* wameingia mkataba na benki ya *NMB* na pia malipo yanaweza kufanywa kupitia benki ya *CRDB*. Hatufahamu kama *TANESCO* kwa tathmini yao wanaweza kupokea malipo kupitia *SACCOS*. Hata hivyo, nadhani hilo ni wazo zuri na naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalipokea, tunakwenda kuwakabidhi *TANESCO* walifanyie utafiti kwa lengo la kumaliza kero hii ya wateja kulipa ankara zao kwa adha inayowapata. Hili suala la *LUKU* hakuna *vending machine* Mikumi na *infrastructure* ya miundombinu ya kulipia kupitia utaratibu wa *LUKU* haupo lakini naomba pia niutumbukize katika utaratibu ule ule wa *TANESCO* kuboresha huduma zao kwa wateja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge maswali yamekwisha na muda umekwisha. Sasa naomba tuwatambue wageni wetu.

Waheshimiwa Wabunge wageni waliopo Bungeni asubuhi hii ni Balozi wa Sweden nchini Tanzania Mheshimiwa Staffan Herrstrom, *can you please raise up*, karibu sana Dodoma na nchini kwetu. (*Makofî*)

Halafu tuna wageni kumi na sita wa Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ambao wameongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo ambaye ni Dr. Naomi Katunzi, naomba asimame. Ahsante. (*Makofî*)

Pia tuna Mkurugenzi Mkuu Profesa John Mkoma; Mkuu wa Taasisi Profesa John Agent Kandoro; Mkurugenzi Mkuu wa Tume ya Nguvu za *Atomic* Ndugu Abraham Nyanda. Ahsante sana tumefurahi kuwaona. (*Makofi*)

Halafu tuna watumishi arobaini na nane kutoka Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia wakiambatana na kiongozi wa msafara Profesa Msambichaka, ndiye *Principle* na wengine wote msimame. Kwa niaba yao wamesimama wachache. (*Makofi*)

Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Naibu Waziri wa Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ana mgeni wake ambaye ni mtoto wake anaitwa Khamis Maulid. Karibu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Margareth Sitta, Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto ana wageni wake ambao ni Mheshimiwa Diwani kutoka Wilaya ya Ilala, ameongozana na wajasiriamali. (*Makofi*)

Kwanza nianze na Mheshimiwa Diwani Ritha Kabati na Bi Berinda Miringo na Bi Shamsa Danga. Karibuni sana.

Tuna wageni wa Mheshimiwa Profesa Mwalyosi ambao ni Waheshimiwa Madiwani wa Halmashauri ya Ludewa, Zebedayo Mgaya na Mathew Kongo. Karibuni sana. (*Makofi*)

Halafu tuna wageni mia moja na ishirini na sita wa Mheshimiwa George Lubeleje ambao ni wanafunzi na Walimu kumi kutoka shule ya msingi Chazungwa. Wasimame walipo, hawapo hapa labda wapo kwenye ukumbi mwingine.

Hawa Waheshimikwa Wabunge wametoka Mpwapwa. Mpwapwa kama mnavyofahamu ni mbali. Kwa hiyo, wamechelewa. Tuna Wanasheria kumi na tano kutoka Tanganyika *Law Society*. Naomba wasimame walipo, nadhani wapo ukumbi mwingine.

Tunao wanafunzi thelathini kutoka shule ya msingi Santhome, wasimame na Walimu wao. Ni kundi lingine tena la Santhome.

Tuna wanafunzi thelathini kutoka shule ya msingi Ipagala B na Walimu wao, wasimame. Ahsanteni sana. Ninyi wa Dodoma Bunge ni lenu kwa hiyo mnaweza kuja kila wakati.

Matangazo ya kazi za Kamati mbalimbali. Waheshimiwa Wabunge jana Mheshimiwa Spika, alitangaza kwamba Kamati ya Uongozi na Tume wangekutana saa saba mchana huu.

Lakini leo ni Ijumaa, watu wengine watakuwa kwenye ibada. Kwa hiyo, badala ya saa saba tutakutana saa nane na nusu katika Ukumbi wa Mikutano wa Spika. Kwa hiyo, wajumbe wote wanaarifiwa hivyo.

Mheshimiwa George Malima Lubeleje, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria na Utawala anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba kutakuwana kikao kitakachofanyika saa tano leo asubuhi katika ukumbi Na. 428.

Mheshimiwa Hassan Khatib, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Ardhi, Maliasili na Mazingira anaomba niwatangazie Wajumbe wa Kamati hiyo kwamba leo saa tano asubuhi kutakuwa na kikao cha Kamati katika Ukumbi Na. 231.

Mheshimiwa William Shellukindo yeye ni Mratibu wa *BR*C, anaomba niwatangazie wanachama wa Bunge *Range Club* kwamba, zoezi la kulenga shabaha litafanyika Jumamosi kesho tarehe 16 Agosti, 2008 Makutupora JKT kuanzia saa tatu asubuhi. Kwa hiyo, mnaondoka hapa saa tatu asubuhi hapa.

Wanachama wote wa *club* hiyo wanaombwa kukutana leo tarehe 15 Agosti, 2008 kwenye Ukumbi wa Msekwa kuanzia saa kumi jioni, nadhani kupanga safari yao ya kesho.

Halafu Mheshimiwa Mwenyekiti wa *Bunge Sports Club*, Naibu Waziri Mheshimiwa Joel Bendera anapenda niwatangazie kwamba kesho Jumamosi tarehe 16 Agosti, 2008 saa kumi jioni timu zetu za Bunge zinacheza michezo ya kirafiki na *football* watacheza na *Mtwara Veteran* halafu *Netball* watacheza na *Dodoma Veterans*. (*Makof*)

Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Wabunge, Mama Kippa anaomba niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba kesho tarehe 16 Agosti, 2008 kuanzia saa moja jioni kutakuwa na tafrija katika ukumbi wa *basement* hapa Bungeni kule chini, watakaota burudani ni bendi ya Twanga Pepeta na *Hammer Q*.

Kwa hiyo, burudani hii imeletwa kwa hisani ya kampuni ya ZAIN wote mnakaribishwa.

Waheshimiwa Wabunge matangazo yamekwisha tuendelee na ratiba nyingine. Katibu endelea na *Order Paper*. (*Makof*)

## HOJA ZA SERIKALI

### **Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009 – Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia**

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa iliyowasilishwa leo hapa Bungeni na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu, Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga inayohusu Wizara yangu, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu sasa likae kama Kamati ili liweze kupokea, kujadili na hatimaye kuitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Taasisi zake kwa mwaka wa fedha 2008/2009.

**NAIBU SPIKA:** Samahani mtoa hoja, kuna tangazo hapa lile lililotangazwa na Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria, kumbe zinatakiwa Kamati mbili zikutane ya Katiba, Sheria na Utawala na Kamati ya Maendeleo ya Jamii. Kwa hiyo, saa tano mtakutana kule chumba Na. 428.

**WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru kwa namna ya pekee Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa heshima kubwa aliyonipa kwa kunitfea kuongoza Wizara hii.

Aidha, naomba kutumia fursa hii, kumpongeza kwa dhati kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Afrika na Mlezi wa Chama cha Wabunge wa Jumuiya ya Madola yaani *CPA* kwa kipindi cha mwaka 2008/2009. Hii ni heshima kubwa kwa Tanzania na Afrika kwa ujumla. Napenda pia kumpongeza Mheshimiwa Dr. Ali Mohammed Shein, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kumsaidia na kumshauri Rais kwa hekima katika utekelezaji wa majukumu mazito aliyonayo.

Aidha, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Mizengo Kayanza Peter Pinda, Mbunge wa Mpanda Mashariki kwa kuteuliwa na kuitishwa na Bunge hili Tukufu kuwa Waziri Mkuu wa 10 wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Napenda pia kuwapongeza Waheshimiwa Mawaziri wenzangu waliopewa nyadhifa za kuongoza Wizara mbalimbali katika Serikali hii ya Awamu ya Nne.

Aidha, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika kwa kuteuliwa kuwa Rais wa Chama cha Mabunge ya Jumuiya ya Madola (*CPA*). Pia nakupongeza wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa jinsi unavyomsaidia kwa dhati Mheshimiwa Spika katika kuendesha kwa ufanisi mkubwa shughuli za kila siku za Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuungana na Waheshimiwa Wabunge wenzangu kumpongeza Mheshimiwa Benedict Ole Nang'oro, kwa kuchaguliwa kwake kuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto. Ushindi alioupatata umeonyesha imani kubwa

waliyonayo wananchi kwa Chama cha Mapinduzi na kwake pia. Aidha, nawapongeza Waheshimiwa Al-Shaymar Kwegyir na Mchungaji Dr. Getrude Lwakatare, kwa kuteuliwa kuwa Wabunge wa CCM.

Vilevile, napenda kuwashukuru sana wananchi wa jimbo langu la Kilolo na uongozi wa Wilaya ya Kilolo kwa ujumla kwa kuendelea kunipa ushirikiano wa dhati katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kuleta maendeleo katika Jimbo letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa namna ya pekee kabisa, namshukuru mke wangu Violet pamoja na familia yangu kwa jinsi wanavyonipa moyo na ushirikiano wa dhati katika utekelezaji wa majukumu yangu ya kila siku.

Aidha, napenda niungane na Waheshimiwa Wabunge, ndugu jamaa na marafiki katika kuwafariji na kuwapa pole familia, ndugu na wapiga kura wa marehemu Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe (CHADEMA) aliyekuwa Mbunge wa Tarime aliyefariki dunia kwa ajali ya gari usiku wa tarehe 28 Julai, 2008 wakati akitokea Dodoma kuelekea Dar es Salaam; Mheshimiwa Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Kiteto, Mbunge wa Chama cha Mapinduzi na Mheshimiwa marehemu Salome Mbatia, aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM). Mwenyezi Mungu azilaze roho ya marehemu mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kutoa shukrani zangu za dhati kwa wale wote walioniwezesha kutekeleza majukumu ya Wizara yangu kwa kipindi kilichopita na ambao wamewezesha kuanda mpango wa mwaka 2008/2009 na kuboresha hoja yangu ambayo naiwasilisha katika hotuba hii. Aidha, natoa shukrani kwa wananchi wote wa Tanzania kwa mchango wao katika kutekeleza majukumu ya Wizara yangu.

Mheshimiwa Naibu Spika, natoa shukrani zangu za pekee kwa Naibu Waziri wangu, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Katibu Mkuu Dr. Naomi Bakunzi Katunzi, watendaji katika Wizara yangu pamoja na taasisi zilizo chini ya Wizara, mashirika mbalimbali ya ndani na nje kwa misaada na ushauri wao. Kwa namna ya pekee natoa shukrani zangu kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Miundombinu chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohamed Hamisi Missanga, Mbunge wa Singida Kusini (CCM) kwa ushauri wao. Aidha, napenda kumshukuru Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mbunge wa Mpanda Kati (CHADEMA) ambaye ni Msemaji Mkuu wa Kambi ya Upinzani kuhusu Wizara yangu na Waziri Kivuli kwa ushirikiano wake na mchango wake katika kuiboresha hoja hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa maelezo mafupi kuhusu chimbuko la Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Tangazo la Serikali Na. 20 la Februari 2008, lililotolewa na Mheshimiwa Jakaya Mrisho Kikwete Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ndilo chimbuko la kuundwa kwa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Wizara iliundwa kwa kuunganishwa kwa Idara ya Mawasiliano iliyokuwa chini ya Wizara ya Miundombinu na Idara ya Sayansi na Teknolojia iliyokuwa chini ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ilikabidhiwa dhamana ya kuhakikisha kwamba Teknolojia ya Habari na Mawasiliano - *TEKNOHAMA (ICT)* kwa pamoja na Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STI) vinachangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu. Jukumu la awali lilikuwa ni kuweka bayana Dira na Dhima ya Wizara ambavyo vitakuwa kiungo muhimu cha juhudzi zote zinazofanywa na Wizara, Taasisi zake pamoja na Wakala chini ya Wizara katika kuyafikia malengo na matarajio ya wadau. Baada ya kuundwa kwa Wizara hii, Taasisi zilizoko chini yake ni:-

- § Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MIST*);
- § Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*);
- § Taasisi ya Afrika ya Sayansi na Teknolojia ya Nelson Mandela (*NMAIST*);
- § Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (*TAEC*);
- § Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (*COSTECH*);
- § Shirika la Posta Tanzania (*TPC*);
- § Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*); na
- § Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*).

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu Wizara ilipoundwa mwezi Februari, 2008 imeendelea na utekelezaji wa majukumu na mipango yake kwa kuzingatia Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 - 2010, Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano, Sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu, Sera ya Taifa ya Posta, Mpango Mkakati wa Wizara, pamoja na ahadi na maagizo mbalimbali ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hivyo lengo la taarifa hii ni kueleza hali ya utekelezaji wa ahadi za Serikali kwa mwaka wa fedha 2007/2008, malengo ya Wizara na makisio ya Bajeti kwa mwaka 2008/2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 iliekeza sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, itekeleze maeneo muhimu yafuatayo:-

- (a) Kuboresha mtandao na huduma za simu za mezani na za kiganjani hadi ngazi ya vijiji.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara yangu, ilisimamia uboreshaji wa mtandao na huduma za mawasiliano nchini kwa kupanua huduma za simu za mezani na kiganjani hadi ngazi ya vijiji. Hadi kufikia Machi, 2008 kuna takribani watumiaji wa huduma za mawasiliano ya simu za mezani 159,077 na kiganjani 9,523,392.

(b) Kuhakikisha kuwa huduma za posta nchini zinapanuliwa hadi vijijini ili kuongeza kasi ya usambazaji barua na vifurushi. Aidha, kuimarisha na kupanua mfumo mpya wa mawasiliano unaotumia teknolojia ya kompyuta. Katika kuhakikisha kuwa huduma za posta nchini zinapanuliwa, Wizara kuititia Shirika la Posta nchini, ilikamilisha ujenzi wa jengo jipya la Posta ya Mpanda, jengo la huduma za *EMS* na *internet café* Morogoro, na awamu ya kwanza ya upanuzi wa majengo ya Posta Kuu za Dodoma na Morogoro.

Aidha, Serikali imeanza mradi wa Kaunta Elektroniki ikiwa ni hatua ya kwanza katika kuimarisha na kupanua mfumo mpya wa mawasiliano unaotumia teknolojia ya kompyuta katika Posta za Dar es Salaam, Morogoro, Arusha na Zanzibar.

(c) Kuongeza kasi ya kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kujenga uwezo wa kuratibu na kuimarisha mfumo huo na kuanzisha mfuko maalum wenyewe lengo la kupeleka huduma za simu na “*internet*” hadi vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliendelea na mchakato wa kuunda Mfuko wa Huduma za Mawasiliano kwa wote “*Universal Communications Access Fund-UCAF*”. Mfuko huu utasaidia kufikisha huduma za mawasiliano vijijini kwa kuwapatia ruzuku wawekezaji walio tayari kupeleka miundombinu na huduma za mawasiliano sehemu zote ambazo hazina mvuto wa kibiashara. Mfuko huu utaanza kutumika rasmi Desemba, 2008.

(d) Kuifanya Tanzania kuwa kiungo kikuu cha mawasiliano Kikanda na Kimataifa “*ICT hub through marine optic fibre system*”.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara yangu katika kutekeleza azma ya kuifanya Tanzania kuwa kiungo kikuu cha mawasiliano Kikanda na Kimataifa, iliratibu shughuli za kuridhia itifikasi ya *NEPAD* ya kujenga mtandao wa baharini unaoitwa *UHURUNET* na ule wa nchi kavu wa *UMOJANET*. Itifikasi hiyo iliridhiwa na Bunge lako Tukufu mwezi Novembra, 2007.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Sayansi na Teknolojia, Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 iliekeza sekta hii kuchukua hatua zifuatazo:-

(a) Shughuli za utafiti na maendeleo (*Research and Development (R&D)*) kutengewa kiasi cha angalau asilimia 1.0 ya bajeti ya Serikali kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa utafiti na maendeleo Wizara yangu, iliratibu Mfuko wa Taifa wa Uendelezaji Sayansi na Teknolojia (*MTUSATE*). Tengeo liliongezeka kutoka shilingi milioni thelathini mwaka 1995 hadi milioni mia sita mwaka 2007. Aidha, tengeo la Serikali kwa upande wa utafiti limeongezeka kutoka asilimia 0.022 na kufikia 0.028 ya pato la Taifa.

(b) Kuingia katika utaratibu wa kusajili na kulinda “*patenting and protecting*” hakimiliki za matokeo ya ubunifu kwa watafiti na kwa Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hatua ya awali ya kusajili na kulinda “*patenting and protecting*” hakimiliki za matokeo ya ubunifu kwa watafiti na kwa Taifa Serikali imerejea na kuhuishwa Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 na kuandaa rasimu ya Sera mpya ya Taifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu. Tunategemea sera hii itakuwa tayari kabla ya mwisho wa mwaka huu wa fedha (2008/2009).

(c) Hali ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na Changamoto zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, shughuli nyingi katika sekta hii zinaendeshwa na sekta binafsi ambazo zimefanikiwa kiutendaji. Kwa upande wa huduma za simu, makampuni ya simu yamepanua huduma zao na mchango wake kiuchumi ni mkubwa kwa mfano katika mwaka wa fedha 2007/2008 Sekta ya Mawasiliano ilichangia asilimia 20.1 ya Pato Ghafi la Taifa.

Hata hivyo, huduma hiyo inakabiliwa na tatizo la matumizi mabaya ya simu za kiganjani. Wizara yangu inatayarisha Muswada wa Sheria utakaowezesha kupata simu kadi (*Sim card*) kwa vitambulisho na kuwezesha kuwachukulia hatua za kisheria wale wote watakaobainika kuwa na matumizi mabaya ya simu hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa Shirika la Posta changamoto kubwa iliyolikibili ni mzigo wa madeni, hali ambayo ilieendelea kuliondolea Shirika uwezo wa kutafuta mtaji na kuwekeza. Mzigo huu wa madeni umelifanya Shirika lisistahili kukopesheka. Serikali kwa kutambua tatizo hilo, imechukua madeni ya takribani sh. 20.4 bilioni na *USD 674,871.41* na kufuta madeni ya sh. 5.2 bilioni na *USD 492,815* ili kusafisha mizania ya Shirika. Tunashukuru Waheshimiwa Wabunge kwa jitihada zenu ambazo zimesaidia kufikia hatua hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhamasisha wanafunzi kupenda masomo ya sayansi; Wizara kwa kushirikiana na taasisi za mafunzo inatekeleza yafuatayo:-

- Inaendesha mafunzo maalum kwa wanafunzi wa kike (*Pre-entry Programme for Female Science Students*) katika kozi ya ufundi na sayansi.
- Imetoa tuzo kwa wahitimu wa kike katika ngazi mbalimbali za elimu wanaofanya vizuri katika masomo ya sayansi, teknolojia na ufundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa utafiti changamoto iliyopo ni kuhakikisha kuwa matokeo ya tafiti mbalimbali zinazofanyika nchini zinawafikia walengwa na hivyo kusaidia mbinu bora za uzalishaji na huduma na hatimaye kukuza kipato na kuondoa umasikini.

Wizara imanzisha masijala ya utafiti lengo likiwa ni kupata kanzi data (*data base*) ya tafiti zilizofanyika nchini na kuona jinsi zitakavyohawilishwa.

(d) Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka 2007/2008

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara yangu imefanikiwa kutekeleza ahadi ilizozitoa Bungeni kwa mwaka wa fedha 2007/2008 kupitia Idara na Taasisi zake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Utawala na Utumishi. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Idara ya Utawala na Utumishi pamoja na mambo mengine ilitekeleza yafuatayo:-

-Iliratibu mafunzo mbalimbali ndani na nje ya nchi kwa watumishi kumi na tisa (19) ili kuwaongezea ujuzi, maarifa na ufanisi katika utendaji wao wa kazi.

-Iliendelea kushirikisha sekta binafsi katika utoaji wa huduma (*non-core services*) Makao Makuu pamoja na Chuo cha Ufundı Arusha (wakati kilipokuwa chini ya Wizara), hususani huduma za ulinzi, usafi na chakula.

-Iliratibu upatikanaji wa vibali vya ajira 1,528 katika Vyuo Vikuu na Taasisi zake kwa lengo la kupunguza uhaba wa wafanyakazi.

-Iliadhimisha siku ya UKIMWI ya Wizara kwa kufanya shughuli mbalimbali zinazohusu upimaji UKIMWI kwa hiari, matumizi ya dawa za kurefusha maisha kwa waishio na virusi vya UKIMWI na kupunguza maambukizo ya UKIMWI kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. Pia iliandaa mwongozo wa kushughulikia taratibu za kutoa lishe na matibabu kwa watumishi waishio na virusi ya UKIMWI. Iliajiri watumishi 33.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Sera na Mipango. Katika Mwaka wa fedha 2007/2008 Idara ya Sera na Mipango ilitekeleza yafuatayo:-

-Iliratibu utekelezaji wa maagizo ya Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya mwaka 2005-2010, na kuwasilisha taarifa za utekelezaji kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu.

-Iliratibu utekelezaji wa miradi mitano ya maendeleo katika Taasisi zilizo chini ya Wizara.

-Iliratibu shughuli za ushirikiano wa Kimataifa, ikiwa ni pamoja na kuratibu mahudhurio kwenye Vikao vya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) na kuingia Mikataba ya Maridhiano na nchi marafiki.

-Iliratibu maandalizi ya Mpango Maalumu wa kuendeleza Sayansi na Teknolojia, Elimu ya Juu na Ufundı utakaofadhiliwa na Benki ya Dunia.

-Iliratibu maandalizi ya mkakati wa kuendeleza Elimu ya Juu na Ufundi ili kukabiliiana na ongezeko la wanafunzi linalotokana na mafanikio ya Mpango wa Maendeleo ya Elimu ya Msingi (*MMEM*) na Sekondari (*MMES*). Hata hivyo kutokana na mabadiliko ya Wizara yaliyofanyika Februari, 2008, utekelezaji wa Programu hii utaratibiwa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.

-Iliratibu uandaaji wa rasimu ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Juu na Ufundi (*MMEJU*) ambayo imekabidhiwa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (*WEMU*) kwa hatua zaidi.

-Iliratibu ukusanyaji, uchambuzi, na hatimaye kutoa chapisho la Takwimu, zinazohusu maendeleo ya sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Mawasiliano. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Idara ya Mawasiliano ilitekeleza kazi zifuatazo:-

-Iliratibu mradi wa kuanzisha Mfumo Mpya wa Anuani na Simbo za Posta (*New Addressing and Postcode System*). Mradi huu umeanza kutekelezwa kwa majaribio katika Manispaa ya Arusha. Mradi huu utarahisisha na kuboresha huduma zinazotolewa na sekta zingine kama za ulinzi na usalama, uhamiaji, biashara (mapato na kodi), vizazi na vifo, vitambulisho vya uraia, sensa ya watu, upigaji kura na utalii.

-Iliendelea kuhamasisha na kuimarisha matumizi ya huduma ya *TEKNOHAMA* kwa kujenga uwezo wa wajasiriamali ili kuongeza tija na uzalishaji. Ilishiriki uanzishajii wa vituo vya Mawasiliano Vijijini (*Rural Multipurpose Community Telecentres*) katika Wilaya za Ludewa (Mchuchuma), Shinyanga Vijijini (Isaka), Hai (Masama) na Singida (Ikungi).

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Sayansi na Teknolojia. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Idara ya Sayansi na Teknolojia ilitekeleza yafuatayo:-

- Iliandaa Rasimu ya Sera ya Taifa ya Utafiti ili kukidhi mahitaji na mazingira ya sasa.

- Imerejea na kuhuishaa Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia ya mwaka 1996 na kuandaa rasimu ya Sera mpya ya Taifa ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu.

-Imeelimisha jamii kupitia vyombo vya habari kuhusu matumizi ya Sayansi na Teknolojia na Ubunifu. Jumla ya vipindi 52 vilirushwa kupitia Shirika la Utangazaji la Taifa.

-Imeratibu uanzishwaji wa Taasisi ya Kujenga Uwezo wa Maarifa na Kuendeleza Sayansi, Teknolojia na Ubunifu barani Afrika taasisi hii itaitwa “*Nelson Mandela African Institute of Science and Technology-Arusha*”.

-Iliratibu uandaaji wa rasimu ya Sera ya Taifa ya Nyuklia inayolenga kukuza matumizi salama ya teknolojia hiyo katika sekta mbalimbali za uchumi.

-Iliratibu uanzishwaji wa Kituo cha Taifa cha Bayoteknolojia ya Kilimo kitakachojengwa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Aidha, program zitakazofundishwa zimeandaliwa, pia Chuo kimetenga majengo ya kuanzia.

-Iliratibu utoaji wa tuzo kwa wanafunzi wa kike 120 waliofanya vizuri katika masomo ya Sayansi na Hisabati katika mitihani ya kumaliza Kidato cha Nne mwaka 2007, Kidato cha Sita mwaka 2008, Vyuo Vikuu, Taasisi za Elimu na Ufundu za Serikali na za binafsi. Aidha, Wizara ilitoa tuzo nane (8) kwa shule za sekondari zilizowezesha wanafunzi hao kufanya vizuri katika masomo hayo.

-Inaendelea na juhudi za kuanzisha ‘*Science Parks*’ kwa kushirikiana na Serikali ya India ambapo Hati ya Maridhiano imeandaliwa bado kusainiwa. Aidha, mnamo mwezi Desemba 2007 Wizara kwa kushirikiana na Taasisi ya “*Mclaughlin-Rotman Centre – MRC*” ya Canada iliandaa mpango mkakati wa kubiasharisha gunduzi mbalimbali za Tiba asilia nchini.

-Imechambua na kuwasilisha Serikalini Mikataba miwili ya Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki Duniani (*International Atomic Energy Agency-IAEA*) inayotakiwa kuridhiwa. Mikataba hiyo ni:-

-Fursa za Upendeleo na Kinga (*Agreement on Privileges and Immunities*).

-Kuimarisha Mfumo wa Menejimenti na Uhifadhi wa Malighafi za Mitambo ya Nyuklia (*Joint Convention on the Safety of Spent Fuel Management and on the Safety of Radioactive Waste Management*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Teknolojia Dar Es Salaam. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam ilitekeleza yafuatayo:-

-Ilidahili jumla ya wanafunzi 852 wa mwaka wa kwanza katika programu za Shahada ya Uhandisi (288), Stashahada ya Ufundu Sanifu (482) na Vyeti vya Ufundu Sanifu (82). Kati yao wanawake ni 121 sawa na asilimia 14.2.

-Ilikamilisha malipo ya ununuzi wa jengo la *NHC* la Chang’ombe ambalo linatumika kama Bweni la wanafunzi lenye uwezo wakulaza wanafunzi 132.

-Imekamilisha maandalizi ya awali ya ujenzi wa jengo la ghorofa 10 litakalokuwa na vyumba vya madarasa tisa (9), kumbi za mihadhara mbili (2), ofisi za wafanyakazi/wahadhiri kumi na nne (14), kafeteria moja (1), maabara za kisasa sita (6) na kituo cha ujasiriamali.

-Imegharimia mafunzo ya watumishi 33 kama ifuatavyo; Uduktari wa falsafa 19, Shahada ya Uzamili 10 na Stashahada ya wakutubi 3. Aidha, wafanyakazi wengine 10 waligharimiwa kusoma kozi za muda mfupi ndani na nje ya nchi.

-Iliendesha mafunzo ya *awali* (*Pre- Entry Course*) Juni-Septemba 2007 kwa wanafunzi 184 kama ifuatavyo:-

- Stashahada ya Uhandisi 73 (13 wasichana na 60 wavulana)

-Shahada ya Uhandisi 111 (22 wasichana na 89 wavulana).

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya. katika mwaka wa fedha 2007/2008. Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya ilitekeleza yafuatayo:-

-Imeongeza udahili wa wanafunzi kutoka 175 hadi wanafunzi 400 wa mwaka wa kwanza kwenye programu za Stashahada ya Uhandisi ongezeko hili ni sawa na asilimia 43. Pia iliongeza idadi ya wanafunzi wa kike kutoka wanafunzi 9 sawa na asilimia 5 kwa mwaka 2005/2006 hadi kufikia wanafunzi 20 sawa na asilimia 12 kwa mwaka 2007/2008.

-Imekamilisha ukarabati wa madarasa 11, ofisi za waalimu 27, barabara za ndani, ujenzi wa bweni la wasichana lenye uwezo wa kulaza wanafunzi 64 na maabara ya vimiminika (*Hydraulic Labs*).

-Imeweka alama za mipaka ya ujenzi wa uzio kuzunguka eneo la taasisi kama hatua za awali za kuimarisha usalama.

Jumla ya watumishi 15 walipelekwa masomoni kama ifuatavyo:-

Watumishi 3 Shahada ya Uzamivu – Afrika Kusini.

Watumishi 7 Shahada ya Uzamili – Afrika Kusini na Dar es Salaam.

Watumishi 2 Shahada ya Kwanza – Dar es Salaam.

Mtumishi 1 Stashahada ya Uzamili – Dar es Salaam.

Watumishi 2 Stashahada ya Juu ya Uhasibu – Dar es Salaam. Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia. Katika mwaka wa fedha 2007/2008 Tume ilitekeleza yafuatayo:-

-Kutambua, kutathmini na kuweka kumbukumbu ya lishe ya aina 349 ya matunda na mboga visiviyolimwa (*collected foods*) katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha na Manyara. Aidha, imeratibu utafiti wa mimea yenye viwatilifu vya kuua mbu.

-Kuratibu miradi mbalimbali ya bayoteknolojia kwa kushirikisha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine.

- Kuwezesha kufanyika kwa mikutano ya kiutafiti ili kuhamasisha ushirikiano wa wanasayansi. Mikutano 4 ya kitaifa; 6 ya kikanda na mmoja wa kimataifa ilifanyika nchini.

- Kupanua masijala ya utafiti ya elektroniki kwa kuongeza idadi ya Taasisi kutoka 20 hadi 40. Aidha, taarifa za watafiti nazo zimeboreshwa.]

- Imekamilisha kuorodhesha teknolojia ambazo zitatumika kuanzisha masjala ya teknolojia zilizobuniwa nchini.

-Imefadhili wagunduzi 3 kuendeleza ugunduzi wao unaohusu: kutengeneza Seba engine, Msekeni air drive-engine, na Maranya water pump. Aidha, wagunduzi 6 walipewa Tuzo ya Taifa ya Ugunduzi wa Kisayansi na Teknolojia tarehe 4 Julai, 2008 katika nyanja ya mazingira, tiba, sayansi shulenii na nishati.

-Imeratibu utengenezaji wa mtambo wa kuchoma taka za hospitali. Aidha, mtambo huo upo katika hatua za majoribio.

-Ilishirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Makazi kuhawilisha mashine za kutengeneza matofali ya udongo na saruji kwa ajili ya kupunguza gharama za ujenzi wa nyumba kwa asilimia 40. Mashine hizi zimeanza kutumika katika Mkoa wa Dar es Salaam.

-Kuimarisha mtandao wa Taasisi za Utafiti na Maendeleo kwa kuongeza idadi ya Taasisi zilizounganishwa kwenye mtandao wa Intaneti kutoka 26 hadi 36.

-Imeendelea kuhamasisha wananchi kuongeza uelewa wa kutumia sayansi na teknolojia, kupitia vipindi 30 kupitia luninga, makala 14 na taarifa 38 katika magazeti.

-Imeanzisha mradi wa majoribio ya mawasiliano ya simu kupitia mtandao wa Intaneti (VoIP) ambayo ni ya bei nafuu Lugoba, Chalinze na Miono, Wilayani Bagamoyo.

-Imeendelea na maandalizi ya Kongamano na Maonyesho ya Tatu ya Kitaifa ya Sayansi na Teknolojia.

-Kuwezesha waandishi 17 kuandaa makala ili hatimaye kutoa kitabu kinachohusu vyanzo vya nishati Tanzania.

-Imehawilisha teknolojia za nishati mbadala za mchanganyiko wa makaa ya mawe na masalia ya mimea (*coal-biomass briquettes*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania. Pamoja na mambo mengine katika mwaka wa fedha 2007/2008, Tume ilitekeleza yafuatayo:-

-Ilizifanyia matengenezo mashine 44 za *x-ray* na vifaa vingine tisa (9) vya elektroniki.

-Ilikusanya mabaki 41 ya vyanzo vya mionzi toka Taasisi na sehemu mbalimbali za nchi na kuhifadhiwa katika mazingira yaliyo salama.

-Iliendelea na awamu ya pili ya ujenzi wa ofisi za Tume Makao Makuu.

-Ilikagua minara ya simu na redio katika vituo 89 kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano na kubaini kuwa mionzi inayosambaa na kuwafikia wananchi ni chini ya viwango vya juu vinavyopendekezwa kimataifa.

-Ilikamilisha ujenzi wa Kituo cha kudhibiti majoribio ya silaha za nyuklia chini ya mkataba wa “*Comprehensive Test Ban Treaty of Nuclear Weapons-CTBT*” ambao Tanzania iliuridhia. Kituo hiki ambacho kipo Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, kimeanza kuendeshwa kwa majoribio.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Posta Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Shirika la Posta Tanzania (*TPC*) ilitekeleza yafuatayo:-

- Limekarabati majengo ya Posta katika Kanda za Kaskazini (Posta Kuu ya Moshi na Songe), Kati (Mahenge na Kigoma) Pwani (Posta kuu ya Dar-es-Salaam na Kijitonyama), Zanzibar (Posta ya Chakechake na Raha Leo) na Ziwa (Posta za Mwanza, Shinyanga na Kahama).-Lilinunua magari tisa (9), nukushi kumi na tatu (13), kompyuta (180) na jenereta tisa (9) kwa ajili ya mradi wa kaunta elektronik “*Counter Automation*“.

Liligharamia mafunzo kwa wafanyakazi (86) katika Chuo cha Posta na (22) nje ya Chuo cha Posta.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya Simu (*Tanzania Telecommunications Company Limited – TTCL*). Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) ilitekeleza yafuatayo:-

- Imekamilisha uwekaji wa mitambo mipy ya “*Digital Microwave Radio – DMR*” katika njia za Dar es Salaam – Morogoro – Dodoma, Dar es Salaam – Tanga – Arusha, Dodoma – Kondoa – Arusha – Namanga, Mbeya – Tunduma – Sumbawanga, na Mtwara – Newala – Masasi – Nachingwea.

-Imeondoa simu za kukoroga (magneto) na kuanzisha huduma za simu za kiganjani zinazotumia teknolojia ya “*Code Division Multiple Access (CDMA)*” katika Mikoa ya Mbeya (Mwakaleli, Lwangwa, Kakende, Kiwira), Iringa (Ilula), Singida (Itigi), Mwanza (Misungwi, Ngudu, Malya), Tabora (Urambo, Sikonge, Kaliua, Itobo, Usoke), Kigoma (Uvinza, Manyovu), Dodoma (Mtera, Mvumi), Lindi (Ruangwa,

Nachingwea, Liwale), Mtwara (Ndanda), Ruvuma (Liuli, Mbambabay, Litembo, Namtumbo na Hanga Abbey).

- Imekamilisha ufungaji wa mtambo wa huduma kwa wateja na utoaji wa Ankara “Customer Care and Billing System – CCBS” kwa ajili ya kuboresha utoaji na usahihi wa Ankara za wateja.

- Ilisambaza mtandao wa huduma za takwimu (*Broadband and Data*) katika makao makuu ya mikoa yote na baadhi ya Wilaya.

- Ilibadilisha mitambo ya zamani (*exchanges*) katika miji ya Arusha, Pemba, Moshi, Tanga, Singida, Bukoba, Kigoma, Utete, Kibiti, Ikwiriri, Mafia na Kilwa Masoko.

- Imekamilisha upembuzi yakinifu wa ujenzi wa njia kuu za mawasiliano kwa kutumia Mkongo wa Kigae (*Optical Fibre Cable*). Arusha-Musoma-Mwanza kupitia mbuga za wanyama za Ngorongoro na Serengeti, Mwanza-Shinyanga-Isaka-Rusumo,Kabanga-Nyakanazi-Bukoba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2007/2008, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitekeleza yafuatayo:-

-Iliwezesha ujenzi wa mitambo ya kupitisha taarifa za intaneti (*Internet Exchange Point – “IXP”*) mipyä katika Manispaa ya Arusha. Aidha, ujenzi wa vituo kama hivyo katika miji ya Mwanza na Mbeya unaendelea.

-Kituo cha Kusajili na Kusimamia matumizi ya anuani pepe zinazotumia jina la nchi yetu “*dot.tzccTLD*” kimeanzishwa katika jengo la Millemium Tower lililoko Kijitonyama - Dar es Salaam.

-Imewezesha uanzishwaji wa mradi wa kuandaa anwani mpya kwa majaribio Mkoani Arusha (*New addressing and post code systems*).

-Imeboresha mfumo wake wa utoaji huduma za leseni na kurahisisha matumizi ya teknolojia ya mawasiliano na kisasa (*Convergic Licences*).

-Inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa kubadilisha Teknolojia ya Utangazaji toka *Analogue* kwenda *Digital* lengo ni kuhakikisha kwamba ifikapo mwaka 2015 Teknolojia ya Utangazaji itakayokuwa inatumika iwe *digital*.

-Inaendelea kushirikiana na Tume ya Mionzi kuhakikisha matumizi salama ya simu za viganjani na mitambo ya mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, Malengo ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2008/2009.

Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara yangu kupitia Idara na Taasisi zake imejiwekea malengo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Utawala na Utumishi pamoja na mambo mengine, inatarajia kutekeleza yafuatayo ili kuimarisha na kuboresha uwezo wa utendaji kazi kwa watumishi wake:-

-Itaajiri watumishi wapya 13 kwa mujibu wa Ikama na mahitaji ya Muundo mpya wa Wizara. Aidha, watumishi wapya watakaoajiriwa watapatiwa mafunzo elekezi.

-Itawapandisha vyeo watumishi waliopo kwa kuzingatia sifa na vigezo vilivyoainishwa katika miundo yao ya utumishi.

-Itawapelea mafunzoni watumishi 33 ili kuwaongezea ujuzi, maarifa na ufanisi katika utendaji kazi.

-Itahamasisha watumishi kupima afya zao; hii itasaidia kutambua watumishi wanaohitaji huduma za ushauri nasaha, dawa za kurefusha maisha pamoja na virutubisho. Pia itatoa mafunzo kuhusu *UKIMWI* kwa watumishi 126 ili kuepuka maambukizi mapya ya *VVU*.

-Itaendesha mafunzo ya kupima utendaji kazi kwa uwazi (*OPRAS*) kwa watumishi 126 ili kukidhi utekelezaji wa malengo ya Wizara.

-Itakamilisha Mkakati wa Habari, Elimu na Mawasiliano (*IEC Strategy*) ili kuboresha utoaji wa habari kwa umma.

-Itakamilisha Mkataba wa Huduma kwa Mteja “*Client Service Charter*” ili kuwa na vigezo bora vyta huduma vinavyopimika.

-Itaandaa na kutekeleza mkakati wa Wizara wa Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

-Itaendelea kuimarisha na kuboresha matumizi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.

-Itaendelea kusimamia manunuzi kwa mujibu wa sheria kanuni na taratibu zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Sera na Mipango. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Idara ya Sera na Mipango inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Itaratibu uandaaji na uhuishaji wa Sera na Sheria mbalimbali zinazosimamiwa na Wizara.-Itaratibu mpango wa mwaka wa tatu wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2005-2010.

- Itaratibu utekelezaji wa sehemu ya Mradi wa ‘Quick win’, inayohusu ICT ambayo itatekelezwa na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.
- Itaratibu utekelezaji na ufuutiliaji wa miradi ya Maendeleo inayotekelzwa na Wizara na Taasisi zilizo chini yake.
- Itarejea na kuratibu utekelezaji wa Mpango Mkakati.
- Itaratibu Maandalizi ya “Mpango Kabambe wa Maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia” (*Communications, Science and Technology Master Plan*).
- Itaendelea kuratibu shughuli za Ushirikiano wa Kikanda na Kimataifa.-Itaratibu uandaaji wa takwimu mbalimbali za Wizara zinazohusu sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Mawasiliano. Katika mwaka wa fedha 2008/2009 Idara ya Mawasiliano inatarajia pamoja na mambo mengine kutekeleza yafuatayo:-

-Itaratibu ujenzi na uendelezaji wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano (*National ICT Infrastructure Backbone*) pamoja na Mkongo wa Kimataifa wa Baharini (*East African Submarine Cable –EASSy Cable*).

- Itaratibu uanzishwaji wa Mfumo mpya wa anuani na namba za Posta nchini (*New Addressing and Postcode Systems*).

- Itakamilisha uanzishaji na kuratibu uendeshaji wa Mfuko wa Huduma ya Mawasiliano kwa wote (*Universal Communications Access Fund*).

- Itaratibu utekelezaji wa miradi ya mawasiliano, posta na vituo vya mawasiliano kwa lengo la kukuza na kuimarisha huduma za mawasiliano kwa wote.

- Itakamilisha uandaaji wa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*TEKNOHAMA*).

-Itafanya tathmini kuhusu hali ya matumizi ya vifaa na huduma za Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*TEKNOHAMA*) “*E-readiness Assessment/Survey*” nchini.

-Itaratibu mradi wa *PAN-AFRICAN e-initiatives* ambao utahusisha *tele-education, tele-medicine na e-government*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Idara ya Sayansi na Teknolojia. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Idara ya Sayansi na Teknolojia inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- Itakamilisha uandaaji wa Sera za Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, Utafiti, Bayoteknolojia na Teknolojia ya Nyuklia.

- Itaendelea kutoa elimu kwa umma kupitia vyombo vya habari kuhusu umuhimu wa matumizi ya sayansi na teknolojia kwa maendeleo ya jamii.
- Itaanza ukarabati wa majengo ya *CARMATEC* ambayo yatatumika kuanzia shughuli za Taasisi ya Nelson Mandela.
- Itaendelea kuratibu na kuwezesha uanzishwaji wa kituo cha Taifa cha Kilimo cha Bayoteknolojia kitakachojengwa Chuo Kikuu cha Sokoine.
- Itaendeleza mkakati wa uhamasishaji wanafunzi na hasa wa kike ili waweze kujiunga na masomo ya sayansi, teknolojia na uhandisi katika ngazi mbali mbali za elimu.
- Itaridhia mikataba yenye maslahi kwa Taifa inayosimamiwa na Wakala wa Kimataifa wa Nguvu za Atomiki (*IAEA*) ili kuwezesha ushirikiano katika upatikanaji wa matumizi salama ya teknolojia ya nyuklia na usimamizi wa kinga ya mionzi.
- Itarejea na kuhuisha Sheria Na. 7 ya mwaka 1986 ilioanzisha Tume ya Sayansi na Teknolojia ili kukidhi mahitaji ya sasa. -Itaandaa mfumo wa kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini kwa kushirikiana na *UNESCO*.

Mheshimiwa Naibu *Spika*, Taasisi ya Teknolojia Dar Es Salaam. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam inatarajia kutekeleza mambo yafuatayo:-

-Itadahili jumla ya wanafunzi 1100 wa mwaka wa kwanza wakiwemo wanafunzi 600 wa Stashahada ya Uhandisi, wanafunzi 420 wa Shahada ya Uhandisi na wanafunzi 80 wa mafunzo ya Cheti cha Teknolojia ya Habari (*IT Basic Certificate*).

-Itaendelea kutoa mafunzo maalum (*Pre – entry course*) ili kuongeza udahili wa wanafunzi wa kike katika Stashahada ya Ufundı Sanifu (25) na Shahada ya Uhandisi (28).

-Itagharimia mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi wapya 28 na ya muda mfupi kwa wafanyakazi 18.

-Itapanua Maktaba ya Taasisi (*Vertical Extension*) ili kuboresha huduma za Maktaba kwa wanafunzi na wafanyakazi.-Itanunua samani za madarasa 14 (*Fixed Chairs/Tables*).

-Itapitia upya mitaala ya programu ya Shahada ya Uhandisi kwa nia ya kutekeleza mwongozo uliotolewa na Baraza la Elimu ya Ufundı Tanzania (*NACTE*).

-Itaanza kufundisha kozi mpya ngazi ya Diploma ya Ufundı Sanifu katika fani zifuatazo:-

*Communication Systems Technology;  
Biomedical Engineering;  
Information Technology;  
Mechatronics Engineering;*

- Itaongeza na kuimarisha shughuli za kitengo cha ‘*Culture of Maintenance*’ cha Taasisi.
- Itaimarisha na kuanzisha ushirikiano na Vyuo vya Elimu ya Juu na vya Ufundi vilivyo nchini na vya kimataifa.-Itafunga mtambo wa mawasiliano ya kutumia kompyuta yenye uwezo mkubwa “*Super Computer*” ambayo imepatikana kwa msaada wa Serikali ya India.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya inakusudia kutekeleza yafuatayo:-

Itaongeza idadi ya wanafunzi kutoka 527 kwa mwaka 2007/2008 hadi wanafunzi 1416 mwaka 2008/2009.

- Itakamilisha taratibu za kuanzisha shahada ya kwanza katika fani za mitambo, ujenzi, umeme, usanifu majengo, sayansi ya biashara na Uhandisi wa Kompyuta (*Bachelor of Engineering*).
- Itagharamia mafunzo maalum ya ualimu (*pedagogical skills*) kwa walimu wahandisi wapya 95 ili kukamilisha taratibu zilizowekwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi.
- Itagharamia mafunzo ya watumishi 24 katika ngazi ya Shahada ya Uzamivu (6), Shahada ya Uzamili (10), Stashahada ya Uzamili (8).
- Itaendeleza ushirikiano na Vyuo vya Ufundi barani Afrika chini ya uratibu wa “*Commonwealth Association of Polytechnics in Africa*” (CAPA).
- Itaendelea na maandalizi ya ujenzi wa jengo la maktaba lenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1600 kutoka idadi ya wanafunzi 200 kwa sasa. Pia itaongeza matumizi ya elektroniki.  
-Itaendeleza ujenzi wa majengo mawili ya kuishi wafanyakazi kwa ajili ya malazi ya wanafunzi.
- Itakarabati majengo na mtandao wa mabomba ya maji safi na taka na mfumo wa umeme.
- Itaendelea kutoa mafunzo ya awali (*Pre-Entry Course*) kwa wanafunzi wa kike katika masomo ya sayansi, uhandisi na teknolojia.

- Itaendelea kugharimia huduma za chakula, ulinzi, usafi na mapokezi kwa njia ya wazabuni kama njia ya kuongeza ufanisi.
- Itanunua na kufunga mashine, mitambo na vifaa vya maabara kwa lengo la kuboresha mafunzo yatolewayo.
- Itanunua vitabu vya kiada na rejea. Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Sayansi na Teknolojia. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Tume ya Sayansi na Teknolojia inatarajia kutekeleza mambo yafuatayo:-

  - Itakamilisha ukarabati wa jengo na ofisi zake.
  - Itaendelea kutoa mwega kwenye miradi ya utafiti kama vile; Mimea, Dawa ya kutibu Malaria, Nishati mbadala, uchomaji wa taka ngumu.
  - Itasimamia na kuendeleza shughuli za bayoteknolojia nchini ikiwemo uanzishaji wa Chama cha Wataalamu wa bayoteknolojia, uzalishaji wa mbegu za mahindi zinazostahimili ukame, kukabiliana na magonjwa ya mazao ya mtama, mihogo na viazi, kusafisha maji taka yatokanayo na viwanda vya samaki na kuzalisha nishati ya bayogesi.
  - Itaendelea kuhawilisha Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (*TEKNOHAMA*) kwa kuwezesha uendeshaji wa vituo vya vijijiini (*telecentres*) vilivyopo Ngara, Kilosa, Sengerema, Wete na Lugoba. Aidha vituo vipya vitatu vitaanzishwa.
  - Itaanzisha tovuti (*web portal*) ya taarifa za bayoanuwai hapa nchini.
  - Itaratibu uandaaji wa vipindi 30 vya luninga, makala 20 na taarifa 40 katika magazeti ili kuendeleza kupanua uelewa wa wananchi kuhusu matumizi ya sayansi na teknolojia kwa maendeleo.
  - Itakamilisha juzu la pili la kitabu cha vyanzo vya nishati Tanzania.
  - Itaendelea kuhawilisha teknolojia za nishati mbadala katika Mikoa ya Shinyanga na Dodoma, hususani bayogesi, upepo na mkaa wa bayomasi. Aidha, Tume itafanya ufuutiliaji ili kubaini matokeo ya matumizi ya teknolojia hii.
  - Itaratibu usimikaji wa mtambo wa kuchoma taka za hospitali katika hospitali ya Lugalo, Dar es Salaam.
  - Itaratibu upatikanaji wa teknolojia ya kusindika mmea wa “*Artemisia*” unaopatikana Lushoto na Njombe, ambao ni kiini cha dawa itumikayo kutibu malaria.
  - Itapanua wigo wa matumizi ya Masjala ya Utafiti na kuanzisha Kanzi data (*Data base*) ya Watafiti na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania pamoja na mambo mengine inatarajia kutekeleza mambo yafuatayo:-

-Itatoa huduma ya upimaji wa mionzi (*Personnel Dosimetry Service*) kwa wafanyakazi wanaokadiriwa kufikia 1300.

-Itakagua Vituo vya mionzi vya X-Ray 150 na minara 70 ya simu za kiganjani na redio.

-Itaendelea kukusanya mabaki ya vyanzo vya mionzi ayonisha na kuyahifadhi katika maabara maalumu, CRWMF iliyoko Njiro na Arusha.

-Itakamilisha ujenzi wa jengo la ofisi Makao Makuu Arusha.

-Itaendelea kutekeleza sheria ndogo za kudhibiti viwango vya mionzi kwenye *vyakula (Protection for Radiation, Control of Radiation Contaminated Foodstuffs Regulations, 1998)* kwa kupima sampuli 2600 za vyakula viingiavyo na vinavyopelekwa nje ya nchi.

-Itaendelea na ukaguzi wa vyanzo vya mionzi katika mazingira katika vituo vipatavyo 26.

-Itaendeleza mipango ya ukaguzi wa migodi ili kubaini hali ya usalama na kupendekeza hatua za kuchukua kufuatia matokeo ya ukaguzi huo.

-Itaendesha kituo (*Radiological Monitoring Station, RMS*) cha kupimia mionzi katika mazingira (*RN64, Dar es Salaam*) chini ya mkataba wa *Comprehensive Test Burn Treaty of Nuclear Weapons – CTBT* ambao Tanzania ni mwanachama.

-Itaendelea kuwapatia mafunzo zaidi wataalamu wake ili kuboresha utendaji wa kazi zao.

-Itaimarisha huduma za matengenezo ya vifaa vya elekroniki na mashine za *x-ray*.

-Itaendeleza mawasiliano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa lengo la kuanzisha ofisi ndogo ya Tume Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Posta. Katika mwaka wa fedha 2008/2009, Shirika la Posta linatarajia kutekeleza mambo yafuatayo:-

-Kuendelea na mradi wa “*Counter Automation*” katika Posta za Mikoa 25 iliyobaki. Hadi hivi sasa ni Mkoa wa Dar es Salaam tu, ambapo mradi huu umekamilika.

-Kujenga posta mpya za Kibondo na Katesh.

-Kukamilisha ukarabati wa majengo ya Posta Kuu za Dar-es-Salaam, Mwanza, - Shinyanga na kuanza ukarabati wa Posta za Tanga, Bukoba, Mbeya, Dodoma, Musoma na Zanzibar (Shangani, Makunduchi na Kijangwani).

-Kununua magari (5) na pikipiki (3) kwa ajili ya usambazaji barua (*Courier Services*) katika jiji la Dar es Salaam.

-Kupanua vituo vya kutoa huduma za intaneti katika miji ya Sumbawanga, Kigoma, Lindi, Musoma, Singida, Songea, Manyara, Chakechake, Wete na Kijitonyama Dar es Salaam.

-Kutoa mafunzo kwa wafanyakazi ili kuongeza tija katika Shirika.

-Kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania kuendeleza mradi wa anuwani na simbo za Posta.

-Kuendeleza na kuingia mikataba mipyä na makampuni mengine katika usafirishaji wa fedha, vifurushi na vipeto.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Kampuni ya Simu itatekeleza mambo yafuatayo;

Kwanza, itaboresha na kupanua njia kuu za mawasiliano (*Digital Microwave Backborne*) kati ya Dar es Salaam-Zanzibar-Pemba-Tanga, Morogoro-Ifakara-Mahenge na Nyololo-Songea-Tunduru. Itashiriki katika usimamizi wa ujenzi wa Mkongo wa mawasiliano wa Taifa. Pili, itaendelea kupanua mtandao wake wa simu za kiganjani katika miji ya Dar es Salaam, Arusha, Mwanza, Zanzibar, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Dodoma na Mbeya. Tatu, itaendelea kubadilisha mitambo ya *exchange* ya zamani na kuweka mipyä ili kukidhi mahitaji halisi ya simu kwa sasa. Mitambo itakayoondolewa na kubadilishwa ni mitambo yote ya *GX5000, DTS* na *Neax*. Kazi hii inatarajiwaa kukamilika mwishoni mwa mwaka 2009. Nne, itapanua mtandao wa *Broadband* ili kuongeza uwezo wa mitambo kwa huduma ya *Broadband* kwa wateja wakubwa na Taasisi kutoka 20,000 za sasa na kufikia 30,000. na tano, itashiriki katika usimamizi wa ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009, Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania inatarajia kutekeleza mipango ifuatayo; kwanza, itaratibu watoa huduma za mawasiliano ili washiriki katika ujenzi wa swichi za intaneti (*Internet Exchange Points* (IXPs) na kuunganisha mitandao yao kwenye swichi hizo.

Pili, itaratibu uunganishwaji wa *Internet Exchange Points* za Kenya, Uganda na Tanzania, kama ilivyoazimiwa na Umoja wa Wadhibiti wa Mawasiliano na Watoa Huduma ya Mawasiliano ya Simu na Posta Afrika Mashariki, tatu, itaaniszha rejestra (*Central Equipment Identification Register-CEIR*) ili kudhibiti matumizi mabaya ya simu za kiganjani kwenye aina yoyote ya mtandao nchini na nchi za Afrika Mashariki na tatu,

itarejea mfumo na taratibu zinazotumika kugawa masafa ikiwa ni pamoja na kukamilisha kugawa masafa yatakayotumika katika *Digital Broadcasting*.

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, itaendelea kupokea na kutathimini maombi ya leseni; kutayarisha na kutoa leseni kwa makampuni yaliyotimiza masharti na taratibu zilizoainishwa na Mamlaka, tano, itaendelea kusimamia na kudhibiti ubora wa huduma za mawasiliano kwa kuyafanyia ukaguzi makampuni yaliyosajiliwa ili kuhakikisha kuwa huduma zinazotolewa zinakidhi viwango vilivyowekwa kwenye leseni zao na sita, itaendelea kuelimisha watumiaji wa huduma za mawasiliano kuhusu taratibu za kuwasilisha malalamiko yao kwa Mamlaka pale ambapo hawakuridhika na huduma wanazopewa na mtoa huduma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara inaazimia kutekeleza yafuatayo, kurejea na kuhuisha Sera na Sheria za Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kuandaa mfumo wa kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu nchini kwa kushirikiana na *UNESCO*, kusimamia ukarabati wa majengo ya *CARMATEC* ili kuiwezesha Taasisi ya Nelson Mandela kuanza shughuli zake, kuimarisha, kupanua na kuendeleza Taasisi za Sayansi na Teknolojia zilizo chini ya Wizara, kwa lengo la kutoa wataalamu wengi zaidi katika fani ya Sayansi na Teknolojia. Aidha, mchakato sasa hivi unaendelea wa kuziwezesha Taasisi za Dar es Salaam (*DIT*) na Mbeya (*MIST*) ili ziweze kutoa wataalam wenye Stashahada, Shahada, Shahada za Uzamili na Uzamivu. (*Makofi*)

Pia kujenga na kuimarisha uwezo wa Wizara kiutendaji kwa njia ya kuajiri wataalamu wapya na kutoa mafunzo kwa wale waliopo katika maeneo yanayohitaji kujenga uwezo, kukamilisha mradi wa ujenzi wa Makao Makuu ya Tume ya Taifa ya Nguvu za Atomiki mkoani Arusha, kuanza ujenzi wa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kwa lengo la kusambaza na kuinua kiwango cha huduma za TEKNOHAMA, kuanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*Universal Communications Access Fund*) kwa lengo la kuwapatia huduma za mawasiliano wananchi wengi hasa wale wanaoishi vijijini, kuimarisha ushirikishwaji wa sekta binafsi kuwekeza katika Sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano kwa kuweka mazingira mazuri ya kuvutia wawekezaji na kuimarisha huduma zinazotolewa na Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) kwa kuhakikisha kuwa wanapata mtaji wa kuijiendesha na kuhimili ushindani na kutoa mchang'o mkubwa zaidi katika Sekta ya Mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuboresha huduma za Posta kwa kupanua mfumo mpya wa mawasiliano unaotumia teknolojia ya Kompyuta, kupanua wigo wa utekelezaji wa mradi wa anuani na simbo za Posta (*Postal Code Addressing System*) na kuanzisha rejesta ili kubaini matumizi mabaya ya simu za kiganjani na kuandaa Muswada wa Sheria ili kuweka utaratibu wa kupata simu kadi kwa vitambulisho badala ya utaratibu holela unaotumika hivi sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutoa shukrani zangu za pekee kwa wadau na wahisani mbalimbali kwa michango yao mikubwa katika Maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Wahisani hao ni pamoja na Marekani, Sweden, Norway, Uhlanzi, Japan, Jamhuri ya Korea ya Kusini, China, India, Benki ya Dunia na

Umoja wa Mataifa. Mashirika mengine ni pamoja na Jumuiya ya Madola, Shirika la Kimataifa la Nguvu za Atomiki Duniani na *Third World Academy of Sciences, International Foundation for Sciences*. Mashirika haya yameonyesha nia ya dhati kusaidia maendeleo ya Sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Wizara inaahidi kuendeleza ushirikiano huu kikamilifu. Aidha, naishukuru sekta binafsi kwa mchango wao katika Pato la Taifa kuitia huduma za simu hususan za kiganjani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, li kuwezesha Wizara yangu kutekeleza mipango iliyojiwekea katika mwaka wa fedha 2008/2009, sasa naliomba Bunge lako Tukufu liidhinishe jumla ya shilingi 42,895,816,000/=, kati ya fedha hizo shilingi 21,292,974,000/= ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, yaani mishahara na matumizi mengineyo na shilingi 21,602,842,000/= ni kwa matumizi ya maendeleo. Kwa upande wa fedha za Maendeleo, fedha za ndani ni kiasi cha shilingi 20,962,842,000/= na fedha za nje ni kiasi cha shilingi 640,000,000/. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa napenda kukushukuru wewe binafsi, Spika pamoja na Bunge lako Tukufu kwa kunisikiliza wakati nikiwasilisha hotuba yangu. Aidha, hotuba hii itapatikana katika tovuti ya Wizara ambayo ni [www.mst.go.tz](http://www.mst.go.tz). (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofî*)

**WAZIRI WA MIUNDOMBINU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki. (*Makofî*)

(*Hoja ilitolewa iamuliwe*)

**MHESHIMIWA ANNE K. MALECELÀ (K.n.y. MHE. MOHAMED H. MISSANGA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MIUNDOMBINU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati yangu ya Miundombinu, naomba nichukue fursa hii, kukushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kwa mujibu wa Kanuni ya 99(7) ya Kanuni za Bunge, Toleo la mwaka 2007, kuhusu Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa Fedha 2008/2009 mbele ya Bunge lako Tukufu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kwa niaba ya Kamati naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika, kwa kuchaguliwa kuwa Mwenyekiti wa Umoja wa Mabunge ya Jumuiya ya Madola (CPA). Tunaamini kuwa atatekeleza majukumu yake hayo kwa kasi na viwango kama ilivyo kawaida yako. (*Makofî*)

Naomba pia niipongeze Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa maandalizi, ushirikiano na mawasilisho mazuri yaliyofanywa na Wizara hii mbele ya Kamati yangu kuhusu Mpango wa Makadirio ya Bajeti ya mwaka 2008/2009. Aidha, Wizara iliwasilisha pia Taarifa ya Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati na Mipango ya Bajeti ya mwaka uliopita wa 2007/2008 na kazi zilizopangwa kufanyika katika mwaka wa fedha wa 2008/2009 ikiwa ni pamoja na maombi ya fedha kwa ajili ya kazi hiyo. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia iliundwa kwa kuunganishwa kwa Idara ya Mawasiliano iliyokuwa chini ya Wizara ya Miundombinu na Idara ya Sayansi na Teknolojia iliyokuwa chini ya Wizara ya Elimu ya Juu, Sayansi na Teknolojia kutohana na Tangazo Na. 20 la Februari, 2008 lililotolewa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ilikabidhiwa dhamana ya kuhakikisha kwamba Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA -ICT) kwa pamoja na Sayansi, Teknolojia na Ubunifu (STI) vinachangia kikamilifu katika maendeleo ya nchi yetu. Hivyo basi, Kamati yangu ya Miundombinu sasa hivi inashughulikia Wizara mbili, yaani Wizara ya Miundombinu na Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia mabadiliko hayo na kuundwa kwa Wizara hii, Kamati ilipata fursa ya kujielimisha kuhusu dira na malengo ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, mpango wa muda wa kati wa matumizi ya fedha za Serikali kwa mwaka 2008/2009 -2010/2011 (*MTEF*).

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na matumizi ya Maendeleo, muhtasari wa mgawanyo wa fedha za Matumizi ya Kawaida kwa Idara na Taasisi kwa Mwaka 2008/2009, mchanganuo wa Matumizi ya Kawaida 2007/2008, Mapato na Matumizi kwa Kipindi cha mwaka 2007/2008, na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya mwaka 2007/2008.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupatiwa elimu hiyo fupi, Kamati ilipata fursa ya kuchambua na kujadili Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka wa fedha wa 2008/2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji ya maagizo ya Kamati yaliyotolewa wakati wa majadiliano ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2007/2008, katika kikao cha tarehe 27 Mei 2007, Kamati ilitoa maagizo yafuatayo kwa utekelezaji kwa Wizara ya Miundombinu iliyokuwa ikishughulikia sekta ya Mawasiliano kwa wakati huo.

Kwanza, Wizara ihakikishe kuwa Jengo la Posta ya Zamani liliopo Mtaa wa Sokoine linarejeshwa kwa Shirika la Posta (TPC), Kamati ipewe taarifa kamili juu ya uanzishwaji wa vituo vya TELECENTER, Kamati ipewe taarifa kamili juu ya uanzishwaji wa Mfuko wa Huduma za Mawasiliano kwa wote (*Universal Communication Access Fund – UCAF*), Kamati ipewe taarifa juu ya baadhi ya wamiliki wa masafa kuhodhi Masafa ya Mawasiliano bila kufuata taratibu za Kisheria, na tatizo la wanafunzi kutopenda masomo ya sayansi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, maagizo yote yemekwishaanza kutekelezwa katika mipango mbalimbali ya Wizara, ambapo baadhi ya maagizo hayo utekelezaji wake unahitaji kufanyiwa utafiti wa kiufundi na ni mipango ya muda mrefu. Kamati imeridhika na mipango mikakati ilijojiwekea Wizara hii katika utekelezaji huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2007/2008 Wizara ilikadiria kukusanya jumla ya shilingi 28,000,000,000/= kama Mapato ya Serikali. Hadi kufikia Machi 2008, Wizara ilikusanya jumla ya shilingi 63,835,724/= sehemu kubwa ya fedha hizo zilitokana na ada ya wanafunzi kutoka Chuo cha Ufundı Arusha. Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2007/2008 Chuo hicho kilitakiwa kuwa Taasisi inayojitegemea. Kwa kuwa mchakato wa kujitegemea ulikuwa haujakamilika Wizara iliendelea kukusanya ada kutoka Taasisi hiyo kama sehemu ya mapato ya Serikali. (*Makofi*)

Katika mwaka wa fedha 2007/2008, jumla ya shilingi 240,443,408,000/= ziliidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, kati ya hizo kiasi cha shilingi 81,690,754,000/= zilitengwa kwa ajili ya mishahara na shilingi 158,752,654,000/= kwa ajili ya matumizi mengineyo hadi kufikia tarehe 31 Machi 2008, Wizara ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya shilingi 182,011,849,499, kati ya fedha hizo shilingi 65,377,091,659/= kwa ajili ya mishahara na shilingi 116,634,757,840 kwa ajili ya matumizi mengineyo. (*Makofi*)

Katika mwaka wa fedha wa 2007/2008 ziliidhinishwa jumla ya shilingi 47,432,389,000/= kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za Maendeleo; kati ya fedha hizo shilingi 28,359,000,000 zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi 19,073,389,000/= zilikuwa ni fedha za nje. Hadi kufikia tarehe 31 Machi, 2008 jumla ya shilingi 25,455,070,884/= zilikuwa zimetolewa na kupelekwa kwenye Taasisi husika, kati ya fedha hizo shilingi 24,901,000,000/= zilikuwa ni fedha za ndani na shilingi 554,070,884/= ni fedha za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mafanikio na changamoto zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wa majukumu ya mwaka wa fedha 2007/2008, ili kuweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia imefanikiwa kuandaa sera zifuatazo, kuandaa Sera ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia, sera ya Taifa ya Mawasiliano ya Simu, sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) na Sera ya Taifa ya Posta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mafanikio yaliyopatikana zilikuwepo pia changamoto ambazo Wizara ilikutana nazo, ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya Wizara yaliyofanywa mwanzoni mwa mwaka 2008, hivyo kuifanya Wizara kuanza kuelekeza majukumu mapya ya Sekta ya Mawasiliano kabla ya mwaka wa fedha 2007/2008 kumalizika, upungufu wa fedha za utafiti ili kukidhi mahitaji ya maendeleo nchini, kutokuwepo kwa mfuko maalumu ya kuendeleza wagunduzi, wavumbuzi na vijana wenye vipaji, kutokuwepo Sera ya Taifa ya Miliki Ubunifu nchini (*Intellectual Property Rights*), kutokuwa na wataalam wa kutosha katika baadhi ya maeneo ya Sayansi, Teknolojia na Ubunifu, na kutokuwa na mazingira ya kuibua na kuendeleza vipaji vya ubunifu na uvumbuzi kwa Watanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kujiwekea mikakati mbalimbali ya kukabiliana na changamoto hizo, ikiwa ni pamoja na kutoa elimu kwa watendaji na wakuu wa taasisi kuhusu mabadiliko yaliyojitokeza, kupanua wigo wa mifuko ya fedha za utafiti kwa njia ya taasisi kushirikiana na sekta mbalimbali za kijamii

na za kiuchumi kwa lengo la kupanua ufadhilli, kujikita zaidi katika kutafuta vyanzo vingine vya mapato badala ya kutegemea Serikali tu, kuanzisha mfumo wa sheria unaofaa kwa maendeleo na uhawilishaji wa teknolojia ikiwemo haki za ubunifu, ufuutiliaji na udhibiti wa uchaguzi na uhawilishaji wa teknolojia pamoja na usalama wa viumbe, kuanzisha vituo vipya vya Sayansi na Teknolojia vyenye lengo la kutoa elimu katika ngazi ya Uzamili na Uzamivu na kuwa na utaratibu wa kuwabakiza *retention scheme*, kuanzisha utaratibu wa utambulishaji, ukuzaji na uendelezaji wa vipaji maalumu, na uwezo wa Sayansi na Teknolojia miongoni mwa Watanzania, hasa vijana kwa maendeleo ya Taifa na kuhuisha mfumo mzima wa Sayansi, Teknolojia na Ubunifu nchini ili kuleta usimamizi mzuri na ufanisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2008/2009, katika kuandaa Bajeti ya mwaka 2008/2009, Wizara ilizingatia mwongozo wa maandalizi ya Bajeti (*MTEF 2008/2009-2010/2011*) uliotolewa na Wizara ya Fedha na Uchumi, mpango mkakati wa Wizara (*Medium Term Strategic Plan*), maelekezo na malengo ya Mkakati wa Kukuza Uchumi na kupunguza Umaskini Tanzania (MKUKUTA), Dira ya Taifa ya Maendeleo ya mwaka 2025, Sera ya Sayansi na Teknolojia, Sera ya Taifa ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA), Sera ya Taifa ya Mawasiliano kwa Simu pamoja na Sera ya Taifa ya Posta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha zilizotengwa na Wizara ya Mawasiliano zimegaiwa kulingana na vipaumbele vya majukumu ya Wizara na taasisi zake. Hivyo basi, fedha zinazoombwu katika mwaka 2008/2009 zinahitajika kwa kutekeleza shughuli zifuatazo, kwanza kuendelea na mchakato kwa kushirikiana na wadau wote wa ndani na nje wa kujenga, kuimarisha na kuendeleza matumizi ya huduma za mtandao wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEKNOHAMA) (*promoting use and application of information and communications technologies – ICTS*) nchini, pili, ujenzi na uendelezaji wa Mkongo wa Kitaifa wa Mawasiliano (*National Broadband Infrastructure Backbone*) pamoja na Mkongo wa Kimataifa wa Baharini (*East African Submarine cable – Eassy Cable*), tatu, kuratibu uanzishwaji wa mfumo mpya wa anuani na namba za Posta nchini (*New Addressing Systems and Postcode*), nne, ukamilishaji wa uanzishwaji na uendeshaji wa mfuko maalum wa kufanikisha maendeleo ya huduma za mawasiliano kwa wote nchini (*Establishment of Universal Communications Access Fund*) na tano, utekelezaji wa miradi ya mawasiliano, Posta, vituo vya mawasiliano (*telecentres*) na umeme hususan sehemu za vijijini kwa lengo la kupunguza umaskini na kuongeza ajira. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sita, uanzishwaji na uimarishaji wa huduma za tovuti na barua pepe vijijini kama sehemu ya programu ya ujenzi wa jamii habari na uelewa (*information/knowledge Society*), saba, kufanya upembuzi yakinifu na kufunga Mtandao wa Mawasiliano wa Elimu na Utafiti (*National Research and Education Network*) kwa majoribio katika Vyuo Vikuu na Taasisi za Utafiti zilizoko Dar es Salaam na Zanzibar chini ya udhamini wa Benki ya Dunia na nane, kuanzisha Kituo cha Kilimo na Biotechnolojia kitakachojengwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (*National Agricultural Biotechnology Centre Affiliated to the Third Component of International Centre of Genetic Engineering and Biotechnoloty in Cape Town - South Africa*) na nane,

kuratibu tafiti za kisayansi katika maeneo yenyе kipaumbele Kitaifa (kilimo na chakula, viwanda, nishati, maliasili, mazingira na afya). (*Makofi*)

Tisa, kuandaa Benki ya Takwimu (*Database*) ya wanasayansi nchini kwa ajili ya kubaini fani zao na kiwango cha elimu walichofikia na maeneo wanayofanyia utafiti, kumi, kuendelea kutoa na kuimarisha huduma za kinga ya mionzi kwa kutoa huduma ya upimaji wa mionzi (*Personnel Dosimetry Service*) na kumi na moja, kuanzisha vituo vipyा vya Sayansi na Teknolojia, kuhuisha mfumo wa Sayansi, Teknolojia na ubunifu nchini kwa kushirikiana na (*UNESCO*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumi na mbili, kuendelea na ukaguzi wa vituo vya matumizi ya mionzi isiyoayonisha ikiwemo minara 70 ya simu za mikononi na redio, kumi na tatu, kuongeza idadi ya Wanafunzi, kuboresha mitaala ya mafunzo na kuvijengea uwezo Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya (*MIST*) na Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam (*DIT*), kumi na nne, kuendelea kuimarisha ushirikiano na Nchi Wahisani, Mashirika ya Kimataifa, Vyuo vya Elimu ya juu na vya Ufundi vilivyo nchini na vya Kimataifa sehemu mbalimbali, kumi na tano, kuimarisha uongozi na uendeshaji wa Wizara, kuwaendeleza Wafanyakazi katika mafunzo na kuwajengea mazingira mazuri ya utendaji kazi, kumi na sita, kuhamasisha watumishi kupima afya zao na kujitokeza ili wenye maambukizi ya VVU/UKIMWI waweze kupata huduma za chakula, madawa na virutubisho na mwisho, kuelimisha watumishi kuhusu masuala ya utunzaji wa mazingira, Jinsia na Utawala Bora ili kuboresha utendaji kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwelekeo wa Bajeti na mpango katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia inakadirwa kuwa na matumizi ya shilingi 42,895,816,000/=. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2008/2009 Wizara imetengewa jumla ya shilingi 21,292,974,000/= kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, ambapo shilingi 471,606,000/= kwa ajili ya kulipia mishahara ya watumishi wa Mashirika na shilingi 13,755,329,000/= ni fedha za matumizi mengineyo (*OC*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2008/2009, Wizara imetengewa shilingi 21,602,842,000/= kwa ajili ya miradi ya maendeleo, kati ya fedha hizo shilingi 20,962,842,000/= ni fedha za ndani na shilingi 640,000,000/= ni fedha za kigeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara hii mpya ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa namna ilivyojipanga kutekeleza majukumu yake ambayo yakitekelezwa kama ilivyojipangia nchi itakuwa imepiga hatua katika maendeleo ya sekta za Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati bado inaishauri Serikali kubuni mikakati ya kupata fedha za ndani ili kuiwezesha Wizara hii iweze kutekeleza mipango ya miradi ya maendeleo kama ilivyojipangia, kwani usoefu umedhihirisha kuwa fedha za kutoka nje kwa wafadhili huchelewa kupatikana kwa muda muafaka hivyo kuchelewesha baadhi ya miradi inayokusudiwa na wakati mwingine inakuwa hazipatikani kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri kuwa Wizara iandae mipango ya utekelezaji (*Action Plan*) kwa kila sera ili mipango itakayotekelawa ijulikane. Aidha, sera na mikakati ya Wizara iainishwe ili kuwezesha tathmini ya utekelezaji wa mipango hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu sekta ya mawasiliano ya Posta, Kamati ya Miundombinu kwa muda mrefu imekuwa ikizungumzia suala la Jengo la Posta ya zamani lililoko Mtaa wa Sokoine kurejeshewa kwa Shirika la Posta Tanzania kwa kuzingatia historia yake. Baada ya jitihada za Kamati kwa kushirikiana na Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Waziri wa Sayansi, Mawasiliano na Teknolojia mchakato wa jengo hilo la Posta kurejeshewa wenyewe uko mbioni kukamilika. Kamati inampongeza sana Mheshimiwa Waziri na Serikali kwa hatua hiyo na inasisitiza kuwa taratibu zikamilishwe mapema ili Shirika la Posta liweze kijiweke mikakati yake ya kujikwamua katika hali ngumu iliyo nayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini pia kuwa hali ya kifedha kwa Shirika la Posta Tanzania ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi unaostahili bado sio nzuri. Hata hivyo, Kamati inaipongeza Serikali nguvu zake zote kwa jitihada za kuchukua madeni ya Shirika hili na kuyafuta katika vitabu, hatua ambayo italiwezesha Shirika la Posta kukopesheka. (*Makofi*)

Aidha, Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali iendelee kutoa mtaji wa kutosha kwa Shirika la Posta Tanzania na kuliwezesha kuwekeza kwenye maeneo yenye kuboresha miundombinu, mitando, vifaa na mitambo ili kuinua viwango vya huduma za Posta kwa wateja, ni vyema tufahamu kwamba bado tunahitaji huduma za Posta. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mataifa mengi hivi sasa duniani yamekuwa na utamaduni wa kutambua maskani na makazi ya kila mwananchi wa nchi husika. Aidha, njia ya kuwa na utambuzi huo ni kwa kila mwananchi kuwa na anuani kwa mfumo wa anuani na Simbo za Posta (*New Addressing System and Post Code*). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu huu utawezesha kumtambua mkazi Kijiografia na kuleta ufanisi katika utawala, usalama, uhamiaji, mapato utoaji wa vitambulisho, hati za kusafiria, usajili, sensa ya watu, upigaji kura na kadhalika. Hivyo, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuwa hatua za awali za kuanzisha mfumo huu wa anuani na Simbo za Posta ambazo zimeanza kuchukuliwa. Kamati inashauri Wizara ishirikiane na Wizara ya Mambo ya Ndani ili zoezi hili liweze kutumika katika kutoa vitambulisho vya Kitaifa kabla ya uchaguzi wa mwaka 2010. Kamati inashauri Wizara ishirikishe wadau husika ili kufanikisha zoezi hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inalishauri Shirika la Posta kubuni mikakati itakayowezesha Shirika kuingia katika soko la ushindani wa kibishara na kuboresha huduma zake kwa kutumia teknolojia za kisasa ili iweze kwenda na wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mfuko wa Huduma za Mawasiliano nchini (*Universal Communication Access Fund*), ambao kwa namna moja au nyingine utasaidia kufikisha huduma za mawasiliano hadi vijijini; Kamati inaishauri tena Wizara iharakishe uanzishwaji wa mfuko huu kwa kuzingatia umuhimu wake kwa maendeleo ya uchumi wa Taifa kwani zoezi hilo linaonyesha kuchukua muda mrefu kukamilishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Wizara inatarajia kuanzisha ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Kitaifa, ambao utasaidia kupunguza gharama za mawasiliano nchini zinazopanda mara kwa mara; Kamati inasisitiza ujenzi wa mkongo ukamilishwe mapema iwezekanavyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuinua maendeleo ya sekta ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEKNOHAMA) nchini, Kamati inaishauri Serikali kuweka juhudzi za makusudi ili elimu hiyo iingizwe kwenye mitaala katika ngazi mbalimbali za elimu nchini. Hii itasaidia kupata na wataalamu wa uhakika katika kusukuma maendeleo ya Taifa hasa ikizingatiwa kuwa dunia imeingia katika mifumo tofauti ya teknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Sekta ya Mawasiliano ya Simu, kwa kuwa hivi karibuni imetangazwa kuwa Kampuni ya Simu za Mkononi *CELTEL* imebadilishwa jina hilo na sasa inajulikana kwa jina la *ZAIN* na kwa kuwa Serikali ya Tanzania ilikuwa na hisa 35% katika Kampuni ya *CELTEL*, Kamati inapenda kujua Serikali imehusishwa kiasi gani katika mabadiliko hayo kwa kuzingatia kuwa Serikali ilikuwa inamiliki hisa hizo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati inapenda kujua kiasi cha gawio (*Dividend*) ambacho Serikali imepata kutokana na kumiliki hisa hizo tangu kuanzishwa kwa Kampuni ya *CELTEL* Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza kuwa Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*) iachane na teknolojia zilizopitwa na wakati. Aidha, Kamati inashauri kuwa Kampuni ya Simu Tanzania ijizatiti katika huduma ya simu za kisasa. *TTCL* inapaswa kuingia katika soko la ushindani na nguvu sawia na Makampuni mengine yanayotoa huduma kama hiyo. Aidha, *TTCL* ibuni mikakati ya kujiongezea kipato kupitia katika huduma nyingine kama za *internet* na kuwa mto huduma katika Wizara na Idara za Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaipongeza Wizara kwa kuanzisha vituo vya mawasiliano nchini (*Telecentres*) kwa nia ya kufikisha mawasiliano hadi kwenye Kata na hatimaye Vijijini. Aidha, kwa kuwa wazo la uanzishwaji wa vituo hivi huibuliwa na wanajamii wenyewe katika maeneo husika, Kamati inaishauri Wizara itoe elimu kwa wananchi juu ya manufaa ya vituo hivyo na kisha ikamilishe uanzishwaji wa vituo hivyo katika maeneo, ambayo bado mfumo huu haujaanzishwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Miundombinu imojiwekea utaratibu wa kukutana na wadau mbalimbali wa sekta inayozisimamia, mojawapo ya sekta hizo ni wamiliki wa Makampuni ya Simu za Mkononi (*Mobile Operators*) pamoja na Mamlaka

ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania (*TCRA*). Katika mikutano hiyo wadau hao waliweza kuwasilisha mbele ya Kamati mapendekezo ya namna wanavyowezwa kushirikiana na Serikali katika ukusanyaji wa kodi katika maeneo ambayo yatasaidia kukuza sekta ya huduma za simu za mikononi na kumpunguzia gharama mlaji wa mwisho (*consumer*) bila kuathiri malengo ya Serikali ya ukusanyaji wa kodi katika sekta hiyo, Kamati imeafikiana na mawazo yao na hivyo kuitaka Serikali kuyapokea na kuyafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwepo na manung'uniko kuhusu matumizi mabaya ya kadi za simu (*Sim cards*), hasa baada ya kadi hizo kuanza kuuzwa kiholela bila kuwepo na udhibiti wa aina yoyote. Kamati inaishauri Serikali iandae rasimu ya Muswada wa Sheria ya Udhibiti wa Ununuzi holela wa kadi hizo pamoja na matumizi mabaya ya kadi na kuwasilishwa Bungeni ili sheria iweze kutungwa. Tungeomba Muswada huo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iimarishe utaratibu wa kukutana na wadau wa sekta husika hasa inapotaka kufanya marekebisho ya ongezeko la kodi na tozo mbalimbali katika sekta husika. Ushirikishwaji ni muhimu ili kuepusha usumbufo usiokuwa wa lazima na kupata maoni ambayo yataisaidia Serikali katika kutekeleza mipango yake kwa ufanisi. Kwa mfano, ongezeko la kodi katika simu za mikononi (*excise duty on mobile phone services*). Ongezeko hilo si tu kama linadumaza matarajio ya huduma hiyo, bali mwananchi wa kawaida ndiye anayetwishwa mzigo wa kuilipa kodi hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipokutana na Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania ilibaini kuwa gharama za simu za mikononi hapa Tanzania ni kubwa kwa maisha ya kawaida ya Watanzania, ikilinganishwa na nchi nyingine duniani. Takwimu zinaonyesha kuwa Tanzania ina tozo ambazo kwa nchi nyingine kama vile Kenya haitozi. Kuwepo na kodi na tozo nyingi kama vile kodi za vifaa kunapandisha gharama ya matumizi ya simu na kufanya matumizi hayo yaonekane kama si muhimu ila ni anasa kwa kuwa si wote watamudu gharama hizo. Kamati inaishauri Serikali kushirikiana na *TCRA* kuendelea kufanya majadiliano na makampuni ya simu za mikononi ili kupata njia mbadala ya kupunguza gharama hizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu taasisi/vyuo vya Sayansi na Teknolojia, Kamati imejulishwa nia ya Serikali ya kujenga Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Nelson Mandela (*The Nelson Mandela Institute of Science and Technology*) huko Arusha katika majengo yaliyokuwa ya *CARMATEC*. Kamati inaipongeza Serikali kwa wazo hilo zuri na inashauri uanzishwaji wa Chuo hicho uanze mapema ikiwezekana katika mwaka huu wa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuwa Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya (*MIST*) na *Dar es Salaam Institute of Technology (DIT)* vipewe hadhi na kutengewa fedha za kutosha kwa maendeleo kutoptera na ukweli kwamba vyuo hivi vinaendelea kupanua shughuli zake kama vile kuongeza idadi ya wanafunzi, ujenzi wa majengo, uzio na miundombinu mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imebaini kuwepo kwa tatizo la ongezeko la kupungua kwa idadi ya wanafunzi katika fani ya sayansi na ambalo bado halijapatiwa ufumbuzi. Kamati inasilitiza Wizara iandae walimu na wataalamu wa masomo ya sayansi yatakayofundishwa kuanzia ngazi ya shule za msingi, ujenzi wa maabara na vifaa mbalimbali vya kisayansi vya kufundishia na kuweka vivutio vitakavyowafanya wanafunzi wapende masomo ya sayansi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali kuviwezesha vyuo hivi na kuvijengea uwezo ili visaidie katika ubunifu na uvumbuzi wa vifaa/vitendea kazi mbalimbali vinavyoweza kumsaidia mwananchi katika kujikwamua kiuchumi. Taasisi hizi zinaweza kushirikiana na *SIDO* kutengeneza vifaa (mashine za kupukuchulia nafaka, majiko ya kutumia nishati ya jua, nishati ya mimea na kadhalika) kwa kutumia malighafi iliyopo nchini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutohana na umuhimu wa Tume ya Nguvu za Atomu Tanzania (*Tanzania Atomic Energy Commission*) na ili Tume hiyo iweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo, Kamati imesikitishwa na Serikali kutoitengea Tume hii fedha za kutosha kwani katika maombi yao ya fedha kwa mwaka huu, kiasi kilichoidhinishwa ni chini ya 50% ya fedha zilizoombwa. Kamati inaishauri Serikali kutoa kipaumbele kwa Tume hii nyeti ili iweze kutekeleza mipango yake iliyojipangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa mwaka 2008/2009, inaomba iidhinishiwe jumla ya shilingi 42,895,816,000/=, kati ya hizo fedha za Matumizi ya Kawaida ni shilingi 21,292,974,000/= ambapo shilingi 477,448,248/= ni fedha za mishahara ya watumishi wa makao makuu na shilingi 7,066,039,000/= ni mishahara ya taasisi zilizo chini ya Wizara na shilingi 13,755,324,000/= ni fedha za Matumizi Mengineyo. Aidha, fedha za Bajeti ya Maendeleo zinazoombwa ni shilingi 21,602,842,000/= kati ya hizo shilingi 20,962,842,000/= ni fedha za ndani na shilingi 640,000,000/= ni fedha za nje. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilipitia na kujadili kwa kina Makadirio ya Bajeti ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia na kuititia kifungu kwa kifungu na kuipitisha na sasa Kamati yangu inaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha maombi hayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru wewe binafsi kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Taarifa ya Kamati yangu, aidha, nawashukuru pia Mheshimiwa Profesa Peter Msolla, Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, Mheshimiwa Dr. Maua Abeid Daftari, Naibu Waziri, Dr. Naomi Katunzi, Katibu Mkuu, pamoja na wataalam wote wa Wizara hii na taasisi zilizo chini yake kwa ushirikiano, ushauri na utaalam wao ambao kwa kiwango kikubwa umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake na kuwasilisha taarifa hii leo katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia niwashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati hii kwa busara zao, hasa kwa kutekeleza kazi za Kamati kwa umahiri na umakini

mkubwa. Ushirikiano wao na kujituma bila kuchoka kwa kupitia na kuchambua mpango na Makadirio ya Bajeti ya Wizara hii na hivyo kufanikisha Taarifa hii, ambayo kwa niaba yao naiwasilisha leo katika Bunge lako Tukufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa nafasi ya kipekee napenda kuwatambua Wajumbe wanaouna Kamati ya Miundombinu amba ni Mheshimiwa Alhaj Mohamed Missanga, Mwenyekiti, Mhe Anne Malecela, Makamu Mwenyekiti na wajumbe ni Mheshimiwa Khadija Salum Al-Qassmy, Mheshimiwa Said Amour Arfi, Mheshimiwa Gosbert Blandes, Mheshimiwa Paschal Degera, Mheshimiwa Bakar Shamis Faki, Mheshimiwa Felix Kijiko, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Mkiwa Adam Kimwanga, Mheshimiwa Suleiman Kumchaya, Mheshimiwa Dr. Festus Limbu, Mheshimiwa Ephraim Madeje, Mheshimiwa Masolwa Cosmas Masolwa, Mheshimiwa Joyce Masunga, Mheshimiwa Herbet Mntangi, Mheshimiwa Dr. Gertrude Mongella, Mheshimiwa Mtutura Abdallah Mtutura, Mheshimiwa Ludovick Mwananza, Mheshimiwa Sigifrid Ngi'tu, Mheshimiwa Mwaka Abdulrahman Ramadhan, Mheshimiwa Profesa Phillemon Sarungi, na Mheshimiwa Godfrey Zambi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho kabisa nachukua fursa hii pia kumshukuru Kaimu Katibu wa Bunge Dr. Thomas Didimu Kashilillah, Makatibu wa Kamati Bibi Justina Mwaja Shauri na Bwana James John Warburg kwa kuihudumia Kamati ipasavyo na kufanikisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati. Aidha, nawashukuru Watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa ushirikiano wao mzuri wa kuiwezesha Kamati yangu utekeleza majukumu yake kwa ukamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Miundombinu, naomba sasa kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. SAID AMOUR ARFI – MSEMAJI WA KAMBI YA UPINZANI kWA WIZARA YA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kwanza kabisa naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kufika hapa Bungeni tukiwa hai na wazima. (*Makofi*)

Pili, naomba nikushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika kwa kunipa nafasi hii muhimu ya kuchangia kwa mujibu wa Kanuni za Bunge Kifungu cha 99(7) toleo la mwaka 2007, na kutoa maoni ya Kambi ya Upinzani kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia kwa mwaka 2008/2009. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Mizengo Pinda, Waziri Mkuu kwa kuteuliwa na Rais kuwa Waziri Mkuu na hatimaye kuthibitishwa na Bunge lako Tukufu, namtakia kazi njema kwenye majukumu yake, tushikamane ili tuweze kulifikisha Taifa letu kwenye maendeleo ya kweli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zaidi nichukue nafasi hii kutoa shukrani na pongezi za kipekee kwa viongozi wa Kambi ya Upinzani kwa ushirikiano wao imara na madhubuti wenye kuiwezesha Kambi ifanye kazi zake kulingana na Kanuni zetu za Bunge. Bila

kusahau, nitoe pia pongezi kwa Wabunge wote wa Upinzani kwa umoja walionao, wakishirikiana na wale wote wawekao mbele maslahi ya nchi hii, kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kwa maslahi ya Taifa na Watanzani wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Kiongozi wa Kambi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed pamoja na Naibu wake Mheshimiwa Dr. Wilbrod Slaa, kwa kunithea kuwa Waziri Kivuli wa Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Napenda kuahidi kuwa nitajitahidi kwa uwezo wangu wote na kuonyesha kuwa hawakukosea katika uteuzi huu. Vile vile nawashukuru wananchi wa Jimbo la Mpanda Kati kwa ushirikiano wanaonipatia katika kufanya kazi yangu vizuri, kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, uwezo na nguvu zangu zote nawaahidi kuwa nitakuwa nao na sitapoteza imani yao kwangu, Mungu awabariki wote. *Amin.*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nichukue nafasi hii kuwapa pole wale wote waliopatwa na maafa na majanga mbalimbali ambayo yote ni miongoni mwa mitihani yake Mwenyezi Mungu Mtukufu. Napenda kuungana na wenzangu katika kuwaombea Marehemu Benedict Losurutia, aliyekuwa Mbunge wa Kiteto (CCM), Mheshimiwa Salome Mbatia aliyekuwa Mbunge wa Viti Maalum (CCM) na Mheshimiwa Chacha Zakayo Wangwe aliyekuwa Mbunge wa Tarime (CHADEMA). Tuwaombee wenzetu wote waliokwishatangulia kwenye makazi mema peponi, na wale waliopatwa na maumivu waweze kupona haraka. *Amin.*

Aidha nimpe pole Mheshimiwa Savelina Mwijage, Mbunge wa Viti Maalum (CUF) kwa kufiwa na mwanawe mpandwa, mjukuu na dereva wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ilani ya uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 - 2010 iliahidi wananchi kuwa nanukuu; "sekte ya mawasiliano .....Chama cha Mapinduzi kitahimiza Serikali kufanya mambo yafuatayo; kwanza, kuboresha mtandao na huduma za simu nchini, pili, kuendelea kupanua huduma za simu za mezani na za mikononi hadi ngazi ya vijiji, tatu, kuhakikisha kuwa huduma za posta nchini zinapanuliwa hadi vijijini ili kuongeza kasi ya usambazaji barua na vifurushi, nne, kuongeza kasi ya kukua kwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika kujenga uwezo wa kuratibu na kuimarisha mfumo huo na kuanzisha mfuko maalum wenye lengo la kupeleka huduma za simu na *internet* hadi vijijini na tano, kuimarisha uwezo wa utabiri wa hali ya hewa nchini kwa kutumia vyombo vyaisi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu mawasiliano ya simu za mikononi, kiwango cha ukuaji wa shughuli za huduma za mawasiliano kilikuwa asilimia 20.1 mwaka 2007 ikilinganishwa na asilimia 19.2 mwaka 2006. Ukuaji huu ulitokana na kuongezeka kwa njia za mawasiliano kwa simu za mikononi na kukamilika kwa uwekiwa wa mitambo ya mawasiliano katika baadhi ya miji ya mikoa. Mchango wa shughuli za mawasiliano katika Pato la Taifa ulikuwa asilimia 2.3 mwaka 2007 ikilinganishwa na asilimia 2.1 mwaka 2006. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa ya hali ya umasikini na maendeleo ya watu ya mwaka 2007 (ukurasa wa 79) inaonyesha kuwa umilikaji wa simu za

mikononi umekua mara nne zaidi kwa kipindi cha miaka minne iliyopita na hili limesaidia kupunguza tatizo la mawasiliano kati ya maeneo ya Mijini na Vijijini, zaidi ya asilimia 65 ya watu wazima waishio Dar es Salaam wanamiliki simu za mikononi wakati huo huo ni 16% tu ndio wanamiliki simu za mikononi maeneo ya vijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuongezeka huko kwa matumizi ya simu za mikononi ukweli ni kuwa ongezeko hilo halijasaidia katika kukuza uchumi wa nchi yetu kwa kiwango stahiki na hii inatokana na ukweli kuwa zaidi ya asilimia 75 ya watu wanaomiliki simu wanazitumia kwa shughuli zao binafsi (*for personal purposes*), huku asilimia 25 tu ndio wanazitumia simu hizo kwa ajili ya masuala ya kibiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na taarifa hizi ni ukweli usiopingika kuwa matumizi ya simu za mikononi badala ya kusaidia kuchangia kasi ya kukua kwa uchumi na kuongeza Pato la Taifa yamekuwa yakiendeleza umaskini wa wananchi wetu, kwani simu hizo hazitumiki kwa ajili ya kufanya shughuli za kiuchumi kama taarifa inavyoonyesha kuwa simu hizo zinatumika kwenye masuala ambayo ni ya kawaida na kijamii zaidi kuliko shughuli za kibiashara na za kukuza uchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007 idadi ya wateja wa simu iliongezeka hadi kufikia 8,488,774 ikilinganishwa na wateja 5,698,441 mwaka 2006 sawa na ongezeko la asilimia 50.0. Ongezeko hili linaleezwa kuwa linatokana na kuongezeka kwa watumiaji wa simu za mikononi hapa nchini pamoja na uwekezaji wa makampuni ya simu kuongezeka. Kambi ya Upinzani inataka kuja Makampuni haya yaliingizia Taifa kiasi gani cha fedha? Je, walilipa kodi kiasi gani? Tunamtaka Waziri alieleze Bunge hili kuwa makampuni haya yalilipa kodi zipi na kiasi gani kwa kila aina na hasa makampuni ya *Vodacom*, *Celtel* (*Zain*), *Tigo* na *Zantel* kwa kila mwaka kutoka mwaka 2005 hadi leo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, takwimu zinaonyesha kuwa Makampuni haya kwa kipindi cha mwaka 2007 yalikuwa na wateja kama ifuatavyo; *Vodacom* 3,870,843, *Celtel* na sasa linaitwa *Zain* 2,505,546, *Tigo* 1,191,678 na *Zantel* 684,214 huku kampuni yetu ya *TTCL* wateja 236,493. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa takwimu hizi ni ukweli usiopingika kuwa Makampuni haya ya simu yanachukua fedha nyingi sana za Watanzania kwa ajili ya huduma za simu za mikononi. Kwa mfano kama wateja hawa kila mmoja akituma *message* moja kwa shilingi 50, kwa siku ni kuwa Makampuni haya yatakuwa yamejiingizia kiasi cha shilingi 424,438,700. Ukiondoa kodi ya VAT ambayo ni asilimia 20 utaona kuwa Serikali inapata kiasi cha shilingi 84,887,740 kwa siku, Makampuni haya yanaingiza mifukoni mwao shilingi 339,550,960 kwa siku kwa ujumbe mmoja tu wa maandishi kwa siku isipokuwa tutakapothebitishiwa wanalipa aina zingine zipi za Kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya simu za mikononi ya *Tigo* iliyokuwa na wateja 1,191,678 kipindi cha mwaka 2007 ambayo ina huduma yake kwa wateja inayoitwa *Extreme* ambayo kama mteja anataka kujisajili kwenye huduma hiyo anapaswa

kulipia kiasi cha shilingi 1,500 kwa siku na mteja ataweza kuwapigia simu wateja wa *Tigo* kwa kutwa nzima. Tukikadiria kuwa robo tatu ya wateja wake wamejisajili kwenye huduma hiyo utaona kuwa kwa kipindi cha saa kumi na mbili za siku kampuni hiyo inajingizia kiasi cha shilingi 1,340,637,750/=. Hizi hakika ni fedha nyingi sana kwa kipimo chochote kile na kwa mizania yeyote ile. Hii ni kwa siku moja tu na kwa wiki moja kampuni hii itaingiza shilingi 9,384,464,250/= kwa makisio haya ndio sababu Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kodi kiasi gani kilikusanya kutoka kwenye makampuni ya simu za mikononi ikionyesha aina ya kila kodi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa kodi ambayo ilipendekezwa na Waziri wa Fedha wakati akiwasilisha Bajeti yake kwa kipindi cha mwaka 2008/2009 isiongezwe kama alivyokusudia, kwani kodi hiyo itaenda kuwaongezea Watanzania amba ni maskini machungu zaidi kwani wao ndio wataktakiwa kulipa kodi hiyo. Kambi ya Upinzani inapendekeza kuwa makampuni haya yawe yanalipa kodi kutokana na mapato makubwa wanayopata kila siku. Hii ni kutokana na ukweli kuwa kupunguza kodi ikiwemo VAT na kodi nyinginezo kutachochea ongezeko la watumiaji wa huduma za simu. Pia athari za kodi kubwa huwaathiri moja kwa moja wananchi wa chini amba ndio wanabebeshwa mzigo huo, asilimia 24.8 ya gharama za simu ni kodi na hivyo kuwaongezea mzigo wananchi wetu maskini. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali ikiamua kuongeza kodi ya muda wa maongezi hadi kufikia asilimia 10 kama ilivyopendekezwa katika Bajeti itaifanya Tanzania kuwa nchi yenyé gharama kubwa za matumizi ya huduma za simu za mikononi Barani Afrika na hili litaidumaza sana sekta hii na itashindwa kukua.

Pia Watanzania maskini wataendelea kuumia kutokana na kodi hizi ambazo kila siku wananchi huwa wanatakiwa kulipa kila kukicha na kwenye bidhaa mbalimbali na au kutokana na gharama watashindwa kuzitumia vizuri simu zao na Tanzania itabaki nchi ya ku-beep tu jambo ambalo si lengo la umiliki wa simu za mikononi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kuwa badala ya kutoza watumiaji wa huduma za simu ni vyema sasa ikafuta misamaha ya kodi (hasa *corporate* na *income tax*) kwa makampuni haya ambayo Serikali iliwaongezea muda wa msamaha na hili linaifanya Serikali kupoteza mapato mengi sana. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia pamoja na kuwasamehe kodi makampuni haya ni kuwa hata faida ambayo wanaipata haiwekezwi hapa nchini kwani hupelekwa nje ya nchi kwa wenye hisa kwenye makampuni hayo na kuwekezwa huko, hapa ni kupaka rangi majumba, na mchango kidogo sana katika michezo, burudani au kutoa zawadi za magari kwa mtu mmoja mmoja badala ya kulipa kodi kwa maendeleo na ustawi wa nchi yetu. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza sababu zilizoifanya Kampuni ya *Celtel* kubadili jina kuwa *Zain*. Faida gani au athari gani kimapato Taifa imepata pale kampuni ya *Celtel* ilipojibadilisha na kuitwa *Zain*

tukizingatia kuwa Serikali ina hisa asilimia 40 katika kampuni hiyo. Je, Serikali ilishirikishwa kiasi gani katika maamuzi hayo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Serikali inatekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi, nanukuu; “Kuendelea kupanua huduma za simu za mezani na za mikononi hadi ngazi ya vijiji.” Sasa huu uwe ni muda wa kutekeleza ilani hiyo kwa vitendo kwa kuondoa kodi hizi kwa wananchi na badala yake makampuni haya ya simu yaanze mara moja kulipa kodi ambazo wamesamehewa na Serikali hii ambayo sasa inataka kwenda kuwadai wananchi wake maskini na kuyasamehe makampuni haya ambayo yanaendelea kujineemesha huku Serikali ikiendelea kuwakamua wananchi wake maskini kila kukicha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ubinafsishaji wa Kampuni ya Simu Tanzania (*TTCL*). Kuna taarifa kuwa ndani ya kampuni yetu ya simu kuna mikataba miwili inayofanya kazi kwa wakati mmoja na mikataba hiyo ni Mkataba wa Ubinafsishaji wa *TTCL* kati ya Serikali ya Tanzania na *MSI/Detecon* (*Celtel International* na au *Zain* kwa sasa) na wa pili ni Mkataba wa Uendeshaji wa *TTCL* kwa kutumia menejiment ya nje (*SaskTel International Inc*). Mkataba mama unamtambua *MSI/DETECON* ambaye alilipia hisa asilimia 35 kwa gharama za *USD 60 million*, fedha hizi zilikuwa ni kwa ajili ya kuiendeleza *TTCL* ila kinyume chake zilienda kuanzisha *Celtel Tanzania Ltd.* kinyume na makubaliano ya Mikataba wa awali ambayo tulielezwa ni kampuni tanzu ya *TTCL*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba huu ambao ulisainiwa tarehe 23 Februari, 2001 ulikuwa wa muda wa miaka 25 kwa *MSI/DETECON* kumiliki hisa asilimia 35. Kambi ya Upinzani inataka kupata majibu kutoka Serikalini kuwa je, hisa hizi za *Celtel International* kwa sasa zinamilikiwa na nani? Kwani tumeona kuwa kuna kampuni nyingine inaitwa *Zain* ambayo ni kampuni kutoka nchini Kuwait sasa ndio inaendesha shughuli za *Celtel* na tunaona kuwa wanafikia hata kubadilisha jina la *Celtel*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mkataba wa pili unahusiana na uendeshaji wa kampuni yetu ya simu *TTCL* kufanywa na wataalamu kutoka nje ya nchi. Mchakato wa kumpata mwendeshaji huyu ulikamilika pale ambapo mwendeshaji ambaye ni *SaskTel International Inc.* kutoka Canada ambaye alianza kazi rasmi 01 Julai, 2007 kwa makubaliano ya mkataba wa miaka mitatu na mpaka sasa ametimiza mwaka mmoja ndani ya *TTCL*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaona kuwa upo udhaifu mkubwa wa usimamizi wa Bodi ya Wakurugenzi kuweza kumsimamia mwendeshaji huyu kwani mpaka sasa mwendeshaji huyu hajaweza kupata fedha kwa ajili ya kuliendesha shirika na hata anapoenda kwenye mabenki mbalimbali huwa bodi ya wakurugenzi haishirikishwi kikamilifu kwenye kufanya majadiliano ya mikopo na mabenki hayo. Kambi ya Upinzani inataka maelezo kutoka kwa Waziri inakuwaje hawa waendeshaji wanaenda kufanya majadiliano na mabenki huku bodi ikiwa haiwakilishwi kikamilifu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (*TCRA*), utafiti uliofanywa na chama cha watoa huduma za simu za mikononi (*GSM Association*)

kupitia kampuni ya *Deloitte and Touche* imeonyesha kuwa punguzo la kodi kwenye huduma za simu huongeza idadi ya watumiaji ambao huchangia katika kukuza Pato la Taifa. Taarifa hiyo imeonyesha kuwa ongezeko la asilimia 10 ya watumiaji wa simu huchangia kukua kwa Pato la Taifa kwa asilimia 1.2. Kwa mfano, nchini Kenya mwaka 2006 simu za mikononi zilichangia asilimia tano ya Pato la Taifa na kutoa ajira kwa watu zaidi ya 200,000. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hiyo inaendelea kuonyesha kuwa ukuaji wa matumizi ya huduma za simu Barani Afrika unakwazwa na kodi mbalimbali za simu za mikononi (*excise duty*) kwa muda wa maongezi (*airtime*) pamoja na ushuru wa forodha mkubwa ambao unatozwa na hili huongeza mzigo mkubwa kwa mtumiaji wa mwisho ambaye ni mwananchi maskini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hadi kufikia mwaka 2002 kodi zilizokuwa zinatozwa kwenye huduma za simu ni *corporation tax*, kodi ya mapato, *local authorities levy* na VAT. Mwezi Julai, 2002 Serikali ilianzisha *excise duty* ya asilimia tano kwa muda wa maongezi (*airtime*) na baadaye kodi hiyo iliongezwa na kuwa asilimia saba. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, hii maana yake ni kuwa unaponunua muda wa maongezi yaani *airtime* ya shilingi 10,000/= hukatwa shilingi 3,000/= ikiwa ni kodi ya Serikali na hivyo mtumiaji huyu hubakia na shilingi 7,000/= tu kama muda wa maongezi. Vivyo hivyo kwa mtumiaji ambae anaweka shilingi 1000/= kwenye simu yake hukatwa shilingi 300/= kama kodi na hivyo kubakiwa na shilingi 700/= tu kama muda wa maongezi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, *TCRA* ni mamlaka ambayo kwa mujibu wa sheria inatakiwa kukusanya ushuru na *fees* husika kutoka kwenye mashirika na makampuni yaliyo katika sekta ya mawasiliano kwa nia ya kusimamia na kudhibiti na kuendeleza sekta hiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Mheshimiwa Waziri alieleze Bunge ni kwa nini fedha za mamlaka zilikuwa zinatumika kujenga viwanja vyatundege kama kile cha Mwanza, kujenga barabara kama vile ile Msata – Bagamoyo, Kambi ya Upinzani inashauri badala ya fedha hizo kurudishwa Hazina Kuu ya Serikali zitumike katika kuendeleza na kuboresha sekta ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, kama vile Mkongo wa Taifa, kituo cha sayansi na teknolojia au tafiti za kisayansi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutotumia mamlaka hii kuwa kama kichaka cha ufisadi badala ya kutumika kwa lengo halisi la uwepo wake, kwani kama mwekezaji ameshapewa nyaraka zote toka *TIC* kwa nini wao wanaingiza ukiritimba unaoweza kusababisha mwekezaji kukata tamaa au kutumia fedha nyingi jambo linalochangia hata huduma yake kuwa aghali sana kuliko inavyotakiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi ya TEKNOHAMA (*computer*). Matumizi ya *computer* (kinakilishi) yapo chini sana hapa nchini, kwani kwa mujibu wa

taarifa za Ripoti ya Hali ya Umasikini na Maendeleo ya Watu ya mwaka 2007 inaonyesha kuwa asilimia 90 ya wanafunzi wa shule za msingi, shulenii mwao hakuna *computer* na hata zile shule chache ambazo zina *computer* asilimia 55 ya *computer* hizo hutumika kwenye ofisi za utawala na wanafunzi hawana uwezo wa ama kuzipata au hata kuzitumia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukuaji wa matumizi ya teknolojia ya *computer* hauwezi kukua kama hali yenye ya matumizi ya nishati ya umeme ni ndogo sana hapa nchini, kwani ukiangalia kwenye Ripoti ya Hali ya Umaskini nchini kwa mwaka 2007 inaonyesha kuwa kati ya Wilaya 20 ambazo zimeunganishwa kwenye gridi ya Taifa ni Wilaya mbili tu za Hai na Mwanga ndio zipo vijijini, Wilaya nyininge 18 zote zipo mijini.

Wakati huo huo ukiangalia Wilaya 20 ambazo zimeunganishwa kidogo zaidi (au hazina umeme) zote hizo zinatokea kuwa ni wilaya za vijijini. Hii inaonyesha kuwa Teknolojia ya matumizi ya *computer* haiwezi kukua nchini kutokana na kuwa inategemea sana matumizi ya nishati ya umeme ambayo haipatikani maeneo mengi ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia kati ya Wilaya 118 zilizoainishwa kwenye sensa ya watu ya mwaka 2002 inaonyesha kuwa ni Wilaya 18 tu zina zaidi ya 20% ya watu wake ambao wanaweza ama wanatumia nishati ya umeme. Huku zaidi ya Wilaya 31 nchini zikiwa hazina kabisa nishati ya umeme na 99% hawatumii kabisa nishati hiyo. Dar es Salaam ndio mkoa ambao una matumizi makubwa ya nishati ya umeme japo nao ni chini ya asilimia 50 ya nyumba ama wakazi wake ndio wana nishati ya umeme. Hii ni hali ya kutisha sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Shirika la Posta, biashara ya posta kwa sasa ni ya ushindani na ili kwenda na ushindani huo, mteja anakuwa ni mfalme kwa maana kuwa barua na vifurushi inabidi apelekwe nyumbani kwake au ofisini kwake. Utendaji wa Shirika letu kwa kiasi kikubwa unakwamisha na mpangilio usioeleweka wa makazi yetu. Mitaa isiyoeleweka, nyumba zisizokuwa na namba kiasi kwamba mtumishi wa posta hawezi kufikisha barua kwa kufuata maelekezo ya anuani, jambo hili kwa kiasi kikubwa linachangia kuliondoa shirika letu kwenye ushindani wa kibiashara. Hii inasababisha vifurushi na barua kukaa kwenye masanduku ya posta kwa muda mrefu na hata kusababisha uharaka wa barua au kifurushi kuitwa na wakati. Hili ni tatizo lililo nje ya shirika na liko ndani ya Serikali (mipango miji). (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kama Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005/2010 inavyosema kwenye kipengele (c) kuwa ninanukuu; “Kuhakikisha kuwa huduma za posta nchini zinapanuliwa hadi vijijini ili kuongeza kasi ya usambazaji barua na vifurushi.” Kambi ya Upinzani itajielekeza kuangalia kama ilani hiyo inatekelezwa na inatekelezwa kwa kiwango gani na hasa kwa kuangalia ufanisi wa shirika hilo pamoja na utendaji wake kwa kipindi cha mwaka 2007 ili kuweza kujiridhisha kuwa Ilani hii ya CCM inatekelezeka ama ilikuwa ni njia tu ya kupata kura za wananchi huku wakijua fika kuwa hawataweza kutekeleza ilani yao waliyowaahidi wananchi wakati wa uchaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Bunge hili likaelezwa ni asilimia kiasi gani cha malengo yaliyoanishwa katika Ilani yametekelezwa wakati tunaelekea kumaliza mwaka wa tatu tangu Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2005 yaani mwaka wa Ilani husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007, barua milioni 16.9 zilitumwa na kusambazwa kupitia mtandao wa posta ndani ya nchi ikilinganishwa na barua milioni 19.9 zilitumwa mwaka 2006, sawa na upungufu wa asilimia 15.1. Barua milioni 6.8 zilitumwa nje ya nchi ikilinganishwa na barua milioni 8.2 zilitumwa mwaka 2006 sawa na upungufu wa asilimia 17.1. Ni dhahiri kuwa upungufu huu umeliletea shirika letu la posta matatizo ya kiuchumi na hasa ikizingatiwa kuwa mapato yake yanatokana na shughuli za utumaji wa barua kwa kiasi kikubwa. Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kueleza ni jinsi gani Shirika letu limejidhatiti katika kukabiliana na ushindani wa barua pepe, jambo linalopunguza kabisa umuhimu wa kutuma barua? Shirika hili lisipokuwa bunifu na kuwa na mipango na mikakati mipyta litafutika kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2007 idadi ya vifurushi vilivyotumwa nchini vilikuwa 29,000 ikilinganishwa na 36,000 mwaka 2006 sawa na upungufu wa asilimia 19.4, idadi ya vifurushi vilivyotumwa nje ya nchi mwaka 2007 ilikuwa 12,000 sawa na kipindi cha mwaka 2006, rejestra zilitumwa nchini mwaka 2007 zilituwa 452,000 ikilinganishwa na rejestra 915,000 mwaka 2006 sawa na upungufu wa asilimia 50.6. Kambi ya Upinzani inahoji huku ndio kutekeleza ilani ya CCM? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri alieleze Bunge hili kuwa kuna mkakati gani wa kukabiliana na hali hii kwani kama ikiachwa iendelee hivyo ni dhahiri kuwa shirika hili litaweza kufa kabisa kutokana na kukosa uwezo wa kujiendesha lenyewe kutokana na mapato yake kupungua. Tunaamini pia kuwa pamoja na sababu ambazo zinaweza kutolewa kuwa shirika lilipunguza uwezo wake kutokana na kukua kwa teknolojia ya upashanaji habari nchini, ila kuna ukweli kuwa shirika halijajiandaa kikamilifu kukabiliana na hali ya ukuaji wa teknolojia hiyo na hivyo kulifanya kushindwa kuendana na wakati wa sasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kumetokea mtindo wa mabasi kusafirisha barua na vifurushi mbalimbali kutoka sehemu moja ya nchi kueleka sehemu nyingine. Tunajiliza je, sheria zinaruhusu? Na kama haziruhusu Serikali inatoa tamko gani kwani hali hii ndio inapelekea Shirika letu la Posta kukosa wateja na hivyo kupunguza uwezo wake wa kujiendesha. Na pia je, wenye mabasi haya wanalipa kodi kutokana na vifurushi hivyo? Kwani wanajipatia fedha nyingi kutokana na kusafirisha mizigo hiyo ambayo Shirika la Posta linapaswa kufanya kazi hiyo. Inakuwaje wenye mabasi ya kusafirisha abiria wanafanya bisha ya kusafirisha vifurushi na fedha? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, moja katika lengo kuu la sera ya sekta ya posta ni ushirikishwaji wa sekta binafsi katika kutoa huduma za posta. Kambi ya Upinzani inauliza ni kweli hata vyombo vya usafirishaji abiria vinaingizwa katika kutoa huduma hiyo na kama ndiyo je, katika kutoa huduma hiyo wanapewa leseni kutoka TCRA? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla utaweza kuona kuwa ufanisi wa shirika letu la posta umepungua sana kwa mwaka 2007 na hata shughuli zake kupungua sana nchi nzima, hii hali haipaswi kuachwa kama ilivyo kwani shirika hili ni muhimu sana kwenye nchi yetu. Kambi ya Upinzani inamtaka Waziri aeleze Wizara yake ina mkakati gani wa kukabiliana na hali hiyo, na pia shirika hili linajjiandaa vipi kukabiliana na mabadiliko ya kukua kwa teknolojia ya habari ulimwenguni?

Aidha, Kambi ya Upinzani inataka kujua hatma ya jengo la Posta ambalo tunataka lirezeshwe kwa Shirika la Posta na mtaji amba Serikali imetoa kwa ajili ya kuliwezesha shirika kujiendesha kibiashara licha ya kufutiwa madeni yake, mtaji unaopaswa kutolewa na Serikali, hii ni kwa mujibu wa sheria iliyopitishwa na Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhus Idara ya Sayansi na Teknolojia, katika Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2007/2008 mojawapo ya mambo ambayo yalitarajiwa kutekelezwa ni kuwekeza zaidi katika utafiti pamoja na matumizi ya sayansi na teknolojia. Hili ni jambo zuri lakini, kuna teknolojia za kila aina na zinatofautiana kulingana na sekta husika. Hivyo basi, Kambi ya Upinzani tunamtaka Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi utafiti huu kwa sasa unafanyika katika nyanja zipo kwani itakuwa ni uharibifu na matumizi mabovu ya raslimali kama hatutaweka nguvu sehemu moja ya teknolojia na kupata matunda yaliyokusudiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo ilikuwa ni kuendeleza majadiliano na India kuhusu uanzishwaji wa vituo vya Sayansi na Teknolojia (*Science Parks*). Kambi ya Upinzani inataka Serikali kueleza vituo hivyo vimejengwa wapi na vinatumikaje kwa vijana wetu? Na Serikali imeanza kunufaika vipi na vituo hivyo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania kwa sasa imebahatika kuwa na maeneo mengi yaliyo na madini ya *Uranium*, madini ambayo yanazalisha nyuklia, na sio hilo tumbali yanaweza kutumika kuzalisha nishati mbalimbali kama umeme. Hivyo basi, itakuwa ni vyema Serikali ikalieleza Bunge hili sera ya nyuklia imefikia wapi? Kwani sasa hivi madini yetu wanaonufaika au watakaonufaika nayo ni wengine na sisi hatujui ni kwa kiasi gani cha *Uranium* tunayo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kambi ya Upinzani inahitaji kujua kituo cha Kilimo na Bioteknolojia cha Taifa kilichotarajiwa kujengwa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kimefikia hatua gani? Aidha, kwa kuwa kulikuwa na utata uliokuwepo kuhusiana na matumizi ya bidhaa za kilimo ambazo zimezalishwa kwa kubadilisha uasaili wake wa genetiki yaani *Genetic Modified Organ (GMO)*, Serikali inasema nini kuhusiana na utata huu? Je, kituo hicho kinajengwa bila ya kuwepo kwa sera na sheria ya *GMO*? Kama hivyo ndivyo kitakuwa kinafanya kazi kwa mwongozo upi?

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Taasisi za Sayansi na Teknolojia za Dar es Salaam na Mbeya, ni ukweli uliowazi kuwa taasisi hizi zinatakiwa kuwa ndio chimbuko na endelezo la vijana wetu kwenye karne hii ya sayansi na teknolojia. Hii inatokana na ukweli kwamba kuna teknolojia rahisi ambazo vijana wetu katika taasisi hizo wamezigundua lakini wamekosa usaidizi kutoka Serikalini. Mfano, vijana wa *DIT*

wamejitalidi kutengeneza mfumo mzuri na rahisi kwenye taa za barabarani, swali ni kwa nini Serikali kupitia kitengo chake cha *TEMESA* wasishirikiane nao katika kuendeleza pale walipoanzia na kufikia wataalam hao wa *DIT?* (*Makofi*)

Aidha, kuna haja gani ya kuagiza taa za kuongoza magari toka nje wakati vijana wetu wanaweza kutengeneza hapa hapa nchini? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kubadili mtazamo na kuanza kutumia vifaa vyetu wenyewe na hivyo ndivyo walivyofanya mataifa yote yaliyoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mpango wa Serikali kuhusiana na taasisi hizi, hauonyeshi ni kwa vipi Serikali itatumia kwa manufaa wahitimu wa taasisi hizi kwa manufaa ya Taifa kwani, inaonyesha mkazo umewekwa katika kudahili tu, je, wanaohitimu wanaachwa tu bila ya kuwepo kwa utaratibu mahsus wakutumia hazina hiyo? Kambi ya Upinzani inaitaka Serikali kutoa ufanuzi kuhusu wataalam hao wanaohitimu katika taasisi hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo kwa niaba ya Kambi ya Upinzani, naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Asante sana kwa kuwasilisha vizuri hotuba yako. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, sasa kwa utaratibu mzuri wa *ku-manage* mambo haya, wale wanaoomba wakiwa wamemalizika katika kipindi fulani, inakuwa vizuri zaidi kwa sababu kuna wengine wameomba mapema, anatokea mwingine hajawahi kuchangia hata mara moja, anakuja kuomba jioni, sasa ana-*interrupt* wale waliowahi. Kama unataka kuzungumza, jipange vizuri mapema, ujulikane na sisi tupange tujue tuna muda gani na namna gani. (*Makofi*)

Kwa hiyo, sisi hapa hatutapokea maombi mengine sasa, tumekamilisha hayo. Ni vizuri tukafanya... unajua kabisa utazungumza Wizara hii, kwa nini unakuja kuomba kesho jioni? Sasa tutakunyima tu sisi hata kama hujachangia hata mara moja. Sasa atakayechangia wa kwanza atakuwa Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, ndiye atakayeanza kama yupo, atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge, atafuatiwa na Mheshimiwa Raynald Mrope na atafuatiwa na Mheshimiwa Dr. Luka Siyame. Mheshimiwa Abdisalaam yupo? Hayupo! Kwa hiyo basi atakuja na Mheshimiwa Anthony Diallo. Basi tunaanza na Mheshimiwa Dr. Binilith Mahenge. (*Makofi*)

**MHE. DR. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii nikawa mchangiaji wa kwanza kwenye hotuba hii muhimu ya Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, na nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri, ye ye pamoja na Naibu wake na watendaji wa Wizara kwa kuandaa hotuba hii nzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kuchangia hotuba hii kwa sababu nafahamu sana kwamba maendeleo ya nchi yoyote ile, nchi zilizoendelea na nchi zinazoendelea yanategemea sana maendeleo ya sayansi na teknolojia. Hilo limethibitika katika nchi zilizoendelea na linaendelea kuthibitika katika nchi zetu hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni wazi kabisa kwamba ili maendeleo ya sayansi na teknolojia yaweze kupatikana, lazima tufanye maandalizi na tufanye maamuzi. Lakini ukiangalia sekta hii imekuwa haipewi kipaumbele, haipewi kipaumbele katika Bajeti na la kushangaza sana ambalo sisi Watanzania tunaliweza, tunaandaa sera nzuri sana, sera ambazo zinaelezea namna ya kutekeleza suala zima la sayansi na teknolojia. Hapa nina sera ya sayansi na teknolojia ya mwaka 1996 ambayo Mheshimiwa Waziri amesema anafanya mkakati wa kui-review upya. Lakini tulitegemea tupate majibu kwamba hii sera toka ilipokuwa imeundwa imefanikiwa kwa kiasi gani na mnapo-review leo hii, mnataka ku-review nini! Kwa mfano, ukiangalia *enrolment* ya wanafunzi wanaoingia Vyuo Vikuu tulitegemea kwamba *enrolment* ya wanafunzi wanaojiunga na masomo ya sayansi iwe kubwa zaidi kama inavyoolekezwa kwenye sera hii ya sayansi na teknolojia kwamba *enrolment* iongezeke kuanzia *level* ya sekondari na hadi Vyuo Vikuu. Lakini ukichukua hiyo *enrolment* utagundua kwamba wanafunzi wanaosoma sayansi ni wachache sana. Kwa hiyo, ni wazi kwamba hatuwezi kupata mapinduzi ya sayansi na teknolojia kwa sababu watalaam tunakuwa hatuna. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimekuwa nikijiuliza vile vile hawa wengi tunaowapata wa Vyuo Vikuu ambao hawachukui sayansi na masomo ya *art*, najiuliza, watakapolaliza watafanya nini kwa sababu tukiwa na wanafunzi kwa mfano, 21,000 waliokuwa *enrolled* mwaka uliopita, kama ingekuwa kati yao 15,000 ni watu wa sayansi, basi tungetegemea kupata mabadiliko makubwa sana. Lakini kama unakuwa na 15,000 ni watu wanaosoma masomo ya *arts* ambao hawawezi kuumba kitu chochote, hawezi *ku-create* kitu chochote, mimi nadhani hapa unakuwa unaandaa bomu lingine la watu watakaohitaji kazi utakuwa huna kazi ya kuwapatia. Wakati ungekuwa na wanasayansi na teknolojia wengi, hawa wanaweza kutekeleza azma nzima ya kujitegemea kwa sababu wanaweza kujiajiri na waka-*create* kazi mbalimbali kwa ajili ya hawa wengine ambao wanasoma masomo ya kawaida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nimejiuliza tatizo ni nini, tulipokuwa tunaongelea suala la utawala bora, tulisema kwamba utawala bora unapimwa kwa *dimensions* kama sita na mojawapo ambayo niliisema wakati ule ni namna Serikali inavyoweza kutekeleza zile sera ambazo zinaandalisha (*Effectiveness of the Government to implement*). Sasa kwenye sera hii ya sayansi na teknolojia inaeleza wazi kabisa kwamba wakati mipango inapofanywa ya Taifa (*National Development Planning*) ihakikishe kwamba ina-*incorporate* wataalam wa sayansi na wa teknolojia ili waweze kuweka vile vipaumbele vya maendeleo. Hilo halitekelezwi na ndio maana maamuzi yanayotolewa yanakuwa ni yale ambayo yanaelekeza kuwa na wataalam wengi ambao siyo wanasayansi na ambao hawawezi kuleta mabadiliko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vile vile tunaona wazi kabisa kwamba mapungufu ya utekelezaji wa hizi *policy* ambazo tumeziweka sisi wenyewe ndiyo yanayojionyesha wazi kwamba tunashindwa kwenda mbele zaidi. Naomba ninukuu kipengele cha hii *Policy* ya mwaka 1996 ukurasa wa 42 kwa idhini yako Mheshimiwa Naibu Spika; “*Incorporation of science and technology in the national economic plan.*” (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Kifungu cha 70 anasema; “*national science and technology implementation plan should be fully integrated into the overall national development plans which in turn must influence and be influenced by the national science and technology policy.*” Na anaendelea kusema; ... “*for a national science and technology system to become an effective instrument for development particularly in solving problems affecting the majority of the population, political commitment at the highest level for government should be secured and this political commitment should be then translated into increased resource allocations to science and technology.*” Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuangalia tu haya hayatekelezwi na ndio maana nataka kuiomba sana Serikali ya Awamu ya Nne kwamba kama tunataka kuona mageuzi ya sayansi na teknolojia, lazima tuwekeze pamoja na kuwekeza kwenye vitu vingine, lakini tuwekeze kwenye *human resources*, kuandaa watalaan mbalimbali katika sekta hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuwa nikifuatilia sana hotuba za Mheshimiwa Rais na hotuba za Mheshimiwa Waziri Mkuu ambazo zinasisitiza sana umuhimu wa kuendeleza sayansi na teknolojia, lakini kuna *gap* pale kati ya hotuba za viongozi na watekelezaji (*Implimentation*) haupo. Kwa hiyo, naomba kutoa mapendekezo kwamba tuhakikishe tunawashirikisha wanasayansi na *technologists* tunapoandaan mipango yetu hii ya sayansi na teknolojia ili tuweze kupata mafanikio. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pointi yangu ya pili ambayo nadhani vile vile inajitokeza kwa sababu ya muono mzima wa wenzetu wanaofanya maamuzi kwamba wanaofanya maamuzi ya sayansi na teknolojia inawezekana pengine wao siyo wanasayansi, siyo *technologists*, huenda ni wanahistoria kwa hiyo ndiyo maana nilipokuwa naangalia kwenye vitabu vyote viwili nya Bajeti, sikuweza kuona fungu lolote ambalo kimetengewa Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya, hamna! Nahitaji sana kupata maelezo kutoka kwa Mheshimiwa Waziri, kama mwaka jana Waziri Mkuu alisimama hapa akasema kabisa kwamba Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya kitaendelea kwa mwelekeo ule ule, lakini kitatoa mpaka *PhD* kama alivyothibitisha Waziri mwenyewe. (*Makofi*)

Sasa watalipa hela kutoka wapi? Hela zinaidhinishwa na Bunge hapa, mle ndani hamna fungu. Lakini vile vile hata Chuo kilichoandikwa mle; Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam, wametengewa shilingi milioni 60, watafanya nini? Na kama kuna hela nje ya hapo, basi zionyeshwe kwenye vitabu hivi ili sisi tunaofanya maamuzi tuzione na tujue kwamba kutakuwa na mabadiliko ya sayansi na teknolojia. (*Makofi*)

Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri atakapokuwa anahitimisha, atueleleze ni kwa nini Chuo cha Sayansi na Teknolojia cha Mbeya hakina fungu kwenye vitabu vyote viwili, kitu gani kimetokea? Inaonyesha wazi kwamba ile Wizara iliyokuwa inakaa pale, inawezekana pale, ni mtu ambaye hajui kabisa suala la ufundi na hii sera hajaipitia ndio maana ikaja haina *content* ya sayansi na teknolojia kwa upande wa Chuo cha Mbeya na

kidogo kwa upande wa *DIT* na hata *COSTECH* wamepewa hela kidogo sana kama shilingi milioni 400, watasimamia vipi, wata-*promote* vipi viwango vyā sayansi na teknolojia katika nchi! Kwa hiyo, nilitaka niseme hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu kuhusu Taasisi hizi mbili, *DIT* na *MIST (Mbeya Institute of Science and Technology)*, napenda kumpongeza Waziri kwamba wameweka mikakati ya kuona kwamba vyuo hivi vinatoa Stashahada, Shahada na mpaka kutoa *Degree za PhD*. Hili ni wazo zuri na nakumbuka mwaka jana Waziri Mkuu aliposema suala hili, alilinganisha mawazo yetu ya kuwa na vyuo kama hivi vinavyolingana na *MIT* ya Marekani (*Machushita Institute of Technology*) na vile vyā *Institute of Technology* vyā India. (*Makofi*)

Lakini inaonekana kwamba sisi ni wazuri wa kulinganisha, lakini siyo wazuri wa kwenda kwenye vitendo, kwa sababu ili tuweze kufuata vyuo kama vyā Marekani vyā *MIT*, basi ni lazima hadhi ya vyuo hivi vyā *DIT* na *MIST* viwe na hadhi sawa ya Chuo Kikuu na vinaweza kupata hadhi vipi ya kuwa Chuo Kikuu kwa sababu kama leo tunasema vyuo hivi viwe vinatoa *degree*, basi *degree* yake iwe ndiyo ile ile inayosimamiwa na Vyuo vingine Vikuu. Inaweza ikatokea vipi hili, basi maana yake ni kwamba lazima anayetoa ithibati awe ni mmoja kwa vyuo hivi ndipo kutakuwa na *competitiveness* ambayo ni sahihi zaidi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini siyo hivyo tu, hatuwezi tukaenda kutafuta kazi katika soko la *SADC* au *East Africa* tukiwa na *degree* mbili, nyingine inatolewa ithibati na mtu mwengine na nyingine na mtu mwengine, nadhani hapa tutakuwa tunajikanganya ndani ya nchi yetu. Kwa hiyo, namuomba Mheshimiwa Waziri waone namna ya ku-*liais* kati ya *NACTE* na *TCU* ili kuona ni namna gani ithibati ya *degree* zinazotolewa na vyuo hivi, basi iwe ni ile ile inayotolewa na Vyuo Vikuu vyā nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, toka tumepata Uhuru, tumekuwa na Vyuo vitatu tu vyā Ufundu; tulikuwa na *Arusha Technical College* na Mbeya na ambavyo hivyo viwili sasa vinaanza kwenda katika *level* ya kuwa Vyuo Vikuu. Tatizo lililojitekeza ni kwamba hatuwekezi kwenye ufundu, vyuo vimebaki vile vile. Mwanzoni kulikuwa na wazo la kuwa na *Technical College* kila *Zone*, hilo limekwenda mpaka likafa. Kwa hiyo, napendekeza kama kweli tunataka mageuzi, tunatakiwa tuwe na hii *cadre* ya *Technicians* kwa wingi, Wahandisi kwa wingi ambao wanaweza kuumba vitu. Hatuwezi kuwapata kwa kuongea, tutawapata kwa kufanya vitendo na hasa Serikali ijielekeze basi kufungua vyuo kama hivi angalau kila Mkoa. Kama Ilani leo inasema kwamba tuwe na Chuo cha *VETA* kila Wilaya, nilidhani kwamba basi kuwe na mkakati wa kuwa na *Technicla College* katika kila Mkoa, hii itasaidia kuwa na idadi kubwa ya watalaam ambao wanaweza wakasaidia kuleta mapinduzi ya sayansi na teknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati nachangia huko nyuma, niliwahi kuelezea tatizo kubwa la mawasiliano katika Wilaya yangu ya Makete. Wilaya ya Makete kijiografia ina milima, kwa hiyo, ile mitandao iliyowekwa kuna baadhi ya kata ambazo hazipati kabisa mawasiliano na nilishamuomba Mheshimiwa Waziri kwamba nina kata yangu moja ya Ikuwo ambayo yenye we imezungukwa na milima na hawana mawasiliano

hayo yote. Ningependa akihitimisha, basi aweze kunisaidia kwamba anawasaidia vipi wananchi wangu wa Makete wale waweze kupata mawasiliano mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimalizie kwa kumuomba Mheshimiwa Waziri atoe ufanuzi ni kwa nini kwenye Bajeti hamna fungu la Chuo cha Taasisi ya Teknolojia Mbeya na atoe vile vile angalizo kwamba watafanya nini ili kuona kwamba hivi vyuo vinapata hadhi sawa na Vyuo Vikuu hata kama vinaendelea kwa jina lao lile lile la Taasisi ya Teknolojia, lakini viwe na hadhi sawa na Chuo Kikuu ili tuweze kuwa na watalaam ambao wataenda kwenye soko la ajira na kuweza kujitegemea. Nashukuru sana, ahsante! (*Makofi*)

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii ili nami nitoe mchango wangu mdogo katika Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa bahati mbaya nina mafua kidogo nadhani kutokana na Nane Nane wakati wa maonyesho, kwa hiyo sauti yangu haitoki vizuri sana, mtanisamehe. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Tutakusikia tu!

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Moja, napenda sana kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia pamoja na Naibu Waziri wake. Hii Wizara ni mpya kabisa, ni mpya kwa sababu mawasiliano ilikuwa zamani pamoja na Idara ya Ujenzi, Miundombinu na kwa upande wa wa sayansi na teknolojia walikuwa na Idara ya Elimu ya Juu. Kwa hiyo, wameunganishwa pamoja imekuwa ni Wizara mpya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoshukuru ni kwamba kwa upande wa mawasiliano ni eneo moja la kujitangaza kwa sababu wana kila aina ya vyombo vya *ICT* kuweza kujitangaza. Sasa ningemshauri Waziri atumie nafasi hii kujitangaza sana, Wizara yake haieleweki, haijulikani kabisa. Huko vijijini ukiwaambia kuna Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, hawaelewi hata maana yake nini. Sasa ningeomba hii elimu itumike ili kuwaeleza wananchi wetu waweze kuelewa hasa nini kinajiri katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wizara hii mchango wangu nianze kwanza, kwa upande wa mawasiliano. Naomba niseme kwamba tulitegemea kwa hivi sasa vijijini kungekuwa na mawasiliano ya kutosha ya simu. Lakini nasikitika kusema kwamba *Detecon* wakati wanaingia mkataba wa kuanzisha *TTCL* walikuwa na mpango uliokuwa umeonesha kwamba wataeneza simu Mikoani, Makao Makuu ya Mikoa, watakwenda Wilayani na wataishia vijijini. Nashukuru kwamba mpaka sasa hivi wamekwenda Mikoani. Lakini, sasa ni muda mrefu mno Wilayani bado hatujafikiwa. Waziri kwa nini? Hebu tueleze hii kampuni inafanya nini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilikuwa na hamu sana ya kununua hizi simu za *TTCL* za Kichina ambazo zinauzwa pale Posta. Simu hizi tumezitumia kwa kutumia

*Broadband* yao kwa ajili ya mawasiliano ya *Internet* na kadhalika, lakini, mpaka sasa hivi simu hizi zinaweza kutumika mwisho Mikoani. Sasa nikienda Masasi nitatumia namna gani na hata wale wauzaji wenyewe wakawa wanashauri kwamba Mzee ukinunua hizi ni kazi bure kwenda Masasi kwa sababu hakuna mtandao. Sasa Waziri atuambie hivi ni kitu gani kinachoifanya *Detecon* mpaka leo haijafika Masasi na itafika lini? Sasa hebu fikiria Wilayani, huko vijiji, ndiyo itafika hiyo? Sasa ningeomba sana katika Wizara hii, ingawa ni mpya, hebu gani wanaweza kufika kijijini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili katika mawasiliano hayo hayo, jamani gharama za simu hasa hizi simu za mkononi ni ghali mno kwa Watanzania wa kawaida. Mimi nalinganisha, ukipiga simu Marekani kwa dola tano, katika dakika tano tu simu inakatika. Mtu akikupigia simu toka Marekani kwa dola tano zile zile mnaongea kwa dakika 45. Sasa, maana yake nini yaani yule unaongea naye mpaka unaishiwa na cha kuongea, unaweza hata ukakusanya mbuzi, wakaja wakacheza pale na nini..., bado hamjamaliza. Lakini upige toka huku kwetu, dakika mbili tu kwisha! Tafadhalii, msilifanye Taifa letu liwe la *ku-beep*, ni lazima muone jinsi gani tunaweza kupunguza gharama na mimi nafikiri hawa wawekezaji hawa walikuja kuwekeza, wanataka kurudisha pesa zao kwa muda mfupi. Sasa Serikali ni lazima muangalie, muwe wajanja. Kurudisha pesa zile, gharama lazima iwe ya muda mrefu. (*Makofii*)

Sasa hivi wanatu-*charge* mno, yaani kuna programu nyingi sijui ya *extreme* ya nini na nini, yote danganya toto. Ukienda *Zantel* watakuambia hivi, ukienda sijui *Celtel* hao, ukienda *Tigo* kila mmoja atakwambia anampa huyu, kumbe ni danganya toto, wao wenyeewe wanapata fedha nyingi zaidi kuliko sisi manufaa tunayoyapata. (*Makofsi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya mambo ya TCRA kama ipo, hebu ituangalizie, iangalie ni jinsi gani wananchi wa Tanzania wanavyoweza kufaidika kutokana na teknolojia hii, kutokana na kutumia mawasiliano haya ya simu ili wananchi waweze kupata faida zaidi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoka hapo, niingie upande wa sayansi na teknolojia. Kwa kweli sayansi na teknolojia nchini hajaelewaka vizuri na watu hawaelewi kwamba wanaweza kutumia sayansi kwa maendeleo yao, tungetumia vitu rahisi tu katika kuelezea na kwa kuitumia hii Wizara yetu. Kwa mfano, wenzetu wanaotoka Ukanda wa Ziwa Victoria, jamii za Wasukuma ambao ni wafugaji wakubwa, Wasukuma wangejua kwamba kutokana na mavi yale ya ng'ombe, wanaweza wakatengeneza gesi ya kupikia, wanaweza wakatengeneza umeme, mbona tungekuwa mbali! Lakini hawana habari wale ndio maana Wasukuma wamesambaa sambaa wamefika mpaka kwetu siku hizi, hawana habari kwamba yale mavi ya wanyama wao yangewza kuwasadia sana sasa. (*Makofsi*)

### **NAIBU SPIKA:** Kinaitwa kinyesi!

**MHE. RAYNALD A. MROPE:** Kinyesi eeh, kingeweza kusaidia sana katika kutengeneza nishati ambayo itawasaidia wao wenyewe kwa kupikia na kwa kuona. Humo humo kuna nishati hii ya kutumia mapangaboi kwa ajili ya kutengeneza umeme (*windmills*) nayo hakuna *effort* zozote za kukuza teknolojia ile vijijini. Sisemi juu hili lililojaa kila mahali. Hatuelekezi nguvu zetu kwenda kuhakikisha kwamba lile juu linatunufaisha ili tupate ile *Solar Power*.

Mheshimiwa Spika, sasa mimi ndio nasema mambo haya madogo madogo haya kwa sayansi na teknolojia, hawa ndio wangeweza kuwaendeleza wananchi wetu kwa kutumia hiyo sayansi walionayo katika makabrasha mbalimbali. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunavyo hivi Vyuo vyetu vya Mbeya na pale Dar es Salaam. Sasa hivi tumegundua gesi, tumegundua gesi nyingi kabisa. Nimeangalia katika vitabu hivi, sikuona chuo chochote ambacho kitakuwa kinafundisha mambo ya gesi kubadili kuwa umeme, gesi kuisindika ili iwe *Compressed Natural Gas (CNG)* kwa ajili ya matumizi ya majumbani, jikoni na hata kuuza nchi za nje. Sasa haya ndiyo mambo ambayo ni muhimu tuyaangalie katika sayansi na teknolojia. (*Makofî*)

Mimi naomba sana Waziri katika *syllabus* zenu hebu badilini. Kwa mfano, kule *Mnazi Bay* sasa hivi tuna shida ya mainjinia kwa sababu wengi wamejifunza teknolojia ya kutengeneza umeme kwa njia hizi mbalimbali, lakini kwa upande wa gesi hatuna watalaaam. Kwa hiyo, hebu tusaidieni, sisi tunataka kutumia sana hasa kwa maeneo yetu, tunataka kutumia gesi ili iweze kutunufaisha. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa katika hilo, nataka kuwaeleza wananchi wa Jimbo langu la Masasi kwamba sisi ambao tutatumia gesi ile kwa umeme kuanzia Jumatatu ijayo, Kampuni ya *ARTUMAS* itakuwa inapita katika vijiji vyetu ili kuhamasisha wananchi waweze kutumia umeme wa gesi. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mpango tulionao ni kwamba wataanza sehemu za Mkungu, wakitoka Mkungu, watakenda Mkweria, wikitoka Mkweria watafika Nanganga, watafika Nangoo, kutoka Nangoo watafika Liputu, kutoka Liputu watafika Mwena kufanya semina za kuwaelewesha wananchi nini maana ya umeme unaotokana na gesi, jinsi ya kutumia utakapounaganishwa. Kwa hiyo, nawaomba sana wajitokeze kwa wingi katika mikutano hii ili waweze kuelewa faida gani zaidi watapata katika kutumia teknolojia hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naona kwamba mambo sasa yanaanza kuiva zaidi kwa upande huu, kwa hiyo, nawasihi sana ndugu zangu waanze kwa wingi kabisa kujitokeza ili wapate manufaa ya hiyo mikutano watakayofanya *ARTUMAS* pamoja na wasaidizi wangu wanaotoka katika ofisi yetu ili kuwaeleza sawa sawa zaidi wananchi watafaidika namna gani. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka kusema kwamba tafadhali tutumie teknolojia na hasa teknolojia ya kisayansi na ifundishwe katika vyuo vyetu, siyo tu hiki cha Dar es salaam na Mbeya, lakini hata *VETA*, kwa sababu gesi iliyosindikwa, jamani inaweza ikatengeneza mambo mengi kama hayo ma-expel tunayozungumzia, ndani mle kuna gesi

iliyosindikwa, ukitaka kutengeneza bidhaa mbalimbali zilizoongezewa thamani za kilimo, kwa mfano *juice* ukitaka kuiweka kwa muda mrefu unatumia gesi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa haya ndio mambo ambayo ningependa na kushukuru kwamba Wizara hii iweze kujielekeza zaidi kwa kuwafundisha wananchi kwa kupitia semina, kwa kufundisha watalaan na watalaan hawa kuwasambaza sehemu mbalimbali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana, huo ndio ulikuwa mchango wangu katika suala hili la sayansi na teknolojia. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Haikuonyesha kama ulikuwa na mafua, umesema vizuri tu! (*Makofi/Kicheko*)

**MHE. DR. LUKE J. SIYAME:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue fursa hii kwa niaba ya wananchi wa Wilaya ya Mbozi hususani wale wa Jimbo la Mbozi Magharibi kukushukuru wewe kwanza kwa kunipa fursa hii ili niweze nami kushiriki katika kuchangia hoja ya Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. (*Makofi*)

Pia, napenda nimpongeze Mheshimiwa Waziri kwa hotuba yake nzuri ambayo kwa hakika imeelezwa kwa upana na kwa upeo mzuri, napenda pia nimpongeze Naibu Waziri wake ambaye kwa hakika katika Wizara hii ni mzoefu na pia Katibu Mkuu, watendaji wa Wizara, Taasisi na hata makampuni ambayo yapo kwenye Wizara hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba nijielekeze hususani kwenye sekta ya mawasiliano nikianza na mawasiliano ya simu. Kwa hakika sasa hivi tunaweza kusema tumepiga hatua kubwa katika kuenyeza mtandao wa simu hususani zile za viganjani hapa nchini na toka uchaguzi wa mwaka 2005 hadi hivi sasa tumepiga hatua kubwa kwa maeneo mengi, japo kule kwetu Wilayani Mbozi hususan Jimbo la Mbozi Magharibi mtandao wa simu kwa eneo kubwa bado ni ndoto tu, eneo hili lenye eneo la mraba wa takribani kilometra za mraba 6,275 kati ya zile kilometra za mraba 9,775 za Wilaya ya Mbozi halina mawasiliano ya simu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunazo Kata 11 Jimboni, kati ya hizo mtandao wa simu hususan hizi za viganjani unaweza ukapatikana katika Kata nne tu, sehemu nyingine sharti watu wapande kwenye miti ama vichuguu ndiyo waweze kusikiliza hizo simu, hivyo basi katika taratibu ile ile kama nilivyosifia kwa sehemu zingine naomba haya makampuni ya simu yawe na jicho la huruma na kuelekeza mitandao yao ya simu kwenye Jimbo hili la Mbozi Magharibi na sehemu nyingine ambazo ziko Wilayani Mbozi ambazo pia hazina mawasiliano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaamini kabisa eneo lile kama litakuwa na mtandao wa mawasiliano ya uhakika inaweza kupiga hatua mbele kwa haraka kimaendeleo kwani rasilimali zipatikanazo kule ni za aina mbalimbali ukianzia madini mazao na hata maeneo

maarufu ya utalii kama watu wanaweza kupata mawasiliano yakaimarishwa basi tunaweza kuona vitu ambavyo katika nchi hii vinapatikana kule tu na si kwingineko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba baada ya kusema hivyo nijielekeze kwenye mtandao wa posta. Kwa hakika huduma za posta kama ilivyo kwa nchi nzima zinatia huruma kwani shirika hili limefikia hatua ambayo kama Serikali haiwezi kuchukua hatua za haraka kuliokoa kwa upande mmoja ni ya kufedhehesha kwa sababu imetokea hapo siku chache za nyuma wananchi wakituma fedha zao hasa kwa njia ya *money fax* ama *EMS* na zikazidi shilingi laki moja basi yule mtu anayetumiwa hana ruhusa ya kuchukua pesa zake mpaka kibali kitoke makao makuu wakati ile pesa ni yake ya halali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaishukuru Serikali kwa kuhakikisha imechukua dhamana ya madeni ya shirika hili na tungependa baada ya hapo wafanyakazi wa shirika hili la posta waonyeshe juhudhi na kuweza kurejesha huduma zao kama ilivyokuwa hapo awali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hivyo naomba nijielekeze kwenye shughuli za sayansi na teknolojia, kama nilivyokwishakusema mwanzo kwamba bila sayansi na teknolojia hakuna maendeleo. Sasa hivi kuna uhaba mkubwa wa wataalamu wa mambo ya sayansi na teknolojia katika nchi hii na katika Bajeti hii mimi naweza kusema haitoshi kuweza kujivunia kwamba ifikapo mwaka 2010 tunaweza tukawa na wataalamu wetu wa kujitosheleza kwa kiwango angalau cha kuweza kusema tunao watu wetu maana malengo yaliyokuwa yamewekwa hapo mwanzo kwa mfano Chuo kama kile cha ufundi cha Mbeya yamekuja yakapotoshwa na hivi sasa inaendelea kuwa ni Taasisi ya Ufundsi ya Mbeya na hata hivyo pesa ambayo imetengewa haielekei kuweza kuonyesha kwamba kutakuwa na maendeleo yoyote katika ufundishaji ama uenezaji wa sayansi na teknolojia katika nchi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naiomba Serikali ijielekeze zaidi katika kuhakikisha mafunzo ya elimu ya sayansi na teknolojia yanapewa kipaumbele zaidi na kwa sababu kuna vyuo ambavyo wakufunzi na wanafunzi waliopo hapo kwa kweli wameweza kuonyesha juhudhi kubwa ya ubunifu kama wangeweza kupewa msaada zaidi ninaamini hatuna sababu ya kuweza kuagiza vitu kwa ajili ya sayansi na teknolojia kutoka nje maana hawa watu wana uwezo wa kuvitengeneza wakipewa msaada wa kifedha na hata ile nafasi ya mafunzo zaidi ili waweze kuboresha utaalamu wao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongee hasa kuhusu mambo ambayo hawa wataalamu kama wangeweza kupewa nafasi wangeweza wakalifanyia hili Taifa na tukaondokana na matatizo mengine kwa mfano mambo ya usambazaji wa umeme katika maeneo mengi. Kama walivyosema wasemaji waliotangulia kwamba tuna rasilimali ya nishati inayoweza kutengeneza umeme kutokana na upemo, jua na hata mabaki ya chakula na tako ambayo kwa kiasi kikubwa badala ya kuweza kutengenezea nishati ya umeme hivi sasa kitu kinachozalisha ni inzi ambao wanasantabaza magonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, naishauri Serikali kwa sababu hivi sasa Jiji kama la Dar es Salaam hata hii Miji mingine ambayo tako zake zinazozalishwa kwa siku kwa

kiasi kikubwa zinaweza zikakusanya na kuweza kutengenezewa nishati ya umeme, Serikali ifanye juhudhi ya kuweza kuhamasisha makampuni na hata watu binafsi kuweza kuanzisha viwanda vya kuweza kutengeneza hiyo nguvu ama nishati kutokana na hizo taka. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa leo niliona niseme hayo machache ambayo naamini Serikali, taasisi na kampuni binafsi ambazo zinajishughulisha na sayansi na teknolojia zikiweza kutoa vipaumbele basi inaweza kuwa ni hatua moja ya kuweza kutupeleka mbele kimaendeleo, nakushukuru na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**MHE. BENSON M. MPESYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nikushukuru sana kwa kuniona ili na mimi niweze kuchangia katika hoja ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nimhakikishie Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwamba ninawaunga mkono katika hotuba nzuri iliyotayarishwa pamoja na watendaji wote wa Wizara hii naamini kabisa mmeefanya kazi nzuri sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze mchango wangu huu kwanza nirejee *Hansard* ya tarehe 20 Julai, 2007. Wakati nikichangia hasa kuhusu *MIST* kule Mbeya, majibu yaliyotolewa na Serikali ni kama yafuatayo, kwanza nianze na hili la Nelson Mandela *Institute*, nadhani Mheshimiwa Waziri amejitahidi sana kueleza inawezekana pale mwanzo hakueleweka lakini baada ya maelezo yake hapa ameeleza kwamba ni vitu viwili tofauti, *Mbeya Institute* itabaki kama *Mbeya Institute* itaendelea kufikia malengo hata ya kutoa *PHD*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa hili lakini nikirejea ukurasa wa 35 na 36 katika hotuba ya Waziri anaeleza kwamba kama sehemu ya kutekeleza haya ambayo tulikubaliana kuanzia mwaka jana kwamba imeanza mchakato wa kutoa shahada ya kwanza, naomba nimshukuru Waziri kwamba hilo linakwenda lakini nitaomba kujua *timeframe*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba leo niseme tu kwamba wahenga wanasema mpende jirani yako kama nafsi yako, na mimi nataka nikuhakikishie Waziri kama jirani yangu kwenye Majimbo nakuunga mkono katika hili lakini naomba tukumbushane tu vitu vya kawaida katika mustakabali wa Taifa hili kwa sababu nchi hii itajengwa na sisi wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza nimekuwa nikipitia *pyramid* ya sekta ya elimu, *pyramid* hii inaonyesha kwamba kunahitaji kubwa sana la upanuzi wa elimu ya juu, mimi nilimshukuru sana Mungu ulipoteuliwa kuongoza Wizara hii maana ningepangiwa Waziri mwingine asingeyaendeleza yale mazuri ambayo tulikuwa tumeanza mimi na wewe hasa kuhusu *MIST* pale Mbeya, lakini Mungu ametenda na ninaamini kabisa ataendela kutenda katika hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri utakubaliana na mimi Mheshimiwa Profesa Msolla, kuwa kuna hitaji la upanuzi wa elimu ya juu kubwa mno ukienda Dodoma hapa nafasi walizonazo na wale walioomba kwa kweli *is very alarming* katika nchi hii, wimbi la wahitimu wa mpango wa *MMES* nalo linakuja, na hakuna kipindi ambacho imeonyesha umuhimu wa sayansi na teknolojia katika kipindi kama hiki, kwanza ukisoma dira ya maendeleo utaona kwamba kumbe tukisisitiza zaidi mawasiliano, sayansi na teknolojia tutakuwa tunafanya mambo mawili makubwa, kwanza sayansi na teknolojia imeonyesha wazi kwamba inaweza kutoa ajira ya kujitegemea kwa watu wanapohitimu katika mafunzo hayo, hilo ndiyo la kwanza tukikazania hapa ni rahisi mtu aliyemaliza mafunzo pale *DIT* au kujajiri kuliko katika sekta zingine hizi tulizozizoea ambazo wanategemea *whiteman collar jobs*, hilo la kwanza katika msisitizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili tumeamua kama Taifa la Watanzania kwamba tunaingia katika mapinduzi ya kijani kukiimarisha kilimo, ni katika taasisi hizi ambapo tutapata *applied sciences*, hii ya kuhangaika na matreksa ya *KUBOTA* yanaweza yakatengenezwa *DIT*, yanaweza yakatengezwa *MIST*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nafikiri hapa haja ni kubwa zaidi lakini wakati ule mwaka jana nilikuonea huruma sana Mheshimiwa Waziri jirani yangu, ulikuwa na majukumu mengi na bila shaka hata taasisi ulizokuwa unaongoza zilikuwa nyingi sana, lakini sasa hivi umepewa kaeneo, mimi sioni, hutasita sasa mionganoni mwa vyuo vyako hivi kimoja ukakipa heshima ukakinyanyua kikawa ni Chuo Kikuu kwa ajili ya sayansi na teknolojia kikizingatia kada za kati zingine na zenyewe ziendelee kufundishwa kwa ajili ya *carrier progression*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nawashukuruni sana, tumezungumza hapa juu ya Nelson Mandela na nimeona katika vitabu vyetu tumetenga fedha za kutosha pale lakini tunamuenzi Mandela ni mionganoni mwa wazee wetu maarufu, mshairi mmoja alisema mtu chake apendacho hakina hila machoni, huridhika kuwa nacho japo hakina thamani, ni lini sisi tunamuenzi Baba wa Taifa? Tumemuenzi Mandela ndiyo hii ni *opportunity moment* sasa ya taasisi hii ambayo aliisemea sana Baba wa Taifa, tumuenzi naye tumpe Chuo chake hiki. Tumemuenzi Mandela sasa ni wakati wa kumuenzi Baba wa Taifa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiendelea katika hili tuje kwenye hili ambalo tulikubaliana mwaka jana kwamba vyuo hivi vya *DIT* pamoa na *MIST* vitaendelea mpaka kutoa Shahada za Uzamivu (*PHDs*) lakini tukaambiya wenzetu kama wale *MIST* kule Marekani na Vyuo vingine vya India ndivyo walivyofanya, lakini kila wakati tunasema Watanzania tunapolinganisha vitu tunasahau baadhi ya *components* ambazo ni muhimu, huwa tunanyofoa nyofoa tu yale maeleo ambayo tunayapenda, mimi huwa nawasikia mkisema wenzetu wa Kenya, lakini mbona hamlinganishi mishahara ya Wabunge wa Kenya na Watanzania? (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimia Naibu Spika, kama tumeamua kulingalisha tufanye ulinganifu ule, mimi nimefanya *research* kuhusu Vyuo hivi, cha kwanza ni kwamba Vyuo hivi vyote ambavyo vinakuwa katika hadhi ya Taasisi vinakuwa na *charter* ya kwake, *charter* ambayo inaonyesha yapi yatakuwa majukumu ya vyuo hivyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kingine ambacho ni muhimu ni ithibati inayoshughulikia Vyuo Vikuu ndiyo ile ile inayoshughulikia na hizi taasisi ambazo zimepewa heshima ya kutoa shahada mpaka za Uzamivu, ndivyo wanavyofanya India ndivyo wanavyofanya Marekani, sasa itawezekanaje sisi tuwaambie hawa watoe *Ph.D* lakini wakati huo huo hawa wengine wako chini ya *NACTE*, hawa wengine wako chini ya *TCU*. Tunaji-*contradict* hapo siyo kwa ajili ya soko la *SADC* lakini vie vile itakuwa ni njia ya kuepuka hizi Shahada za *dot com*, miezi sita mtu anasema nina *Ph.D* ndiyo hizi za kuziogopa hizi, lazima tuwe *consistent*, mtu atakuambia mimi ni Daktari wa falsafa ukimwuuliza amesoma chuo gani hawezi kukuambia mpaka afe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana Mheshimiwa Waziri katika muendelezo huo unaokwenda nao tunaomba bodi ya Ithibati ya Vyuo hivi ilingane na ile ambayo ni ya Vyuo Vikuu, tunaomba Vyuo hivi viwe na *charter* za kwake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kubwa lingine Mheshimiwa Waziri ambalo hata wewe mwenyewe utaenda ku-*surf* kwenye *internet* ni *funding* ya vyuo kama hivi ni kubwa sana hata mara mbili kuliko Vyuo Vikuu vya kawaida kwa sababu ya hawa watu wanafanya vitu *practically*, wanafanya *innovations*, vitu vingine hapa tunapobabaika tunawapelekea tu wao unakuta baada ya muda wametoka na jibu la kisayansi wanakuja kwa ajili ya utekelezaji, kwa hiyo, *funding* yake ni lazima iwe kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naangalia *volume two* na *volume four*, vyote hakuna mahali unapoonyesha kwamba *MIST* una-*commit* sasa wanaingia kutoa shahada, umechukia nini ndugu yangu? Si maandiko yanasema mpende jirani yako kama nafsi yako, mbona mimi leo nimekupenda nimekuunga mkono mapema, hebu niionyeshe basi hizi ulizozitenga kwa ajili ya *MIST* ziko kwenye vitabu gani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema haya tunayoyasema si kwamba tunayaokota tu, tunayaangalia na watu wengine tatizo hili la kuwa na wimbi kubwa la watu wanaohitaji elimu lilitokea Norway, wenzetu walifanyaje Norway tuangalie naomba ninukuu hapa; “*Other countries have acted to widen University access with great success, Norway pioneered their idea making a political decision to have a University in every region of the country in order to extend the ridge of higher education, a political will,*” hao walikuwa ni watu wa Norway ambao sisi ni marafiki zetu, tuangalie waliotutawala *United Kingdom* wanasesmaj; “*Similarly the United Kingdom promoted the majority of polytechnic collages to University status to enhance and support the traditional institutions.*” (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, dhambi yako Mheshimiwa Msolla iko wapi kuitangaza *MIST* kuwa Chuo Kikuu, iko wapi hapa? Hawa wamebadili *Polytechnic* kuwa Vyuo Vikuu na haya ninayoyazungumza mwezi Mei tulikaa kama *RCC* kule Mbeya, azimio moja kubwa linatamka wazi kwamba tuiombe Serikali iendelee na azma na hili lipo kwenye ilani na tunamuenzi Baba wa Taifa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niishie hapa kwa kusema ni vyema Vyuo hivi vikapewa majukumu yake kama vilivyo vyuo ambavyo tunaiga mifano yake kama vile

hiki cha *MIST* kule Marekani na vingine vya India na pia hatuna dhambi yoyote kama vingine hivi tutavipa heshima na kuvibadilisha hasa tukitegemea kwamba tutakuwa na wimbi kubwa la wanafunzi watakaomaliza kidato cha sita katika mpango wa *MMES*, tumejiandaaje katika kulipokea hili, litakuwa tatizo katika sekta la elimu, litakuwa tatizo katika mambo ya ajira ni lazima tuwaandalie hawa *venues* za kuwafanya waishi na wafurahie kwamba tuliovatangulia tumefanya maandalizi mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuunga mkono hoja hii lakini nafikiri atanipa majibu na kunipatia Chuo changu Kikuu cha Mbeya yaani *University of Science and Technology*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, maana yake ikishakuwa ni sayansi na teknolojia wazungumzaji hawamalizi muda wao, maneno machache vitendo vikubwa.

Basi mchana tukirudi tutakuwa na wachangiaji wafuatao, Mheshimiwa Abdisalaam Issa Khatib, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Anthony Diallo, Mheshimiwa John Lwanji, Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mheshimiwa Peter Serukamba, Mheshimiwa Ludovick Mwananzila, Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia, Mheshimiwa Bujiku Sakila na Mheshimiwa Kaika Telele, hawa ndiyo watakopewa nafasi jioni. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, nawatangazia kwamba Wajumbe wote wa Kamati ya Uongozi siyo ya Chama cha Mapinduzi, Kamati ya Uongozi ya Bunge kwa maana ya Wenyeviti pamoja na Tume tutakuwa na Kikao saa nane na nusu mchana, kwa kuwa hatuna matangazo mengine nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja.

(*Saa 06.53 mchana Bunge lilifungwa mpaka saa 11.00 jioni*)  
(*Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia*)

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaondoka mchana, tuliwataja watakaofuata. Tunaendelea na majadiliano.

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza jioni hii, ili niweze kuchangia hoja iliyo mbele yetu. Kwanza, namshukuru Mheshimiwa Waziri na timu yake yote, kwa kazi nzuri ambayo wameionyesha katika hotuba yao nzuri. Nina hakika ni mwanzo mzuri na nina hakika sekta hii itaweza kwenda mbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda la ujumla, kumekuwa na *tendency* hapa ya Wizara nyingi ambazo zinatakiwa *ku-head* sekta, kufikiria kana kwamba ni Wizara za Mashirika ya Umma. Ukiangalia ukurasa wa nne mpaka wa tano, unawenza kudhani kwamba, *exhaustively* hii Wizara inasimamia hizo taasisi tu siyo sekta ya mawasiliano na Sayansi na Teknolojia. Nadhani hilo limeonekana kwenye maeneo mengi. Ukiambiwa Wizara ya Utamaduni na Michezo nayo utadhani ni Wizara ya Yanga na Simba. Timu zilizoko Kigoma na sehemu nyingine hawazifahamu. Kwa hiyo, ninaomba tuwe tunajua

hizi Wizara ni za Serikali ni za nchi nzima au inapobidi ni za sekta nzima ambazo zimetajwa chini ya *instrument* hiyo iliyounda Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo ambayo ningependa labda Mheshimiwa Waziri aniambie; katika kuuza *shares* za makampuni kuna aina nyingi; mara kwa mara unapouzwa *shares* unapewa bei ambayo ni *premium*, yaani ni bei *better* kuliko *share* wakati huo zinazwaje kwenye soko la mitaji. Sasa *TTCL* tunafahamu ilikuwa bado ina-share *Celtel*. Sasa *Celtel International* wakati inauzwa kwa hii kampuni inayoitwa *Zain*, *for sure* hatukupata. Bahati mbaya wakati ule *Celtel Tanzania* haikuwa kwenye *stock exchange*, lakini ilipokuwa ni *part of Celtel international* lazima kuna *premium* ambayo ilikuwa inasababisha *share* za *TTLC* kwenye *Celtel* ziwe na bei tofauti. Sasa nilitaka kufahamu hii *transaction* ilileta manufaa gani kwa *TTLC* au walibaki na ile *book value* au fedha ambazo tulitoa kama mtaji? Kwa kawaida, nina hakika lazima kuna *premium* au kuna fedha zaidi ambazo zilitengenezwa kwa kuiiza *Celtel* ambayo ilikuwa *Celtel International* na *Celtel Tanzania* ikiwa *part of Celtel International*. Napenda nielewe faida tulizozipata.

Kuhusu mambo ya simu, napenda niyapongeze makampuni ya simu yote, ila *TTCL* nitawapongeza kidogo. Nawapongeza kidogo kwenye hii *service* yao ya *ADSL*, ambayo ni *landline* wanapositumia kwenye *data* zimekuwa ni ukombozi, tunapata *speed* kubwa kuliko tungetumia utaratibu mwagine. Upande wa *mobile*, nitapenda Waziri anieleze ni kwa nini *TTCL* waliamua kuanzisha *mobile*, lakini badala ya kutumia *GSM* wakaamua kwenda *CDMA*; kwa sababu gani *handset* zao *including* mtandao wao unakuwa hauingiliani na mtandao mwagine? Kwa hiyo, inakuwa kama mkiuza simu kwa mtumiaji ambako *TTCL* hawana huo mtandao inakuwa ni tatizo. Kwa nini tubadilishe *protocol* badala ya *ku-unify*, kwa sababu teknolojia *direction* yake ni *convergence*. Sasa ungetegemea kwamba, hata tunapochagua aina fulani ya *protocol*, nina hakika *regulator* alitakiwa kuliona hilo, *as a result* ni *duplication* ya *efforts* na *resources* ambazo zingeweza kutumika kwa pamoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa *TCRA* bado naona kuna maeneo mengi ambayo wanatakiwa kusimamia zaidi. La kwanza, ningependa sana na kila siku nalisema hili, *TCRA* wangkuwa *independent*. Hizi *regulatory authorities* zinatakiwa ziwe *independent*, zisiwe *answerable* kwa Wizara yoyote. Sababu zipo nyingi, nadhani tumezieleza kwenye maeneo mengi na juzi juzi hapa tulikuwa tunazungumzia wakati wa Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kwamba, wanakuwa na uhuru zaidi na ni kweli kwamba, wakiwa huru zaidi watakuwa na maamuzi mengine angalau Serikali haiyapendi lakini yatakuwa na manufaa kwa nchi.

Napenda niwapongeze sana, wamejitahidi sana *though* bado kuna *services* nyingi hazijaingizwa kwenye ushindani. Mfano, *domestic local fixed lines* bado ni *monopoly*. *International fixed long distance lines* bado ni *monopoly*. *Wireless lines local looping* ingawa haitumiki sana lakini *technology* bado ni *monopoly*, ambapo ingeweza kufanywa na wengine; ni teknolojia inayopitwa na wakati lakini bado ina manufaa kwenye baadhi ya maeneo.

*Data* bado kwa kiwango kikubwa ni *monopoly*. Kwenye hizi simu za mikononi ndiyo kuna *competition* na mambo mengine, lakini si kwa kiwango kinachotakiwa. Kwa hiyo, bado wana jukumu kubwa la kuona kwamba, *services* za mawasiliano nchini hapa zinakuwa huru zaidi na zinakwenda mbele zaidi, kwa sababu unavyojua wanaposema kwamba watu wenye simu za mikononi wapo *subscriber* milioni tisa. Mimi nadhani wange-*quantify* zaidi, kwa sababu ninavyofahamu mimi, mtu mmoja mara nyingi anakuwa na *line* kama nne, tano na *nine million number* nadhani ni namba ya *subscriber*. Unapokuja *head count* ya binadamu walio na simu, hatujafika milioni tisa. Kwa hiyo, ni vizuri wakati unafanya *study*, tukajua *exactly* kwa sababu ile idadi ya *Cellular Phones per 1,000 people* bado ipo chini sana ukilinganisha na baadhi ya jirani zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *internet* bado matumizi ni kidogo sana, hatujaweza kufikia kiwango ambacho maazimio mengi tu mara ya mwisho walifanya kikao hapo Rwanda wakaazimia, sidhani kama hata *MDGs* tutafikia kwenye upande wa *telecom*. Nina hakika kwamba, tuna njia ndefu ya kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, upande wa *Commission* ya Sayansi wanafanya kazi nzuri lakini pia kama tunavyoona kwenye bajeti, fedha hazitoshi. Ningependa sana wawe wana-*publish research proposals* na *research outcomes at least* kila miezi sita, maana kuna *research* nyingi sana zina-*take place* katika nchi hii, lakini hatujui na usipojua ina maana hatuko *informed* na tunakuwa hatuna manufaa licha ya kwamba, kuna watu wanatoka nje kufanya utafiti na wanapopata matokeo yake hatuyajui. Kwa hiyo, nina hakika wangkuwa na fedha nyingi, wangeweza ku-*publish proposal* na *findings* za *research*. Hilo linaweza kuthibitishwa, mpaka sasa hivi ukiangalia idadi ya *local patents* ambayo inafanywa na Watanzania, *almost* hakuna. Ina maana bado hatujawa na *scientists*, wavumbuzi na kadhalika. Inatokana na nini? Inatokana na bajeti kama mlivyoona ni *less than 0.01* ya *GDP so far*.

Kwa hiyo, inatuonyesha kwamba, bado sisi hatuwezi kuringa. Tungekuwa na uwezo huo, tungekuwa tunapata fedha nyingi sana hata kwa kuuza *royalty* tungepata *license fees* na kadhalika. Kwa vile hatuna uvumbuzi ambao unaweza kusemwa kwamba ni kazi ya Watanzania, tunakuwa nyuma kwa kila sekta kwa upande wa Sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nalipongeza sana Shirika la Posta Tanzania, wamejitahidi sana, kwa sababu wana mambo mengi ambayo yanawakwaza, kwa mfano, nyumba zetu nyingi hazina *physical address*. Nina hakika kama tungekuwa na *physical address*, nyumba namba saba mtaa huu, lakini unakuta mitaa inaingiliana Dar es Salaam unakuta mitaa hiyo hiyo ipo Morogoro na kadhalika. Nadhani bado pale tuna kazi, nina hakika kwamba wangeweza kufikia kupeleka hata barua nyumbani, lakini sasa hivi ni vigumu. Huwa naona hata *Kurya Company* zinapata tabu sana wakati mwingine *ku-deliver mails*. Wana ushindani mkubwa *Kurya Company* zimekuja juu, nina hakika na wao walijitahidi, kuna kuna *EMS* na nyingine lakini wanahitaji jitihada zaidi ili kushindana.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilipenda Mheshimiwa Waziri anieleze hasa upande wa Sayansi, kuna *mechanism* gani ambayo imewekwa? Kwa kawaida *basic science*

inafanywa na *universities*, lakini haya mambo ya teknolojia ambayo ni *applied research* na kadhalika, pamoja na *industry*, yanatakiwa yote yawe yanaunganishwa; kwamba, wanapofanywa *research* halafu wana-develop a product, hiyo *product* iwe *commercialized*. Sasa sielewi sera yetu ikoje; hawa wanafanya utafiti wakimaliza wana-file papers pale mambo yamekwisha. Wametumia fedha nyingi sana kwenye utafiti, lakini unakuwa hauna manufaa kwa uchumi wa Taifa. Ningependa njue sera yetu *so far* ikoje kwenye suala kama hilo?

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naelewa biashara ya *Cellular* ni ya *private including TTCL* wanafanya kwa kujitegemea; wana bodi yao na kadhalika. Ningeomba tu kwenye jimbo langu, waonyeshe *coverage* hasa upande wa Kaskazini zaidi, mbele ya *Airport* bado *coverage* ya simu za mkononi siyo nzuri.

**NAIBU SPIKA:** Jimbo lenyewe wala hatulijui.

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Jimbo la Ilemela.

**NAIBU SPIKA:** Wapi huko?

**MHE. ANTHONY M. DIALLO:** Mwanza, *Tanzania, East Africa. (Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nadhani niishie hapo, mambo ni mengi muda hautoshi. Napenda nirudie kwa kuwapongeza sana Wizara.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kusema naunga mkono hoja. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana nashukuru kwa mchango wako mzuri.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na mimi nichangie hoja iliyopo mbele yetu. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Viongozi wote wa Wizara, kwa kazi nzuri waliyoifanya ikizingatiwa kwamba, hii ni Wizara mpya. Ninayo machache, baada ya kutoa pongezi na mimi niweze kuyachangia katika Sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mawasiliano ya simu ni muhimu kama ilivyo reli, barabara na bandari. Kwa hiyo, mawasiliano ya simu ni nyenzo muhimu sana kwa maendeleo ya nchi. Nilipokuwa naangalia hali halisi ya mawasiliano ya simu Tanzania, ukienda kwenye historia, mimi ninajaribu kuangalia katika upande wa kodi zinazotozwa kwenye simu Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2002 kwenye mambo ya simu walikuwa wanatoza *corporate tax*, kodi ya mapato, *local authority levy*, *VAT* na *Excise Duty*, ambayo ilikuwa *five percent*. Wakati *excise duty* imeanzishwa on *airtime*, ambayo ilikuwa ni *five percent*, *TCRA* ambao walikuwa wanafanya kazi nzuri sana, wao walikuwa wanatoza mrabaha wa asilimia tano. Baada ya Serikali kuanzisha *excise duty*,

*TCRA* wakashusha ile *amount* ya mrabaha kuwa 0.08, ambapo kwa kweli walishusha kwa kiwango kikubwa sana, kwa sababu *TCRA* ni muhimu sana ili *industry* hii iweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, upo utafiti ambao umefanyika ambao ni muhimu sana, tunapokuwa tunataka kutoza kodi kwenye hii Sekta ili iweze kukua; kuna mambo ya msingi lazima tuyazingatie. Utafiti uliofanyika, leo tukiamua kupunguza ama kuongeza huduma za utumiaji wa simu, zikiongezeka kwa asilimia kumi na Pato la Taifa nalo litaongezeka kuwa *1.2 percent* ya *GDP*.

Kwa hiyo, unapokuwa na watumiaji wengi wa simu vilevile na Pato la Taifa nalo linakua. Kwa hiyo, ni muhimu sana tunapokuwa tunaweka kodi kwenye sekta hii, tuangalie hayo mambo katika ujumla wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2006, Sekta hii ya Simu ilichangia asilimia tano ya *GDP* ya nchi ya Kenya ambacho ni kiasi kikubwa sana na ilitoa ajira karibu 200,000. Sekta hiyo ndogo sana ya simu na ndiyo ilikuwa inaanza. Kwa hiyo, unaweza ukaona sekta hii ni ya msingi sana katika maendeleo ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini yapo mambo ambayo tungependa tujaribu kushauriana vizuri ili tuweze kuyaweka vizuri. Tatizo kubwa la Afrika katika simu hasa hizi za mikononi ni kodi; kodi ni kubwa sana. Kodi ikishakuwa kubwa, maana yake unawafanya watu wengi wasitumie huduma hiyo na watu wengi wasipotumia huduma hiyo, maana yake mwisho wa siku na wewe kama Serikali, unapoteza kiwango kikubwa sana cha fedha na baadaye nitasema kwa kila unapoongeza ama ukipunguza Serikali ita-*benefit* namna gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, juzi Waziri wa Fedha ameongeza *excise duty on airtime* imefika asilimia kumi kutoka asilimia saba. Hiki ni kiwango kikubwa sana na tuisisahau katika *study* hii iliyofanyika Tanzania, sisi ni wa pili kwa kodi kubwa kwenye simu duniani baada ya Uturuki. Kwa hiyo, unaweza kuona tuisipokuwa waangalifu, hii Sekta haitakua lakini kwa sababu tunadhani nia ni kutafuta kodi, kumbe tungeweza kuiacha tukapanua wigo wa kodi kwa kuiacha kodi iweze kulipika na kwa sababu hiyo watu wengi sana wanaweza kushiriki kwenye kukuza sekta hii. (*Makofî*)

Mheshimiwa Naibu Spika, zipo hizo kodi kwenye *handset*; *handset* hizi kama hujaweka *line*, basically hili halina maana ni chombo kimekaa tu. Tumeweka kodi kubwa kumbe tungeweza kuiondoa hapo ili watu wengi waweze ku-access hizo *handset*. Kwa sababu *handset* hazina maana mpaka pale tu ambapo umeweke *line* ya simu. Kwa hiyo, nadhani mambo hayo wenzetu waweze kuyafikiria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia upo ushahidi kwamba, iwapo tutapunguza gharama za *VAT*, kuna mambo fulani karibu manne yatatokea kwenye sekta hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Afrika Mashariki kodi zinazotozwa ni mara mbili ya wastani wa kodi zozote duniani; *about 17.4%* kwa sababu ya *VAT*. Tukipunguza kodi ya *VAT*, tutachochea watu wengi kuwa na simu za mkononi na matumizi yatakuwa makubwa sana na kwa sababu hiyo, uchumi wa nchi utakua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia ukiangalia kodi inayotozwa kwenye *handset* ni karibu asilimia 24.8 kwa gharama hiyo ambayo ni kubwa sana na hii kwa kweli inafanya *industry* hii isiweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema, sisi ni wa pili duniani kwa kuwa na kodi baada ya Uturuki ambayo ni asilimia 45 na sisi asilimia 30 ipo kwenye gharama za simu. Maana yake ni kwamba, ukinunua *air-time* ya shilingi 10,000, shilingi 3,000 zote ni kodi. Hii kodi ni kubwa sana, kama tunataka sekta hii iweze kukua lazima wenzetu wafikirie namna ya kufanya. Kwa hiyo, nilitaka kulisema hili ni jambo la msingi sana ili tuweze kwenda mbele. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nilisema kwamba, utafiti unaonyesha tukipunguza kodi ya maongezi ya vifaa vyta simu kwa asilimia tano tu, tupunguze toka ilivyo sasa ndani ya miaka kumi, matumizi yataongezeka kwa asilimia saba, mtandao utapanuka kwa asilimia tano, pato la watu wanaota huduma hizo litaongezeka kwa asilimia nane, ajira itaongezeka, lakini pia kodi ya nchi itaongezeka kwa asilimia nne ambapo hii ni kubwa sana. Lazima tuwaombe wenzetu wa Wizara ya Fedha na Uchumi na Wizara hii, waweze kufikiria namna ya *ku-scrutinize* hili suala la kodi ni la msingi sana ili Sekta hii iweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia suala ambalo bahati nzuri Waziri amelisema leo asubuhi ni suala la simu kadi. Tanzania unakwenda hapo nje unanunua simu kadi unavyotaka, duniani haiko hivyo hata kidogo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, Mwezi Aprili, 2008, nilikwenda India, nikawa natafuta simu kadi ninunue, nikaambiwa lazima nitoe *photocopy* ya *passport*, nitoe *photocopy* ya *ticket* yangu, nikasema yote ya nini? Akasema hapa huwezi kupata simu kadi ni tofauti na Tanzania, matokeo yake ni nini? Kwa sababu sisi simu kadi zinaokotwa, mtu ananunua simu kadi kwa shilingi 500 ama zinatolewa bure, ndiyo maana leo kuna simu kadi nyingi sana zinatukana watu, zinatumika kwenye ujambazi, lazima hili tulifanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi ningeomba sana wenzetu wa *TCRA* pamoja na Wizara, walete sheria au *regulation* ibadilishwe, simu kadi zote ziwe *registered*, lakini pia bei ya simu kadi iwe kubwa ili mtu asiweze kununua leo na kesho akaitupa kwa ajili ya kumtukana mtu mmoja. Hili ni jambo la hatari sana, lakini yote ni kwa sababu tumeacha kila kitu kipo wazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia tukiweka bei kwenye *handset*, Serikali itapata mapato. Ninawaombeni sana kwenye hili la simu kadi, tuzisajili lakini tuziwekee bei ili kuondoa hao watu amba wanakuja, anafika leo tu ndiyo zinatumika kwenye mtandao wa kufanya vitu viovu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sana watu wa Kampuni ya Simu watusaidie. Gharama zote za simu kwa maana unaanzia gharama, faida, mpaka kodi,

ziwe wazi ziweze kujulikana. Kwa sababu ipo *myth* inaanza kutembea unadhani labda hawa gharama zao hazijulikani, wanapata faida kubwa; ni vizuri waweze kuzitangaza ili ziweze kufahamika tujue kama ni kweli tunapata kiasi gani.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la *post code*; bahati nzuri Waziri amelisema, tumeanza Arusha kwa ajili ya *post code*. *Post code* ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu, ningeomba Mradi huu wa *post code* uunganishwe na Mradi wa Vitambulisho vya Uraia, kwa sababu vitambulisho vya uraia unampaje mtu ambaye hujaweza kum-*identify* yuko wapi, anatoka wapi? Ni msingi sana *project* hii ioanishwe na hii ya vitambulisho vya uraia. Ukweli *post code* itasaidia siyo tu kumletea barua nyumbani, itasaidia kwenye mambo ya benki na kwenye mambo ya kulipa *utilities* yote. Ukishakuwa na *post code* inakuwa ni rahisi sana. Hata kama nchi yetu bado mitaa siyo mizuri, lakini bado ipo teknolojia tunayoweza kuwa-*identify* watu wetu wanakaa wapi, wanatoka wapi; ni rahisi na itatusaidia hata kwenye vita yetu ya kupambana na uharamia. Ni msingi sana *project* hii niombe kwa kweli iunganishwe na hiyo ya kwetu ya vitambulisho vya uraia.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini jambo lingine ni *ICT backbone*; tumechelewa sana. Naomba jambo la *ICT backbone* wenzetu wanakwenda mbele. Kwa kweli suala la *ICT* ni muhimu sana. Leo *ICT* ikija utapunguza gharama za Serikali kwa kiasi kikubwa sana, utakapoifanya kuwa na hii *government*, gharama za uendeshaji wa Serikali zitapungua, zitatusaidia kwenye shule zetu na kwenye hospitali. Jambo hili ni muhimu sana liwekewe kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho nilitaka niongelee habari ya sayansi na teknoloji. Unaangalia bajeti iliyowekwa kwa ajili ya sayansi na teknolojia unaogopa. Mimi nitaomba kwanza, kabla sijalijadili jambo hili, nim-*quote* mwanasayansi mmoja ambaye kulikuwa kuna mkutano kule Jamaica tarehe 4 Novemba, 2005 aliongelea umuhimu wa sayansi na teknolojia. Nitaomba nim-*quote* kwa Kiingereza anasema: “*Within the context of globalization, the country’s ability to achieve and maintain a high standard of living, would depend on the extent to which it could harness the science and technology.*” Akaenda mbali zaidi, anasema: “*To enhance the international competitiveness of the country, it is therefore critical for us to promote science and technology in the education system, this will ensure the economy of the country remained competitive.*”

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nchi hii hatuji-*address* vizuri kwenye sayansi na teknolojia hatuwezi kuendelea. Ukiangalia China kwa nini imeendelea; ni kwa sababu ya sayansi na teknolojia. Ukishakuwa na sayansi na teknolojia, una uhakika utapata watu wako (*human capital*), ambayo ni *quality* inaweza ika-*compete*. Nilikuwa nasikia habari ya kuanzisha viwanda Tanzania, lakini kwa hali ilivyo sasa, hata ukijenga kiwanda *Tanzania; unity cost* ya *labour* in China ni *cheaper* kuliko kiwanda tutakachokijenga Tanzania, lakini kule unapata *labour* ambayo ni *skilled labour*. Kwa hiyo, lazima turudi tujipange upya kwamba, lazima tuhangaike na suala la sayansi na teknolojia. Ukiangalia kwenye kitabu chenye fedha hapa; sayansi na teknolojia imepewa fedha kidogo sana; unajiuliza hivi tunataka kwenda wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia, angalia nchi zote zilizoendelea na lazima tuanze kufikiria hivi kwa mwaka tunawapeleka watoto wetu wangapi kwenda kujifunza duniani, kwa wale ambao teknolojia yao ipo mbali zaidi ili warudi *multiply effect* iwe kubwa kwa watu wetu. Mimi naona hatujafanya *much* kwenye sayansi na teknolojia na hatujafanya *much* kwa sababu tumeweka fedha kidogo sana. Kwa kweli bila sayansi na teknolojia, hatuwezi kutoka na wengine wanassema *in fact* mwaka huu kwenye Uchaguzi wa Marekani, wanassema walete mdahalo kuangalia wale wanaogombea Urais, wanaelewaje kuhusu *importance* ya science education. Research na innovation ni msingi sana kwao, unaweza ukaona nchi zilizoendelea zina-invest kwenye mambo ya sayansi na teknolojia.

Ukiangalia vitabu vyetu vya bajeti, unaona kweli bado tunalo tatizo kwenye Sayansi na teknolojia. Viwanda tunavyoviongelea vitakuaje bila kuwa na sayansi na teknolojia? Kwa hiyo, naomba wenzetu tuwasaidie na mimi naamini, Mheshimiwa Profesa Msolla, ana uwezo mkubwa hili anaweza kulifanya, lakini bila kumpa *resources* hawezu kufanya lolote. Bila kumpa *resources* tutakuwa tunassema tu na ukisoma Sera yetu ya Sayansi na Teknolojia, unajiuliza tuna tatizo wapi? Sera yetu ni nzuri sana na mwelekeo upo. Tunayo *Vision 2025* tunassema, by 2025 Tanzania itakuwa *semi industrial country*, yenyе uchumi wa kati duniani; maana yake ni nini?

Maana yake lazima sayansi, teknolojia na *innovation* iendane na hiyo. Ukijiuliza leo tumebakiza miaka mingapi kufika 2025? *Can we really say* tutaweza kufika tunakotaka kwenda? Tunaweza tukawa *competitive* kwenye sayansi na teknolojia, hatuwezi kwenda bila *kufanya research, how much we are putting on a research*; lakini pia watu wakishafanya *research* tunafanya nini kutumia hiso *research*, maana tuna *research* nydingi sana hatuzitekelezi? Ni muhimu sana tuweze kujitahidi katika sayansi na teknolojia ili tuweze kuondoka hapa tulipo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nawashukuru sana na nawapongeza tena. Suala la kodi kwenye simu ni la msingi sana, kwa sababu kodi ni kubwa sana na matokeo yake *industry* hii ya simu haitakua. Watusaidie wenzetu ili *industry* hii iweze kukua.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuunga mkono hoja hii.

**MHE. PINDI H. CHANA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia. Nianze kwa kuipongeza Wizara kwa shughuli ambazo Wizara imekuwa ikizifanya katika nchi yetu; imejitahidi sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kujitahidi huko, bado zipo changamoto kadhaa ambazo naomba nitumie nafasi hii kuishauri Serikali kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tunaposema mawasiliano, ninavyofahamu mimi, mawasiliano yanasaidia kuokoa muda na katika lugha ya wenzetu Waingereza wanasema kwamba, muda ni fedha (*time is money*). Katika nchi yetu, suala la mawasiliano ni jambo ambalo ni muhimu sana kulitilia maanani.

Wenzetu wanasema kwamba, sasa hivi ni *error of global economy* na *error* hiyo ndiyo hiyo ambayo inatumia vitendea kazi mbalimbali vya mawasiliano ya kisayansi na teknolojia, ambavyo vikiwepo basi uzalishaji wa maeneo mengine ya kiuchumi yanaenda vizuri, kwa haraka na kwa wakati unaofaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na shughuli nzuri ambazo Wizara imekuwa ikizifanya, bado katika nchi yetu suala la sayansi na teknolojia liko nyuma. Ningombwa kushauri kama ifuatavyo:-

Nilidhani jambo hili, vijana wetu ambao wako mashulenii na vyuo vikuu, waanze kufundishwa kama somo katika mitaala. Mambo ya sayansi na teknolojia hata kama hakuna vitendea kazi, hakuna umeme wala kompyuta, lakini katika *theory* tukianza kuwafundisha watoto wetu leo itatusaidia sana. Mtoto anamaliza *Form Four*, anamaliza *A level* hata *idea* ya kompyuta. Inabidi aanze upya kwenda kwenye kozi!

Mheshimiwa Naibu Spika, hata tunaposema ajira hazipatikani, ajira nyingi za wawekezaji wanaweka kwenye *internet*. Lazima mtu awe na uwezo wa ku-access, kuangalia anaweka *CV* yake mahali pale, akishaweka wakati mwengine hata yeye anatafutwa hata kama hajaenda ku-*apply* kwa ajili ya kazi. Kwa hiyo, suala la mawasiliano, sayansi na teknolojia, hasa kwa wakati huu ni jambo muhimu sana. Wanasema wenzetu ni wakati wa utandawazi, dunia kuwa kijiji. Kwa hiyo, ningombwa sana, jambo hili Wizara ya Elimu ilifikirie ikishirikiana na Wizara ya Mawasiliano, liwe ni somo.

Watoto wa wenzetu wa nchi jirani na nchi zilizoendelea, wakiwa bado katika elimu ya *Primary*, wanaweza kabisa kutumia kompyuta. Masomo mengine, mambo mbalimbali na utafiti unapatikana mle, anakuwa na uelewa mkubwa zaidi. Maana yake mashindano yanazidi kwenda. Vile vile ipo haja ya kuboresha huduma hizi za mawasiliano katika sekta mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa taaluma yangu ya Sheria, nimekuwa ni shahidi wa haki za binadamu maeneo mbalimbali, zinavyoweza kupotea au wakati mwengine kuchelewa kutekelezwa na hii ni kutokana na mawasiliano. Mawasiliano katika nchi yetu, yamekuwa ni gharama sana. Iwe ni simu na hata ikiwa ni kusafiri *physically*, mawasiliano yamekuwa ni gharama sana. Kwa mfano, mtu ame-*retire* anadai haki zake, wanasema *terminal benefits* anaambiya lete faili, wakati mwengine mwananchi huyu yupo kule Kijijini Ludewa, anatakiwa alichukue faili kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa alipeleke Mkoani. Akifika Mkoani anaambiya sasa faili hili linatakiwa liende Hazina wakafanye *calculation* waone kazi ulianza lini, umemaliza lini, ili kuweza kuandaa haki zako. Unashuhudia mtu katika harakati za mawasiliano, akifika

Dar es Salaam anaambiwa sasa kuna barua moja kwa Mkurugenzi ukaichukue; unatakiwa kurudi Ludewa.

Usafiri atakaotumia iwe ni kwa *bus* au kwa njia yoyote ni gharama sana. Kwa hiyo, jambo hili ni lazima tulitafakari sana, mawasiliano yamekuwa ni gharama sana. Kwa kuwa mawasiliano yamekuwa ni gharama, basi haki inakuwa ni vigumu sana kutendeka kwa wakati unaofaa. Nilidhani, Serikali ijaribu kuangalia maeneo mengine ya sekta binafsi. Sekta binafsi kwa mfano, Mashirika ya Umma, *let say* benki; leo hii mtu anaweza akafungua akaunti Iringa, akiwa Shinyanga anaweza kuulizia *balance* ya kwenye akaunti yake; *in few minutes* wanamwambia *balance* yako ni hii; ulichukua hela jana ukiwa Dodoma, ulichukuwa hela juzi ukiwa Dar es Salaam. Haya yote ni masuala ya *IT*; sasa iweje sisi tushindwe kufanya hivyo upande wa Serikali? Mtu anapokuwa ameajiriwa, tufahamu basi kuwepo kwa utaratibu ambao ni *computerized*. Huyu mtu mafao yake kila mwaka amekatwa kiasi fulani, mapato yake yamekwenda katika ile mifuko ya hifadhi na sasa hivi anadai kiasi fulani.

Sasa mwananchi kwa mfano ame-*retire* hana mafungu, hana mshahara, anapataje *terminal benefits* kwa kusafiri? Bado hiyo imekuwa ni changamoto kubwa sana katika nchi yetu. Wakati umefika sasa wa mambo mengi ya kiserikali siyo sisi tuanze kuinua mafaili, uchukue upeleke kwa Mkuu wa Mkoa. Mkuu wa Mkoa sasa liende Hazina, lirudishwe. Aaah sasa tujaribu kutafakari ili mambo hayo yafanyike kwa haraka na haki iweze kutendeka na uchumi utaenda kwa haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa ufahamu wangu mdogo, ninajua mawasiliano si biashara ni huduma. *Communication is not a profit making business, it is a service.* Kwa hiyo, *the cheaper the service, production* inakuwa kubwa. Kwa hiyo, wakati umefika wa Serikali *ku-regulate*. Tusiyaachie mashirika binafsi yakajipangia viwango wanavyovijua wao. Endapo mawasiliano yatakuwa na bei ya chini, Serikali itakapoweka *limitation* kwamba, iwe ni viwango vya simu au viwango vya nauli, ukilinganisha nauli sasa hivi za mabasi na kima cha chini cha Serikali, utakuta mtu ana watoto watatu, wote asubuhi wanakwenda shule. Nauli za mabasi wanafunzi ni Sh. 200 *go and return*. Yeye mwenyewe anaunganisha mabasi mawili, mawasiliano yamekuwa ni gharama. Kwa hiyo, ipo haja ya kulitafakari; iwe ni *SUMATRA* au vyombo vyetu mbalimbali vinavyohusika na masuala ya mawasiliano, kwa kweli wakati umefika sasa wa kuhakikisha kwamba, gharama hizi za mawasiliano zinapungua sana. Wawekezaji wengi wamejitahidi sana kuwekeza katika sekta mbalimbali hasa zile za simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli wanapata mafungu mengi sana na tunawashukuru kwa sababu kwa upande mmoja au mwingine, pamoja na huduma hiyo ya kuwekeza katika mawasiliano ya simu, kwa mfano, *mobile telephones* pia wanajitahidi sana kuchangia mashule, huduma za afya na kadhalika. Tunaomba waendelee na moyo huo. Nawashukuru pia Shirika la Vodacom, ambalo sasa hivi linajenga *Ward* ya *Maternity* Wilaya ya Ludewa. Wanafanya vizuri, lakini basi vile vitendea kazi vyao ambavyo wamekuwa wakinunua nje ya nchi, tujaribu kutafakari tupate viwanda viwepo nchini mwetu ili ipatikane ajira na mambo mengine kama hayo, badala ya kuagiza kutoka nchi za nje.

Kwa kuwa mashirika haya ni makubwa, yapo mengi na kuna soko la vitendea kazi nya aina hiyo; ikiwezekana nashauri kiwanda kiwepo nchini, kwani sasa ni wakati wa kuanzisha vitega uchumi nya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyokwisha kusema kwamba, wakati umefika sasa utafiti uliokuwa umefanyika hivi karibuni, yupo mtafiti mmoja aliwahi kusema kwamba, kutokana na uhaba wa mawasiliano; kusipokuwa na mawasiliano ya kompyuta, yakifanyika *manually*, mtu kusafiri na kadhalika, katika *transaction* moja wakati mwingine anahitaji siku zisizopungua 48, anahitaji sahihi zisizopungua 25 kutokana na ule urasimu kutoka hapa chukua faili nenda hapa, njoo keshokutwa; kesho Ijumaa, Jumamosi, Jumapili, hatufanyi kazi inabidi usubiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba sana Wizara itafakiri hilo. Ombi langu lingine ni kwamba, masuala haya ya sayansi na teknolojia, sasa yawekwe katika mitaala ya shule zetu; iwe ni shule za msingi, sekondari au vyuo vikuu hata kwa kuanzia kwa *theory* na baadaye kadiri siku zinavyokwenda, watafanya *practical*. Baada ya mchango huo, nitakuwa tayari kuunga mkono hoja endapo ushauri wangu utazingatiwa. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Kutoa shilingi kwa sababu ya mtandao siyo *efficient enough!*

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatambue wageni ambao wapo hapa; wengine tuliwatambulisha asubuhi kumbe hawakuwepo. Tunao wageni 126 wa Mheshimiwa George Lubeleje, ambao ni wanafunzi 120 na walimu kumi kutoka Shule ya Msingi Mtegeta; naomba wasimame walimu na wanafunzi kutoka Mtegeta.

(*Hapa wageni waliotajwa walismama*)

**NAIBU SPIKA:** Ooooh! Karibuni sana, asubuhi tuliwa-*miss*, nasikia mlikuwa mmepeata matatizo ya usafiri. Pia kuna wageni kutoka Shule ya Msingi Chazungwa, ndiyo hao? Chazungwa wapo? Haya ahsante. Ahsante sana walimu na watoto. (*Makofi*)

Halafu tuna Mawakili 30 kutoka *Tanganyika Law Society*, ambao wamekuja kutembelea Bunge, baada ya kumaliza Mkutano wao wa Robo Mwaka uliofanyika katika Ukumbi wa Mtakatifu Gasper; naomba wasimame kama wapo.

(*Hapa wageni waliotajwa walismama*)

**NAIBU SPIKA:** Oooh! Ahsanteni sana. Nadhani mmekuja wakati mzuri, karibu sana. Ahsante sana. (*Makofi*)

Halafu tuna Wanakwaya 40 wa Mtakatifu Maria kutoka Parokia ya Kiwanja cha Ndege, huko ninakosali mimi. Wasimame walipo.

(*Hapa wageni waliotajwa walismama*)

**NAIBU SPIKA:** Kumbe na wao wapo hapa hapa; karibuni sana. Nawashukuru nyote na karibuni sana.

Tunaendelea na Mheshimiwa Lwanji, halafu Mheshimiwa Lodovick Mwananzila ajiandae na Mheshimiwa Profesa Idris Mtulia ajiandae.

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia hoja ya Wizara hii ya Mawasiliiano, Sayansi na Teknolojia. Ninaunga mkono hoja na nichukue nafasi hii pia kuwapongeza Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa ushirikiano wanaotupa. Kila mara tunapowagongea milango na kuwapigia simu kwamba, kuna dosari basi huwa ni wepesi wa kutusikia na kutusaidia. Nawaomba kwamba, moyo huu uweze kuuendeleza.

Mheshimiwa Naibu Spika, jana tulisikia kwamba, kati ya Wabunge kumi ndani ya Bunge hili ni Wabunge wawili tu ambao akisema au akisikika akizungumza, basi anazungumza maneno sahihi (maneno ya kweli).

**NAIBU SPIKA:** Alisemaje mimi sikusikia?

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Nasema jana katika uchangiaji, ndugu yetu mmoja alisema kwamba, ndani ya Bunge hili kati ya Wabunge kumi ni Wabunge wawili tu ambao wakisimama na kuzungumza unawenza kuamini maneno yao. Maana alifikia hatua ya kusema kwamba, kati ya 100 basi ni 20. Sasa kati ya kumi ni wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kusema kwamba, mimi ni mmojawapo ambaye ninasema kweli. Sijafanya *research* ya kujua hilo. Labda nitaamini baadaye kama nikifanya *research*, lakini mimi husimama hapa na kusema kweli daima. Nimewekeza kwa hilo jimboni kwangu. Si mtu ninayeweza kuja kuzungumza uwongo au kuzungumza mambo ambayo hayaaminiki. Kwa hiyo, hilo nilidhani niliweke wazi.

**NAIBU SPIKA:** Zile zilikuwa tuhuma zake tu, maana yake Kanuni yetu inasema; tutasema kweli daima humu ndani. Kwa hiyo, nafikiri alipenda kufurahisha watu tu, lakini hakuna mtu anayeruhusiwa kusema uwongo humu ndani. Kwa hiyo, Mheshimiwa usiwe na shaka, sisi tunaamini wote mnavyosema. (*Makofî*)

**MHE. JOHN P. LWANJI:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Ninaunga mkono mapendekezo ya Kamati ya Miundombinu, kuhusu Shirika la Posta. Shirika la Posta wote tunalifahamu na tarehe 13 Septemba, 2007, Serikali iliamua kuliboresha Shirika hili na kilichokuwa kimebakia ni utekelezaji tu. Sasa ilikuwa iharakishe mchakato wa kuchukua na kufuta madeni ya muda mrefu ya Shirika hili. Sasa sijui kama hatua hizo zipo mbioni au zimechukuliwa? Ni vizuri tukalinusuru Shirika hili na kuliondolea ukata, ili liweze kuboresha sekta hii ya mawasiliiano.

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuna asiyefahamu umuhimu wa Shirika hili, lisiachwe likafa kama mashirika mengine ya umma yalivyokufa. Umuhimu wa Posta unajulikana, bila hivyo basi hakuna mawasiliano ya uhakika na hatuwezi kuachia sekta hii ya mawasiliano mikononi mwa watu binafsi peke yao. Kwa hiyo, ningeliomba hatua hizi ziweze kuchukuliwa. Madeni hayo ilikubali kufuta yanayofikia bilioni 5.2 na dola 490 katika madeni ya *IDA*. Nitapenda kujua kama hatua hiyo imechukuliwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ichukue hatua basi ya kutenga pesa ilizoahidi bilioni 8.2 kwa ajili ya kuwalipa wafanyakazi na wastaifu wa lililokuwa Shirika la Posta, kabla halijatengenishwa kutoka Simu na ile Tume au Mamlaka ya Mawasiliano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeliomba pia ule mtaji iliyoahidi wa shilingi bilioni 24 ziweze kutolewa. Huu mchakato unachukua muda gani? Hii iliazimiwa kihalali kwamba, ili Shirika liweze kutoa huduma chini ya Sheria ya Bunge Namba 19 ya Mwaka 1993 ndivyo ilivyoelekeza hivi. Sheria hii inaitaka Serikali ilipie mtaji, kitu ambacho Serikali haijatekeleza tangu shirika hili lianzishwe Januari, 1994.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali iliahidi wakati huo; *actually*, mtaji siyo 42 bilioni ni 24 bilioni. Sasa iharakishe basi ili shirika hili liweze kupata ahueni lisonge mbele na liweze kuwahudumia. Shirika hili limepanga mambo mengi tu mazuri; limepanga ujenzi wa Posta za kisasa 47, kwa gharama za shilingi bilioni tano; ukarabati wa Ofisi 67 kwa gharama ya shilingi bilioni 1.7; na ununuzi wa vitendea kazi kwa kuzingatia mabadiliko ya teknolojia shilingi bilioni 3.9. Kwa maana kwamba, zinazotakiwa sasa hivi ni shilingi bilioni 10.6 za haraka ili kuweza kuboresha masuala haya muhimu katika shirika hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya kutokamilisha hizo ahadi za Serikali ni kwamba, Shirika hili linashindwa kuhimili ushindani. Shirika haliwezi kusonga mbele bila mitaji hiyo inayotakiwa na inashindwa kuijendesha kibashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, inapofikia wakati mishahara inakuwa kitendawili, wanaanza kuwa na wasiwasi, fedha za wateja unatuma haziwafikii kwa muda badala yake zinaanza kutumiwa na Shirika kwa mambo mengine. Basi shirika hilo lina matatizo na wateja hufikia hatua ya kuweza kupoteza imani.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ninatoa rai kwamba, shirika hili lisaidiwe haraka iwezekanavyo ili liweze kuondokana na matatizo haya. Namshukuru sana Waziri wa Wiizara hii, kwa jinsi alivyotanzua tatizo la Posta ile ya Itigi, tulikuwa hatuna *money fax* iliharibika kwa muda mrefu, lakini tulipomwona tukaletewa *money fax* mpya. Ninawaomba Wananchi wa Jimbo langu na hasa Itigi, Mgandu, wasiende Manyoni mpaka Singida kuhatarisha maisha yao, watumie hiyo *money fax* iliyopo hapo.

Wengi wanasitasita, nadhani wanaogopa lakini inafanya kazi na haipitii tena Manyoni ni *direct line*. Kwa hiyo, ningeliwaomba Wananchi wa Jimbo hili na hasa Itigi, pamoa na Mgandu, waweze kuokoa pesa zao au badala ya kuingia gharama basi waweze kutuma pesa zao kwa *money fax* hiyo, badala ya kwenda Posta ya Manyoni au Singida.

Tunaomba jengo imara hapo, maana jengo la *Railway* lile ni la zamani. Nadhani mtaangalia suala hilo ili tuweze kuondokana na tatizo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, *issue* ya minara nadhani kila mmoja anajua kwamba, sasa sisi Wabunge tuna tabu na hizi simu za mkononi. Kwa sababu sasa hivi inaonekana hata *priority* unapokwenda huko vijiji, watu hawakuulizi sana matatizo ya msingi; kuna suala la maji, zahanati, lakini utaambiwa Mheshimiwa minara itakuja lini? Sasa tuna minara Itigi, Tigo, Celtel na Vodacom, Celtel wakasogea mpaka Mgandu. Kati ya Itigi, Legezamwendo mpaka Lulanga haisikiki, mitandao haipatikani pale. Sasa watu wengi wamenunua simu zao Mgandu, wanafanya biashara, lakini wanasikika pale pale Mgandu, lakini hapa katikati hakuna.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba, unaweza ukafikiri ni *luxury* lakini maeneo haya ndiyo yenye matukio makubwa ya ujambazi. Ujambazi ni mwungi sehemu hizi, kwa hiyo, watu wanaona ili kuwa na uhakika wa usalama ni vyema kuwa na vitu kama hivi. Mabasi mengi yametekwa, tena mwaka jana kuna basi moja lilisimamishwa si mbali sana na Itigi Mjini, lakini kwa kuwa kulikuwa hakuna mtandao pale, basi watu walishushwa, wakavuliwa nguo, wakanyang'anywa kila kitu na mwisho wakaingizwa kwenye basi wakiwa hivyo. Ilichukua operesheni karibu saa nzima. Laiti mtu mmoja angekuwa amewahi kupiga simu mapema, wangekutwa wanafanya operesheni ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeliomba minara ifike Rungwa kwenye hifadhi, wawindaji wanakuja kule pamoja na watalii, sasa wanalazimika kutumia *satellite falls*, kitu ambacho wangeweza kutumia hizi simu za kawaida za mkononi. Simu za mkononi zinapata faida kubwa sana, haya makampuni, lakini katika sehemu ambazo minara imepita hakuna faida kubwa wanayoiacha pale. Sasa wasaidie kuchangia maendeleo ya wananchi pale basi. Ingelikuwa ni vyema wachangie, kwa mfano, kama Vijiji vya Njilii pale na pale Kamenyanga, wameshusha mpaka *transforma*; sasa kwa nini wasichangie pale kuwapa umeme; umeme unapita juu yao tu?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani nitamwona Mheshimiwa Waziri kuhusu hilo ili tuweze kusaidiana, tusonge mbele kimaendeleo. Bara letu lipo nyuma kisayansi na hii inaelewka kabisa, hata mwanaharakati mmoja amesema Bara letu limebakia kuwa la mwisho duniani kimaendeleo na kadiri wenzetu wanavyozidi kumiliki sayari za angani, ndivyo sisi tunavyozidi kuamini kwamba, tunaweza kusafiri kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza kwa ungo na kwamba, viungo vya mwili wa albino vitatuletea utajiri. Sasa vitu hivi ni kweli, lakini hata huyu anayesafiri kwa ungo labda pengine angependa kumpigia mwenzake simu kwamba ninakuja huko. Ninachosema ni kwamba, *priority* ni ipi maana tumepitwa na wakati? Wenzetu wanakwenda kwenye sayari sisi hata maji huku hatuna. Unakwenda vijijini, unadaiwa simu za mkononi, sasa hivi ukimpelekea mwananchi wako simu ya mkononi ya twanga pepeta atakurudishia. Atasema siitaki, anataka simu ya uhakika, lakini maji hana na shule hazipo. Utamwona kana kwamba, anataka anasa ambazo haziwezi kuziendesha, lakini ukweli wenyewe ni kwamba, anataka kwenda na wakati. Tumeachwa nyuma, hili Bara tuko nyuma, lakini watu wanataka kusonga mbele.

Kwa hiyo, *point* yangu ni kwamba, Serikali iharakishe kuleta maendeleo kwa watu. Sisi sasa hivi tumekuwa ni tatizo hilo. Unapokwenda pale mwananchi atakuambia

anataka simu, kila mtu atakwambia anataka simu. Sasa ukimwambia kwamba, bwana mimi ninashughulika kwanza na masuala ya maji au nashughulikia masuala ya barabara au ya zahanati; anasema kwanza nataka nipate simu. Nadhani kama kuna uwezekano basi tupate ufumbuzi wa suala hilo ili tuweze kukidhi haja zao twende na wakati. Tutaendelea kuwa nyuma mpaka lini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani hii Wizara itatusaidia na mimi nimeona nia ya hii Wizara si mbaya na viongozi wake wamejipanga kuweza kutusaidia na kuweza kwenda na wakati. Ninasisitiza kwamba, *priority* ya minara sasa hivi isiishie tu mijini. Makampuni haya ya simu yaagizwe na ikiwezekana yashauriwe yaweze kuwekeza zaidi vijijini na yasadie kuleta maendeleo. Wanafanya sherehe kubwa sana huko mijini na mashindano, pesa zinazotumika katika mashindano na katika simu zao hizo ni nyingi sana lakini wananchi ambako minara inapita hawana maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana kwa mchango wako. Sasa nimwite Mheshimiwa Mwananzila na Mheshimiwa Profesa Mtulia ajiandae.

**MHE. LUDOVICK J. MWANANZILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii pamoja na hotuba iliyotolewa na Waziri, nawapongeza sana Mheshimiwa Prof. Msolla, pamoja na Mheshimiwa Dr. Maua Daftari na Viongozi mbalimbali, Katibu Mkuu na Wataalam wanaotoka katika Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ni ya msingi sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Wizara hii ndiyo msingi wa mwelekeo wa nchi yetu ya Tanzania. Katika ulimwengu wa kisasa, bila Wizara hii kwa kweli hatuwezi kuingia vizuri katika ulimwengu wa sayansi na teknolojia. Kwa sababu Wizara hii ukiangalia Taasisi zilizoko chini yake, Taasisi za Mionzi ya Atomiki, Taasisi ya Uchunguzi na Utafiti wa Sayansi, Utafiti wa Elimu mbalimbali na Taasisi nyingine zote, ndizo kiini cha maendeleo ya nchi yetu kwa sababu tafiti zitakazofanywa katika taasisi hizi, zikiweza kuwekwa katika vitendo ndiyo zitaweza kuleta maendeleo makubwa ya nchi yetu. Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia, ndiyo inayotuwezesha sisi kuishi vizuri na majirani zetu na hata nchi za ng'ambo za Ulaya, Marekani na Asia ili tuweze kufanya shughuli za biashara, shughuli za kiserikali, taasisi na mambo ya aina hiyo. Hii ni Wizara muhimu sana, lazima Serikali iangalie jinsi gani itaweza kuipatia fedha za kutosha ili iweze kutufikisha 2025 katika mazingira ambayo yamo katika malengo ya Wizara hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara hii ukiangalia taasisi zake ni Wizara itakayosaidia nchi yetu kuingia katika maendeleo ya viwanda, kilimo, uvumbuzi na mawasiliano ya aina mbalimbali hapa nchini. Mawasiliano ya redio, mawasiliano ya televisheni na mawasiliano ya mitando mbalimbali ambayo yamo katika nchi yetu.

Tunaiomba Serikali iipatie Wizara hii fedha za kutosha; miaka inayokuja, ipewe kipaumbele ili iweze kuwekeza fedha nyingi tuweze kupata maendeleo tunayoyahitaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie kuhusu mkongo wa taifa. Gharama za mawasiliano ya simu za mkononi, ni kubwa sana ukilinganisha na nchi za ulaya. Sababu kubwa ni kwamba, mawasiliano ni lazima yapitie katika setelaiti na mawasiliano haya yakipitia katika setelaiti ni lazima ulipie gharama kubwa sana kwa wale waliorusha vyombo hivyo na kuviweka huko angani. Hata televisheni zinazorusha matangazo yake kwa kupitia setelaiti, wanalipia gharama kubwa sana. Tukiwa na mkongo wetu unaopita katika bahari na katika nchi yetu ya Tanzania, tunaweza kupunguza gharama ya mawasiliano katika nchi yetu ya Tanzania kama si kwa robo hata kwa nusu. Hivyo, mtandao huu ni muhimu sana. Lazima Wizara hii ihakikishe kwamba, mtandao huu wa mkongo wa taifa unajengwa ili tuweze kuunganishwa na nchi nyingine tupunguze gharama ya mawasiliano.

Wabunge wengi waliosimama hapa, wameelezea kuhusu gharama za mawasiliano vijijini, mawasiliano mijini na mawasiliano ya nchi jirani na nchi za ng'ambo. Yote haya yanatokana na teknolojia tunayoitumia sasa; tunatumia teknolojia ya kisasa ambayo ni gharama kubwa sana kwa wananchi wa kawaida. Hivyo, tukienda katika mtandao huu unaotumia mkongo, tutapunguza gharama kwa sehemu kubwa sana, lakini papo hapo Serikali iangalie jinsi ya kujadiliana na taasisi hizi au mashirika haya ya mitandao kama Celtel au Zain, Vodacom, Zantel na mitandao mingine ili waweze kuona ni jinsi gani watakavyoweza kupunguza gharama za matumizi ya simu za mkononi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwapongeze sana Kampuni ya Zain au Celtel kwa jinsi ambavyo wameeneza mtandao katika Jimbo langu la Kalambo. Walijenga mwanzo mnara katika Kijiji cha Kipapa na ukawa ndio mwanzo wa kusambaza mtandao wa simu katika Jimbo langu la Kalambo. Wamejenga minara katika vijiji mbalimbali na katika Kata zangu mbalimbali; mfano, Matai wamejenga mnara, Mwazye wamejenga mnara, Mkowe, Kasanga, Kisumba na Ulumi. Minara hii imeweza kuwafikia wananchi zaidi ya  $\frac{3}{4}$  katika jimbo langu. Wamefanya hivyo katika mkoa wote wa Rukwa, pia katika Halmashauri ya Sumbawanga, Bonde la Rukwa na katika Wilaya ya Nkasi na Mpanda. Tunawashukuru sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini katika Jimbo langu la Kalambo, zipo Kata zangu mbili hazipati mtandao wa *Celtel*; Kata ya Mambwenkoswe, Kalembe na Kata ya Sopa na Katete. Eneo hili ni la milima ndio maana sio rahisi watu wote wakaweza kupata mtandao. Nimeshazungumza mara nyingi na Naibu Waziri, nikamweleza kuhusu suala hili, nimezungumza na wataalam wa *Celtel* nikawaandikia barua wameniahidi kwamba, watakwenda kufanya uchunguzi ili minara ijengwe katika maeneo ya Katete, Sopa, Mambonkoswe na Kalembe. Ikishajengwa minara kama mitatu au minne katika maeneo haya, nina uhakika wananchi katika Jimbo la Kalambo wote watapata mawasiliano.

Mimi nakuomba Mheshimiwa Waziri, unisaidie ili Kampuni hii ya *Zain* iweze kufanya kazi hiyo ya kumalizia sehemu hizo ambazo wananchi hawapati mtandao. Katika Kijiji cha Mwazye, mnara umejengwa bondeni, ungejengwa juu ya mlima uliopo

karibu na Kijiji cha Mwazye, nina uhakika Vijiji vya Kambo, Kifone vyote vingepata mawasiliano vizuri ili tuweze kukamilisha mtandao mzuri katika Jimbo langu la Kalambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie juu ya *fair competition*. Kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia, *fair competition* haipo kwa kiwango kikubwa, ndio maana mashirika yetu mawili haya, yanafanya kazi katika mazingira magumu sana. Wakati Shirika la Posta lilipotengana na Shirika la *TTCL*, wengi walifikiri kwamba, Shirika la Posta baada ya muda si zaidi ya miaka minne hivi Shirika hili litakuwa limekuwa, lakini shirika hili ambalo asilimia mia moja ya hisa zake zote au mali yote ile ni ya Serikali limeendelea kudumu.

Kama wenzangu walivyozungumza, halijapewa mtaji hadi leo. Naomba sana Mheshimiwa Waziri, pamoja na kazi nzuri ambayo umeifanya ambayo sisi tunakupongeza, kwa kulisaidia shirika hili. Tunaomba usichoke, uendelee kutusaidia ili wafanyakazi katika Shirika hili la Posta, waweze kupata mtaji wa kufanya kazi na waweze kupata fedha za kufanya uwekezaji. Serikali ichukue madeni yasiyolipika, iangalie zile kodi ambazo *TRA* wamekuwa wakiidai Posta, kiasi ambacho wanalazimika hata kuchukua pesa za wateja kwenda kulipia *TRA*. Suala la *fair competition*, naomba sana yapo makampuni ambayo yameanzishwa, yanafanya kazi zilezile ambazo Posta inafanya; kuchukua vifurushi na vipeto, kuchukua barua, kutuma pesa, lakini hatuna uhakika kama watu hawa wanatozwa fedha au kodi inayolingana na kazi na kodi inayotozwa Posta. Posta kwa kusafirisha barua, wanatozwa kodi lakini mabasi ya makampuni mengi yanafanya biashara ya kusafirisha barua, hawatozwi kodi kwa ajili ya kusafirisha barua, kusafirisha vipeto, kusafirisha fedha, badala yake wanatozwa kodi kwa ajili ya kusafirisha barua na mizigo. Hii si haki, tunaomba sana Serikali iangalie ni jinsi gani ya kuweza kuwatoza wote sawa ili walau wafanye biashara katika mazingira yanayolingana.

Mheshimiwa Naibu Spika, *TTCL* ambao tulifikiri wako salama kwa sababu ya kazi walizokuwa wanazifanya, lakini hivi sasa shirika la simu lipo katika matata makubwa sana, kwa namna ambayo wameingizwa katika mikataba ya ajabu ajabu na hivi sasa wanapata shida. Sasa simu ambazo wanazo, wameshapitwa na makampuni binafsi ambayo yalikuja nyuma na kuahidi kwamba, yatasaidia na yatalipa kwa shirika hili ambalo lipo katika matatizo makubwa sana ya kiundeshaji, kimtaji na mambo mengine ya namna hiyo. Tunaomba shirika hili nalo lipewe uwezo kwa kuwa na *fair competition* na makampuni haya makubwa ambayo sasa yameingia hapa nchini na kufanya biashara ambayo ilikuwa ndio biashara ya msingi ya shirika hili la *TTCL*.

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la kuunganisha Shirika la Posta na Benki ya Posta, ambalo limezungumzwa kwa muda mrefu. Suala hili lingeweza kusaidia sana shirika letu la Posta liweze kufanya vizuri. Kuna wakati mazungumzo yalikuwa yamefikia hatua nzuri, lakini kukatokea mizengwe na matatizo mbalimbali hapo kati. Tunaomba nalo uliangalie liwezekane, kwa sababu mtandao wa Posta umeenea mpaka vijijini; kama Benki ya Posta ingekwenda sambamba na mtandao huu wa Shirika la Posta, nina uhakika Shirika hili nalo lingeweza kufanya vizuri hasa katika maeneo ya vijijini ambako hakuna Benki ya Posta.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kuendeleza Chuo cha Mbeya – *MIST*; Mheshimiwa Waziri, tunakuomba sana chuo hiki kimekuwa ni cha muda mrefu kilijengwa na Warusi; wameacha *structures* ambazo hazijakamilika na majengo ambayo hayajakamilika. Nina uhakika, kama Serikali itawekeza fedha za kutosha, chuo hiki kitakuwa ni cha msingi sana kwa Mkoa wa Mbeya, Mkoa wa Rukwa, Ruvuma, pamoja na Mkoa wa Iringa katika eneo hili la Nyanda za Juu Kusini. Chuo hiki kikishirikiana na vyuo vingine vilivyomo katika Kanda hii, vitaleta maendeleo ya kilimo na mawasiliano katika eneo hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja hii. (*Makofi*)

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii na mimi nichangie kidogo juu ya hoja iliyo mbele yetu. Awali ya yote, naomba kumpongeza kwa dhati kabisa Mheshimiwa Waziri, Mheshimiwa Naibu wa Waziri, Wakurugenzi wote na Watendaji wote wa Wizara hii. Wametuletea hotuba nzuri, yaani kinyume chake ni hotuba fupi sana, lakini imejaa mambo mengi kuliko hotuba nyingine; zinakuwa ndefu lakini mambo machache. Hongera nyingi sana na mimi naunga mkono hoja kwa asilimia mia moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nizungumzie suala la mawasiliano. Mawasiliano yanaanza ndani ya nyumba, yakiharibika hakuna maendeleo ndani ya nyumba. Mawasiliano Kiwilaya, Kitaifa na Kimataifa. Kwa hiyo, jambo kubwa ni kwamba, Wananchi wa Rufiji wanaomba kuishukuru sana Wizara hii kwa kupeleka *TTCL new exchange machines*, kwa Mji wa Utete, Kibiti na Ikwiriri, tunawashukuru sana. Vile vile naomba nitoe shukrani kwa makampuni ya simu za viganja, yaani Celtel/Zain, Tigo, Vodacom, hawa wapo katika miji yote mikubwa mitatu ya Wilaya ya Rufiji, yaani Utete, Ikwiriri na Kibiti na hata Muhoro.

Ninaomba nimitaje Naibu wa Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, tumemsumbuwa sana kule Rufiji na tunashukuru sasa *Celtel* wamepeleka huduma ya simu ya kiganja mpaka kijiji cha mwisho karibu na *Selous*, kinaitwa Mloka. Natoa pongezi kwa kazi nzuri ya kampuni hii. Kampuni hii vilevile inajenga minara katika Kijiji cha Kilimani, Ngarambe na Mbwara. Hili jambo linatia sana moyo na ninaomba ikiwezekana, Waziri uwaandikie barua kwamba, yupo Mbunge wa Rufiji anawashukuru sana. Hata hivyo, nilikuwa naomba Celtel au Zain wafahamu tu kuwa, kuna *gap* ya kilometra karibu 65 kutoka mnara hadi mnara; kwa mfano, Vijiji vya Ngorongo, Nyikanza, Nyaminywili na Ntanza, havipati mawasiliano kutoka mnara wa Mloka. Kwa hiyo, naomba teknolojia iongezwe ili watu hawa nao wapate au waongezewe mnara au waongeze ukubwa wa mnara ule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kushukuru sana na kufurahishwa sana na shuguli za simu za viganja, lipo suala la bei. Gharama ni kubwa mno, inafika mahali hata sisi wenye kipato kizuri tunaona tabu kutumia simu hizi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba

ikubalike tu kwamba, hawa wawekezaji wanataka faida na sisi tumeweka kodi pale. Kwa hiyo, lilikuwa jambo zuri kwamba, Serikali na *TICRA* na wawekezaji wakae katika *round table* ioneckane gharama hasa iliyotumika kufanya mtandao ule ufanye kazi katika nchi yetu, inafanana na gharama ya fedha tunazolipa? Inakuwa kinyume, sisi tumetembea; najua ukiwa India pale dola tano unaweza kuzungumza kwa saa hata tatu au nne, lakini hapa kwetu dola tano utasikia inakata tu basi, kama hujui ujue hamna kitu. Kwa hiyo, nadhani hili ni jambo muhimu kwa sababu hii ni *service*; hivi hawa wenzetu hawaoni kama wanatunyonya sana jamani? Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri, ukubali muwaite hawa jamaa mzungumze ili warudishe bei iwe chini kidogo. Haitoshi tu kuwa na wema wa *ku-sponsor* mipira, *wana-sponsor* sijui shule mbili, lakini unanyonya watu kiasi kwamba, mwisho tutashindwa hata kutumia simu hizi. Kwa hiyo, nilikuwa naomba sana suala hili litiliwe mkazo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa naomba nizungumzie juu ya sayansi na teknolojia. Hili ni suala muhimu sana na ninadhani Serikali nzima ingekubali tu kwamba, *Science and Technology Ministry* ndio ingekuwa *lead Ministry*, kwa sababu hakuna maendeleo popote duniani. Hapa nilipo mimi nazungumza na ninasikika shauri ya sayansi na teknolojia, ingekuwa hii imezimika hapa msingenipata. Acha hiyo, wewe zungumza katika kila nyanja, bado utakuta sayansi na teknolojia ndio jibu la kuleta maendeleo. Kitu kinachotisha ni kwamba, Serikali haionyeshi kama inataka Sayansi na Teknolojia iwe *lead Ministry*, ukitazama bajeti yake, inatisha.

Kwa hiyo, sayansi ni ghali; nataka kurudia kuwa sayansi na teknolojia ni ghali, kwa hiyo, Serikali ni lazima ikubali kutoa fedha nyingi katika Wizara hii ili tupate maendeleo na sisi tuingie katika dunia ya utandawazi. Sayansi inatakiwa itoe majibu kwa kila mtu na kwa kila nchi. Wenzetu Marekani wanazungumzia sayansi itawaambia kuna nini juu ya sayari ya *Mars*, lakini sisi hapa tunataka sayansi ituambie juu ya kubadilisha kilimo chetu kikawa kilimo chenye faida kubwa, kwa maana ya utafiti wa mbegu, *soil*, vyombo vyenyewe, yaani vitendea kazi, tunataka sayansi iseme. Inasaidiaje kutatua matatizo ya uvuvi, matatizo ya viwandani, matatizo mengi ya kuleta maendeleo yako katika sayansi. Sayansi inatakiwa itupatie majibu. Magonjwa ya kuambukiza Tanzania; pamoja na UKIMWI tumetoa fedha kiasi gani ili watu wafanye utafiti ili na sisi tuepukane na magonjwa haya? Kwa hiyo, tunayo kazi kubwa na naomba tuipe Wizara hii fedha za kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna matatizo ya utendaji kazi katika Serikali, katika uchumi wa nchi kwa maana ya biashara na viwanda, kwa sababu watu wetu bado wapo nyuma katika sayansi na teknolojia. Hatujafikia kitu kinachoitwa *the critical mass*; *critical mass* ni kwamba, tukiweza kuwa na watu, *technically TEKNOHAMA literate* kwa *level* ya 50%, nchi hiyo inaweza kwenda mbele sana katika maendeleo na ndio alama ya kusema kwamba, sasa tunaendelea. Lakini unapofika katika Wizara au viongozi hawa ukiwapa kompyuta wanaiogopa, hawajui kutafuta taarifa kutoka kwenye *internet* na hii nadhani sasa hivi nchi yetu inaweza kuwa labda wenye uwezo huo ni kama 20%. Sasa hapa ni vizuri, sisi madaktari tunasema ukijua ndwele (ugonjwa), yaani *the diagnosis* basi inakuwa ni rahisi kutibu. Tunasema hivi; ukitaka maendeleo ya haraka, *diagnosis* yake ni kwamba ni lazima unyanyue sayansi na teknolojia katika utendaji wote

wa *economy* nzima kutoka Serikalini, katika viwanda, katika mashamba na pia katika biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumpongeza Waziri kwamba, katika kitabu chake cha hotuba, ukurasa wa 34 ameonyesha kwamba, udahili wa wanasayansi umeongezeka sana hasa katika Chuo cha Dar es Salaam, *DIT* na *MIST* – Mbeya. Hii ni alama nzuri, lakini naomba nirudie yale niliyoyasema katika bajeti ya elimu kwamba, Serikali yetu ikubali kuwaweka wanasayansi mstari wa mbele katika maslahi yao, marupurupu mengine na kuiheshimu sayansi; bila kufanya hivyo tatarudi palepale. Ninaomba sana, tuache wivu, tuwape wanasayansi mishahara mizuri, isitoshe ninaomba vijana wanaochukua mchepuo wa sayansi, wafutiwe ada zote za shule mpaka *University*. Hiyo haitoshi, bado Serikali ifanye kitu kinachoitwa *aggressive recruitment*. Iende nje itangaze tunataka walimu wa sayansi wengi Tanzania na wapate walimu wengi waje. Nchi marafiki kama wana *peace corps programme* ili tupate walimu wengi tufundishe sayansi katika nchi yetu, ndio msingi wa maendeleo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, lipo suala la nishati mbadala; kule Rufiji ng'ombe wamekuja siku hizi tu wala yale mavi yao hatuwezi kuyagusa.

**NAIBU SPIKA:** Tunasema kinyesi bwana wewe!

**MHE. PROF. IDRIS A. MTULIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, samahani, kinyesi. Ile *bio-gas*, wazee wangu mtusamehe sisi. Sasa na ukitazama upopo kule hauvumi kama Dodoma, lakini kitu kimoja tuna hakika sana, jua lipo kila mahali katika nchi yetu hii. Kwa hiyo, nilikuwa ninaiomba Wizara, ifanye utafiti mpya, sio kugundua nishati hiyo hapana. Wafanye utafiti ili vile vyombo vya kutoa nishati hii kwa maana ya *solar panels* zitengenezwe kwa bei rahisi na ikiwezekana Serikali. Kwa maana hapa ninamtaka hata ndugu yangu Mheshimiwa Ngeleja, Waziri wa Nishati, wakubali *ksponsor* namna ya utengenezaji wa *solar panels* kwa bei rahisi; kwa maana watoe *subsidies* ili watu wengi wanunue *solar panels* ili tuweze kupata *rural electrification* kwa kutumia *solar panels* ambazo zitamfikia kila mtu na maisha yetu yatanyanyuka sana. Hili lipo katika uwezo wetu na ninadhani ni suala la kuamua tu na mimi naomba sana Mheshimiwa Waziri, hili ulitilie maanani. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, lipo suala la *atomic energy*; hii ni nishati ya hali ya juu, inataka mazungumzo mengi na mikataba, lakini tusiifumbie macho kwa sababu siku hizi hiyo ndio njia nzuri ya kupata umeme na nishati ya kutuwezesha nchi hii bila tabu ya kwenda katika *gas* au kutumia *diesel* au kutumia maji (*hydro power*). Baada ya kusema haya, naomba nirudie machache kwa msisitizo; Mheshimiwa Waziri na Serikali nzima ikubali, bila sayansi hatuwezi kwenda mbele. Serikali ikubali kuongeza bajeti ya Wizara hii na mkubali kufuta karo zote za wanafunzi wa mchepuo wa sayansi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema haya, naunga mkono hoja na ahsante kwa kunisikiliza.

**MHE. KAIKA S. TELELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia Wizara hii ya Mawasiliano, Sayansi na

Teknolojia; Wizara ambayo ni mpya. Kama kawaida, naomba na mimi nimpongeze sana Waziri, Mheshimiwa Prof. Peter Msolla, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dr. Maua Daftari, Katibu Mkuu wa Wizara na Wataalam wote ambao wametutayarishia hotuba nzuri, fupi, lakini imejaa mambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, sayansi na teknolojia katika maendeleo ya taifa ni muhimu. Juzi tulipokuwa tunachangia Wizara ya Viwanda, Biashara na Masoko, ilionekana kwamba ni lazima kwanza, tufanye mapinduzi ya kilimo ndipo twende kwenye viwanda na kwa maana hiyo tunaweza kupata maendeleo ya taifa letu. Vivyo hivyo tukifanya mapinduzi katika sayansi na teknolojia, maendeleo ya taifa letu yanaweza yakapatikana mijini na vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa muda mrefu sasa, masomo ya sayansi na teknolojia, mafunzo ya ufundi kwa vijana wetu kuanzia shule za msingi, sekondari na vyuo vikuu, hayajapewa uzito au umuhimu unaostahili na ndio maana tunakuwa na wanafunzi wachache wanaopenda kuchukua masomo ya sayansi, lakini wengi wanachukua masomo ya *arts*. Sasa sijui ni mepesi au namna gani, lakini uzito hatujautilia katika masomo ya sayansi? Lazima tufanye mabadiliko makubwa na ya haraka sana; ni lazima tujitahidi sana kuwasomesha wanafunzi wetu na kuwashamasisha wapende hayo masomo ya sayansi. Pia kama alivyokiri Mheshimiwa Waziri mwenyewe katika ukurasa wa 11 kwamba, naomba ninukuu: “Katika kuwashamasisha wanafunzi kupenda masomo ya sayansi, Wizara kwa kushirikiana na taasisi za mafunzo, inaendelea na mafunzo maalum kwa wanafunzi wa kike (*Pre-entry Programme for Female Science Students*), katika kozi ya ufundi na sayansi.” Anasema pia imetoa tuze kwa wahitimu wa kike katika ngazi mbalimbali, wanaofanya vizuri katika masomo ya sayansi. Naomba hili liwe *applied* kwa wanafunzi wa kiume, kwa sababu katika taifa, wote tunahitaji wanasayansi waliobobea wa kike na wa kiume. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kawaida matokeo ya utafiti yanatakiwa yaelekezwe kwa walengwa, lakini inavyoonekana ni kwamba, tafiti nyingi zinafanyika katika sehemu mbalimbali, katika Idara na katika taasisi mbalimbali, lakini utafiti ule hauelekezwi kwa walengwa ili kuweza kuboresha maisha ya wananchi, kwa maana ya kuwaondolea umaskini au kwa kupunguza umaskini wa wananchi uliokithiri kwa kiasi kikubwa. Kwa mfano, kule Ngorongoro, eneo la Ngorongoro ni eneo la Kimataifa, ni eneo la urithi wa dunia, ambalo limefanyiwa utafiti mwangi sana wa wanyamapor na binadamu wanavyoishi na wanyama wale bila madhara. Utafiti umefanyika mkubwa sana, lakini kwa kweli ukijaribu kuangalia maendeleo ya watu pale, hayalingani kabisa na utafiti na mapendekezo yanayotokana na utafiti unaofanywa na wataalam mbalimbali na kwamba, mapendekezo yanatolewa kwa upande wa wanyamapor lakini pia kwa binadamu kwamba, wakiweza kufanya hili na lile, wanaweza wakapenda kuendelea kuhifadhi wanyama hawa kwa ubora zaidi. Mkazo unatiliwa zaidi kwa wanyamapor kuliko maendeleo ya watu.

Kwa mfano, kasi ya kujenga hoteli na lodge katika eneo la Ngorongoro ni kubwa na haina vikwazo vya kusema kwamba, lazima ifanywe *Environment Impact Assessment (EIA)* na kadhalika. Katika kujenga Shule za Msingi, Shule za Sekondari au Shule za

Ufundu, unaambiwa lazima ifanyike *EIA*, inaonekana sasa kama hii *EIA* inakuwa adui wa maendeleo, kitu ambacho sidhani kama ni kweli. Hizi ni tafsiri za ovyo za watu tu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vivyo hivyo katika kujenga nyumba bora za kuishi watu, hilo nalo utaambiwa *Environmental Impact Assessment*, mimi sikatai lakini kwa kweli *EIA* isitafsiriwe kama ni adui au kitu cha kuzuia maendeleo ya watu. Vivyo hivyo, kwa ujenzi wa minara ya simu, unaambiwa lazima *EIA* ifanyike; kwa nini tusifanye *Environmental Audit* kwanza, yakajengwa kwa sababu hivi vitu tunavihitaji kwa ajili ya mawasiliano lakini tukafanya *Environmental Audit* kwamba, hii itakuja baadaye na siyo kutanguliza *Environmental Impact Assessment* kwa sababu inachukua muda mrefu iende Baraza la Mazingira, ni matatizo makubwa sana. Mimi nina shule zangu mbili zimependekezwa kujengwa katika Kata ya Nainokonoka na Olbalbal; huu ni mwaka wa nane hatujaweza kujenga shule zile, pesa tunazitenga lakini shule hazijengwi kwa sababu ya vikwazo kama hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tulishasema pia kwamba, katika eneo la hifadhi, hakuna kilimo wala biashara ya aina yoyote, lakini wangeiimarisha sekta ya mifugo wale ndugu zangu wasingegekuwa na malalamiko, lakini hakuna programu ambayo iko wazi katika kujaribu kusaidia hilo zao la mifugo, ambayo inawabeba Wananchi wengi wa Ngorongoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, simu za mkononi pamoja na kwamba, zinaendeshwa kwa sehemu kubwa na kampuni au sekta binafsi, zimesaidia sana suala la mawasiliano vijijini na mijini. Napenda niwashukuru sana Kampuni za Vodacom, Celtel au Zain siku hizi na Tigo, lakini Vodacom na Celtel ndiyo makampuni ambayo yametangulia kwenda huko Loliondo na Waso na kuweka mtandao kule. Niwahamasishe pia wale wa Tigo na Zantel na makampuni mengine yote ambayo yapo tayari kufanya kazi hii, waelekee huko Ngorongoro, Loliondo, kwa sababu ni Wilaya ambayo iko pembezoni ili tusiendelee na sisi kuangalia luninga za Kenya na kusikiliza Redio ya KBC.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeambiwa kwamba, hizi simu za mkononi zinachangia katika pato ghafi la taifa (20.1%), si haba lakini kwa kweli gharama ya simu hizi ni kubwa sana. Kama walivyosema wenzangu, Serikali iangalie namna ya kupunguza gharama hizi kwa sababu ni kubwa ili wananchi wengi waweze kununua na kuzitumia. Katika Jimbo langu la Uchaguzi, maeneo kama Engaresero, Malambo, Digodigo, Sendui, Oldonyo-Sambu, Pinyinyi na Monik ni maeneo ambayo hayana mawasiliano hata kidogo. Nimeshazungumza na Mheshimiwa Naibu Waziri, nimemuandikia Naibu Waziri, nina imani atanisaidia, tumekubaliana lakini nataka wananchi wasikie vilevile kwamba, tunazungumzia maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, watumiaji wa simu za mkononi wamekuwa wengi sana na kada mbalimbali za maisha; wazee, vijana, matajiri na maskini wafanye biashara, wanatumia wafugaji na kadhalik. Naomba haya makampuni yanapokuwa yanakwenda kule, wasiende tu kuhesabu nyumba za batii, hamtapata watu; mtakadiria tu kwamba, watumiaji wa hizi simu ni wachache sana katika maeneo yale, lakini wale walioko

mbugani na ng'ombe wao na mifugo yao, wanakuwa na *handsets* na kwa hiyo wanakuwa na haki ya kupata hizi simu.

Mheshimiwa Naibu Spika, simu hizi zinatumika katika kutoa taarifa mbalimbali za maendeleo na wananchi wanapashana habari, wanatoa taarifa za ujambazi, wizi wa mifugo, kuvamiwa watalii na watu wengine kupashana habari kwa ujumla; kwa hiyo, ni kitu muhimu sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru kwa kunipa nafasi na ninaunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofit*)

**NAIBU SPIKA:** Nataka niamini kwamba, watoto walioko upande huu ndiyo wale wa Chazungwa, kama ni wao wasimame.

(*Hapa wageni walijotajwa walismama*)

**NAIBU SPIKA:** Karibuni sana tumeambiwa mlipata matatizo ya usafiri lakini hatimaye mmeefika, ingawa mmekikosa kipindi cha maswali cha asubuhi. Karibuni sana. (*Makofit*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Dr. Harrison G. Mwakyembe, halafu msemaji wetu mwengine atakuwa ooh! simwoni tena.

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa niweze kuchangia.

Nina mambo machache na nitaongea kwa kifupi tu. Kwanza, nimpongeze Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa bajeti nzuri ya Wizara yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, niende moja kwa moja katika ukurasa wa nane wa Hotuba ya Waziri, ambapo Waziri ananukuu Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2005 ikielekeza Sekta hii ya Sayansi na Teknolojia. Ninanukuu: “Kuingia katika utaratibu wa kusajili na kulinda haki miliki za matokeo ya ubunifu kwa watafiti na kwa Taifa, yaani *patenting and protecting*.”

Mheshimiwa Naibu Spika, ubunifu daima unatokana na utafiti na utafiti unawekezwa na ndiyo maana Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya 2005, inaligusia suala hili vizuri sana kuielekeza sekta hii kwamba iwekeze zaidi kwenye shughuli za utafiti na maendeleo, yaani kwenye *R and D, Research and Development*; na kwamba itengewe kiasi cha angalau asilimia moja ya Bajeti ya Serikali kila mwaka. Hayo ndiyo maelekezo ya Ilani ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ukurasa wa 9 wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, haelezi waziwazi *R and D, Research Development*, imechukua asilimia ngapi kwenye bajeti hii. Huioni waziwazi, lakini anatueleza tu na ninamnukuu hapa: “Tengeo la Serikali kwa upande wa utafiti limeongezeka kutoka 0.022% na kufikia 0.08% ya Pato la Taifa.”

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli ongezeko hili ni dogo mno, ukizingatia kwamba, nchi yetu ilishiriki katika *The Lagos Plan of Action for Accelerated Development in Africa*, ambayo iliweka kwenye miaka ya 70, asilimia moja ya Pato la Taifa kuwa ndiyo kiwango cha chini ambacho nchi zote za Kiafrika zinatakiwa zifike na hata kwenda mbele zaidi. Sasa kwa mwendo huu wa kusuasua, azma hiyo sidhani kama tutaifikia miaka ya hivi karibuni. Tutaendelea kuwa duni katika Sayansi na Teknolojia sekta ambayo wote tunakubaliana kwamba, ndiyo nyenzo ya msingi ya maendeleo ya dunia ya leo na dunia ya kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba tu Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, kwa mwaka unaokuja, tupate picha tofauti kidogo au tengeo la Serikali kwa ajili ya kuendeleza *Research and Development* iwe imeongezeka kidogo.

Ukurasa wa kumi wa Hotuba ya Mheshimiwa Waziri, unaeleza mbinu mbalimbali za kuhamasisha wanafunzi kupenda masomo ya sayansi, mbinu ambazo mimi kimsingi naafiki kuwa ni nzuri sana. Namshukuru sana Mbunge mwenzangu, Mheshimiwa Prof. Idris Ali Mtulia. Ameongea vizuri na ameongeza vivutio zaidi. Ametoka kusema kwamba, mishahara iwe mizuri zaidi kwa Wataalam wa Sayansi, suala ambalo mimi nakubaliana naye na vilevile ametoa pendekezo zuri sana kwamba, pengine wanafunzi wetu wanaosoma sayansi, wasamehewe ada kutoka shule za chini kabisa mpaka vyuo vikuu. Hii ni hoja nzuri kabisa. Mbali na mbinu hizi, mimi ninaomba Wizara ishirikiane na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu katika kupambana na wimbi la vyeti feki nchini. Vyeti vya aina hii, vinawapa vijana wetu imani feki (*false confidence*) kuwa, hata usipojitätidi sana shuleni, hata usipofaulu bado ipo nafasi kwani kuna vyeti vya kununua. Sasa bila kupambana na hiyo tabia iliyojengeka sana sasa hivi, tutakuwa na tatizo kubwa na ningombaa Mheshimiwa Waziri, naelewa amepambana sana na hili suala, aendelee tu kupambana nalo bila kuangalia sura.

Mheshimiwa Naibu Spika, si rahisi kufanikiwa kwenye *Science and Technology* ikiwa msingi wa elimu ni mbovu, si mzuri. Kwa hiyo, upo umuhimu kwa Wizara hii ya Mawasiliano kwa kweli kufanya kazi kwa karibu sana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundu ili elimu yetu ya msingi iwe inawaandaa vijana wetu barabara ili waweze kupambana na hatua za juu za masomo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, kuna tabia ambayo imezuka nchini hapa, tunaweza kuiona ni ya kawaida tu lakini inaathiri sana fikra na maendeleo ya watoto wetu. Ni vitu ambavyo havikuwepo huko nyuma, lakini sasa hivi imezuka tabia ya kilimbukeni kweli kweli. Mtoto anamaliza darasa la saba, ni sherehe kubwa na mpaka joho la *graduation* anavishwa. Mtoto anamaliza *Form Four* ni sherehe kubwa na wengine mpaka wanachangisha, yaani wazazi wao; na joho la *graduation*. Mtu anahitimoo Cheti na joho! Inakuwa kama hatuna *order* na mpangilio sahihi nchini. Mimi ninaomba Serikali iwe makini zaidi kama ilivyokuwa huko nyuma. Haya majoho yanayovishwa kwa kozi mbalimbali huko chini yangepingwa tu marufuku.

Mheshimiwa Naibu Spika, zamani uvaaji wa joho ilikuwa ni moja ya vitu vinavyomtia ari kijana kuweza kusoma kwa nguvu zaidi; kwamba, mimi nataka nivae joho lile la Chuo Kikuu. Lakini kama anaweza kulivaa joho Darasa la Saba; atapigania nini? Naweza kuvalaa joho kwa Cheti tu cha Uhasibu, nitapigania nini?

**NAIBU SPIKA:** Nakwambia Chekechea!

**MHE. DR. HARRISON G. MWAKYEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Kweli hata Chekechea. Wazazi wa siku hizi sijui Luninga zinatuharibu; eti na wao wanachangisha eti mwanangu amemaliza Chekechea!

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ningeomba Mheshimiwa Waziri ayaangalie sana.

Napendekeza vilevile suala kuhusu Viongozi wetu. Mimi naomba Viongozi wanisamehe, lakini nadhani nasema ukweli. Viongozi wetu wengi wancomesha watoto wao nje ya nchi. Mimi naamini hii imetumaliza sana Watanzania, kwa sababu Viongozi wenyewe watoto nje ya nchi, hawapati msukumo ule wa kweli wa kuhangaikia maendeleo ya elimu hapa nchini. Si wanomasoma nje watoto wake? Kwa hiyo, mimi naomba na ninapendekeza kuwa, moja ya masharti ya kupewa uongozi Tanzania sasa iwe ni kuhakikisha watoto wako wanomasoma hapa hapa. Tubanane hapa hapa ili na wewe uweze kutumia muda wako wote kuhakikisha kwamba, elimu hapa inakuwa bora. Sasa kama wewe ni kiongozi, una nafasi na fursa ya kusomesha watoto wako *South Africa* na kadhalika, utapata wapi ari ya kusukuma elimu hapa nchini?

Mheshimiwa Naibu Spika, nimefarijika kiasi na hali ambayo Mheshimiwa Waziri ameitoa ya kuboresha hali kwa ujumla Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Mbeya. Wabunge wenzangu Mheshimiwa Benson Mpesa na Mheshimiwa Ludovick Mwananzila wameliongelea hili kwa kirefu. Basi tunaomba *seriousness* kidogo iwepo kwa Serikali katika kukiendeleza chuo hiki ambacho kwa kipindi fulani, tulidhani hiki ni chuo yatima. Tunasubiri kwa hamu utekelezaji tulioahidiwa hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakuhakikishia bajeti ijayo tutafuatilia kila *aspect* ambayo Mheshimiwa Waziri ameahidi kuwa itatimizwa kwa ajili ya hicho chuo.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, lengo letu limebaki palepale la kuendelea kudai kwamba, taasisi hii iwe Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia ili hapo baadaye mahitaji yakiongezeka, chuo hiki nacho kiweze kuunda taasisi mbalimbali chini yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kumalizia, naomba niipongeze Serikali kwa kuliokoa Shirika la Posta. Lilikuwa linadondoka. Hii hatua ya kubeba na kufuta madeni yote ili kusafisha mizania ya shirika, kwa kweli ilikuwa ni hatua muhimu sana. Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri, tunawapongeza sana.

Lakini nitoe pendelezo moja dogo tu la Shirika letu la Posta kuwa wabunifu zaidi pia katika shughuli zao. Mimi nimekuwa Zambia, nimeliona Shirika la Posta kule

likitumia utaratibu tofauti katika kufanya *delivery*. Hapa Tanzania Shirika la Posta linafanya *delivery* usiku na *vans* hizi tunazoziita *hard top*, zinakimbia zimebeba magazeti, barua na vifurushi. Tunakutana nazo, kwa kweli zinafanya kazi kubwa sana. Lakini wenzetu Zambia hawatumii magari haya madogo madogo, wanatumia *special luxury buses*, mabasi mazuri sana ambayo yanatembea usiku tu. Kwa mfano, Shirika letu hapa liki-*adopt* hiyo *system* likaomba *special licence*, mabasi ya *luxury* mazuri yatatoka usiku kusafirisha abiria lakini yanabebe vilevile yatabeba vifurushi. Vilevile wanakuwa na Askari wa kutosha mle ndani. Watafanya biashara nzuri sana. Nimeona *it is working very well* kwa wenzetu wa Zambia badala ya kutuma vijigari hivi vidogovidogo, vinakwenda na kurudi. Ni kumaliza mafuta bure, wala huwezi ku-*maximise investment* yako.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba niseme kwamba, mimi naunga mkono hoja na ninaomba niishie hapa. Ahsante sana.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikushukuru sana kwa kunipa nafasi jioni hii, nami nichangie machache sana kwa sababu nilikuwa sijajiaanda vizuri, nilifikiri tutaendelea mpaka Jumatatu.

Naomba nikushukuru kwanza, kwa kunipa nafasi na pia nimpongeze Mheshimiwa Waziri, kwa kutuletea hotuba nzuri, pamoja na Watendaji wake wote.

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwamba, mimi naiunga mkono hotuba hii asilimia mia kwa mia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba kutoa ushauri kama walivyotoa ushauri wenzangu; kama tunataka tufanye vizuri zaidi kwa jinsi tunavyokwenda na mabadiliko ya dunia, Wizara hii ni Wizara muhimu sana. Lakini nayo ili iende kwa kasi, tunaomba Wizara hii si vibaya wakashirikiana kwa karibu zaidi na Tume ya Mipango na Wizara ya Elimu, kwa sababu endapo watasema wakae wao peke yao bila kushirikiana na Tume ya Mipango ambayo itaanizishwa hivi karibuni, mawazo yao ambayo watakuwa wameyafikiria kwa sababu hayatakuwa kwenye Tume ya Mipango, nina uhakika hatutafanikiwa. Ukweli ni kwamba, Wizara hii ndiyo injini ya kutupeleka kule tunakotaka kwenda.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niulize swali dogo tu; ukotoka hapa ukienda Dodoma Hoteli lakini kwa nyuma yake kama sikosei, kuna jengo tunaambiwa ni la Posta au la Simu. Jengo lile lipo pale limekaa zaidi ya miaka 13 sasa. Mheshimiwa Waziri, atakapohitimisha si vibaya kutueleza lile jengo ni mali ya nani; na kwa nini limetelekezwa kiasi kile? Zile ni pesa za Serikali zimelala pale, ingekuwa ni vizuri zaidi; sasa hivi tunasema kwamba tuhamie Dodoma, jengo lile nina uhakika kama Serikali ingetaka lile jengo lingeweza kukarabatiwa kwa sababu ni mali ya Serikali, lingeweza kukamilishwa na likatumika kwa ajili ya shughuli ya Ofisi za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine la pili, mtusaidie na wenzangu wamesema, kwa sababu hivi sasa Tanzania imekuwa ni sehemu ya kuchukua vitu vibovu kutoka huko nje.

Tunaletewa sisi vitu vibovu hapa, tunanunua na tunavitumia. Sasa kwa sababu tuna wataalam wetu hapa, zipo simu mbovu zinakuja tunazitumia na tunaziweka kwenye masikio, maana yake ili usikilize ni lazima simu hiyo iwekwe kwenye masikio, mionzi yake inapita kwenye kichwa na kadhalika. Mtuambie ni lini sasa kazi itafanyika ya kuziangalia zile simu bora, ndizo ziruhusiwe kuingia nchini badala ya kila simu kuingia na kuzitumia bila kuzichunguza.

Mheshimiwa Naibu Spika, namwomba sana Mheshimiwa Waziri, hili ulitafute lakini kwa kweli endapo tutaacha hivi hivi, baada ya muda inawezekana Watanzania wako watapata matatizo.

La tatu, kama nilivyosema awali kwamba ni vizuri sasa kama kwa kweli tunataka twende na Sayansi na Teknolojia, Wizara ya Elimu, Wizara yako na Tume ya Mipango, wakakaa pamoja. Ili tupate wataalam wa kuweza kusimamia mambo ya Sayansi na Teknolojia ni lazima tupate wasomi waliosoma Sayansi na si vinginevyo. Kwa hiyo, tukifanya hivyo nina uhakika tutafika mbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine nizungumzie kuhusu tovuti za Serikali. *Websites* hizi tuna utaratibu wa kuzichukua lakini nina uhakika *kuzi-update*, yaani kuziweka ziwe taarifa za leo au za jana, bado hatujafika huko. Utashangaa leo tarehe 15 Agosti, 2008, ukienda kufungua *Website* ya Bunge, utakuta taarifa za kifo cha Marehemu Mheshimiwa Chacha Wangwe. Marehemu Chacha Wangwe amefariki karibu wiki moja na zaidi sasa, lakini zile *current information* hazipo. Sasa kuna upungufu na matatizo ya *kuzi-update* hizi *information*, kwa sababu hizi taarifa wenzetu kule nje wanasesma tunataka kuangalia *website* ya Bunge, anakuta taarifa za miezi miwili nyuma. Utashangaa ukienda pale Maelezo, nafikiri na ninyi wenyewe mmeefika pale; wameshindwa jinsi ya kuiendesha imekaa pale sasa haina mtu wa kuisimamia hii *website* ya Serikali. Leo ukienda pale Maelezo utakuta wamebandika picha ukutani za ziara za Mheshimiwa Rais; vitu vimeshapitwa na wakati. Ndiyo maana kukawa na *Website* ya Serikali, vitu vile unatakiwa uvionyeshe ili kila mtu atakayefungua aliyepo Kigoma, Musoma na kadhalika, aangalie vitu vilivyofanyika jana na juzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini utashangaa inawezekana hata *website* za Wizara nyingine; Wizara ya Utalii, watalii wako nje kule wanataka kuangalia hali ya hewa ya Tanzania, wanataka kuangalia wapi waende lazima watakwenda kwenye *website*, wanakuta imedumaa haina maelezo ya kutosha. Utashangaa, unaweza ukakuta pameandikwa matatizo tu mle ndani badala kuelezea mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, cha kushangaza, tunaambiwa ATCL haina *website* kama ipo ni mbuvu. Kwa sayansi ya leo, watu hawataki kuandika barua, wanataka waingie kwenye *website* waangalie Wizara, Idara na Serikali; waangalie kilichopo ni nini ambacho ukitoka hapa ukienda kwenye mkoaa fulani au kwenye Wizara fulani ukitaka kuangalia ukikute, lakini unafungua *website* unakuta hakuna kitu. Mimi nashauri ni vizuri sasa hao wataalam wa IT tuwaache, lakini ni lazima hizi *website* ili ziwe zinafanyiwa kazi lazima waandishi wa habari watumike, yaani waajiriwe si vinginevyo. Ukisema tu kwamba, umchukue huyu mtaalamu wa IT, hataweza ku-*update information*

kama inavyotakiwa, lakini kama utakuwa na Mwandishi wa Habari aliyebolea utakuta taarifa za Serikali zipo tena mpya. Watu wengi sasa utashangaa wanaangalia kwenye *website* ya Michuzi. Michuzi ni Mwandishi mmoja yupo Dar es Salaam, watu wanaangalia *website* ya Michuzi badala ya kuangalia *website* ya Serikali, kwa sababu kila wakati anaisugua anai-update.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba sana wenzetu basi tutumie wataalam zaidi kuliko kutumia hawa watu wa IT. Watu wa *IT* wawepo lakini Waandishi wa Habari ni vizuri zaidi wakatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba uniruhusu kwa kumalizia, nimpongeze sana Naibu Waziri, Mheshimiwa Maua Daftari, kwa kazi nzuri aliyoifanya. Tulileta maombi kama Wabunge, mimi na Mheshimiwa Bujiku Sakila, kwa Wilaya yetu ya Kwimba; hivi sasa mawasiliano yapo kila sehemu. Tunashukuru sana na tunaomba tuendelee hivyo hivyo. Sijui ule utaratibu ukoje, lakini tunakwenda na teknolojia, nafikiri na wenzangu wamesema minara imezidi, unaweza ukakuta sehemu moja ina minara mitano. Sasa tuone namna gani kama wanaweza hawa wakashirikiana badala ya kuweka minara mitano ikawepo miwili au mmoja ikiwezekana. Ukitoka hapo nje ukiangalia kule mlimani, utaona ule utitiri wa minara. Mimi nashauri, kwa sababu haya ni mambo ya kitaalamu, si vibaya sana basi minara hiyo nayo ikapunguzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu Mkongo wa Taifa unaoitwa *Fibre Optic Cable*, Mradi huu kama ukisimamiwa vizuri na ukatekelezwa vizuri, huyu ndiye mkombozi wa mawasiliano kama huu Mradi ukienda vizuri hata kwenye shule zetu na kwenye hospitali. Utasaidia sana namna ya kufundisha, lakini pia utasaidia sana hata mtu anaweza akawa Muhimbili akafanya *operation* akiwa Bugando Hospitali. Kwa hiyo, nashauri Mradi huu uharakishwe ili ulete tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hayo, nirudie tena kwamba, nakushukuru sana na ninaunga mkono hoja.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, napenda kusema kwamba, wale niliokuwa nao kwenye orodha, ukiondoa watatu ambao hawapo humu ndani, hakuna aliyebacki, kwa hiyo wamekwisha. Sasa hii Wizara ilikuwa ni ya siku mbili, lakini kwa sababu wachangiaji wamekwisha, Jumatatu asubuhi Waziri na Naibu wake, watapewa muda wa kujibu hoja hizi mlizozitoa, halafu jioni yaani saa kumi na moja, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wataingia. Jumatatu hiyo hiyo mtapewa mabadiliko kidogo ya ratiba za Wizara zilizobaki, kwa sababu kadiri tunavyoendelea, basi mambo yanabadilika kidogo.

Kwa hiyo, Jumatatu mtapewa mabadiliko ya Utaratibu wa Wizara za kuchangia na bahati nzuri Wizara ya Fedha na Uchumi katika ratiba ya sasa, ilikuwa na siku moja lakini tumeongeta kwa hiyo zitakuwa siku mbili, kwa sababu tunapozungumza hali ya uchumi wa nchi hatuzungumzii Wizara yenyewe. Kwa hiyo, tutapata nafasi ya kuzungumzia Wizara yenyewe kwa muda wa siku mbili, mabadiliko mtayapata siku ya Jumatatu. Lakini Jumatatu jioni, yaani saa kumi na moja, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la

Kujenga Taifa itaingia. Kwa hiyo, Kamati inayohusika ijiandae na Wasemaji wa Kambi ya Upinzani pia wajiandae, kwa sababu itabidi Jumatatu asubuhi waweke hati zao hapa Mezani, kwa hiyo muwe tayari. Kwa hiyo, nina matangazo machache, mengine ni kukumbusha, lakini lingine jipyä ni kwamba, Mkugenzi Msaidizi wa Huduma za Wabunge anasema niwatangazie Waheshimiwa Wabunge kwamba, kuna kikundi cha Wajasiriamali kiitwacho Somo Moto, kinafanya maonyesho ya aina mbalimbali ya mavazi kwenye Viwanja vya Bunge, walianza leo wataendelea na kesho. Kwa hiyo, katika pitapita yenu huko mpite pia.

Nakumbusha kwamba, kesho hiyo hiyo tarehe 16 Agosti, 2008, ndiyo kuna mashindano yale ya michezo ya kirafiki kati ya timu ya miguu ya Bunge na Mtwara Veterans, halafu na timu ya Netbal ya Wabunge na Dodoma Veterans; hiyo itakuwa saa kumi jioni katika viwanja vya michezo vya Jamhuri. Halafu pia kesho hiyo hiyo saa moja jioni, kutakuwa na tafrija katika Ukumbi wa Basement hapa Bungeni mnapafahamu. Watakaota burudani ni Bendi ya Twangapepete na Hama-q. Burudani hii imeletwa kwa hisani ya Kampuni ya Zain. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge, mnakaribishwa kwa shughuli zote.

Napenda kuwashukuru sana, kwa wiki hii tumefanya kazi nyingi na nzuri. Ninaomba muwe na weekend njema na ninawashukuru sana kwa ushirikiano mliotupa. Kwa hiyo, naahirisha Kikao cha Bunge mpaka Siku ya Jumatatu saa tatu asubuhi.

*(Saa 01.09 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Jumatatu,  
Tarehe 18 Agosti, 2008 Saa Tatu Asubuhi)*